# Nipashe

Jumatatu Aprili 8, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579886

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




UKURASA 13



## Asimulia alivyotumia mil. 200/- kutibia TB, saratani 'bandia'

UKURASA 2

# WIKI NGUMU KWA MAFISADI

- Udhibiti wa mapato na matumizi ya serikali
- Wizi wa fedha za wizara, idara na mashirika ya umma
- Mchwa wa fedha za halmashauri mbalimbali nchini
- Malipo kwa watu na miradi 'hewa' maeneo mbalimbali
- Uendeshaji na usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii
- Taarifa ya kuongezeka kwa Deni la Taifa

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wakiitikia dua iki-somwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, katika kaburi la Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, katika viwanja vya Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar jana. **Habaru Uk. 5. PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WAZIRI ATUMBUA OC CID KWA TUHUMA ZA RUSHWA**
WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara...

UKURASA WA 3


**VIWANDA UCHENJUAJI MADINI VYATIWA KUFULI**
NAIBU Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, amevifunga viwanda vya uchenjuaji wa madini 15 vilivyopo wilayani...

UKURASA WA 12

**MAPYA YAIBUKA KESI MAUAJI MWANAFUNZI**
UPANDE wa mashtaka katika kesi ya mauaji ya mwanafunzi wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari ya Scholastica...

## JPM aamuru msako waliofilisi benki

UKURASA 2



## ACT sasa yaibomoa ngome CUF

UKURASA 5

**MICHEZO** SABABU SIMBA KUTOKA SARE NA TP MAZEMBE UK. 18

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wiki ngumu kwa mafisadi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

NI wiki ngumu kwa mafisadi! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na juma hili kuwa maalum kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwasilisha ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyoanzisha Ofisi ya CAG, inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha nne (4) cha ibara hiyo, baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika, wawasilishe taarifa hiyo kwenye mkutano wa kwanza wa Bunge utakaofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika mkutano huo kabla ya kupita siku saba tangu siku ulipoanza.

CAG, Prof. Mussa Assad, ameshakabidhi ripoti hiyo kwa Rais.

Mkutano wa Bunge la Bajeti unaoendelea jijini Dodoma ulianza Jumanne Aprili 2, mwaka huu, hivyo ripoti ya ukaguzi ya CAG kwa mwaka wa fedha 2017/18 inapaswa kuwasilishwa bungeni ndani ya siku tatu kuanzia leo, yaani ndani ya siku saba tangu kuanza kwa mkutano (siku za mwishoni mwa wiki na sikukuu hazihesabiki).

Ripoti ya mwaka ya CAG imekuwa ikiangazia hali ya Deni la Taifa na uhimilivu wake, udhibiti wa mapato na matumizi ya serikali, wizi wa fedha za wizara, idara na mashirika ya umma, 'mchwa' wa fedha za halmashauri mbalimbali nchini, malipo kwa watu na miradi 'hewa' pamoja na uendeshaji na usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Miongoni mwa hoja ambazo zinatarajiwa kuwa gumzo katika ripoti ya CAG ya mwaka 2017/18, ni madai ya uwapo wa ufisadi katika mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo sasa ipo miwili baada ya kuundwa kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) uliounganisha mifuko minne ya PSPF, PPF, LAPF na GEPF.

INAENDELEA UK. 8

## Asimulia alivyotumia milioni 200/- kutibia TB, saratani 'hewa'

**Na Romana Mallya**

MHASIBU Baltazar Saunaky (61), amesimulia namna ambavyo ametumia Sh. milioni 200 kutibu ugonjwa wa saratani na kifua kikuu (TB) wakati alikuwa haumwi maradhi hayo na sasa anaumwa ugonjwa ambao utamgharibu Sh. milioni 57.5 ambazo hana.

Saunaky ni mkazi wa Kijenge mkoani Arusha na baada ya taarifa yake kurushwa kwenye moja ya mitandao ya kijamii, Nipashe ilimtafuta na ndipo alipobainisha kuwa alianza kusumbuliwa na uti wa mgongo tangu mwaka 1999.

"Nilipofanyiwa vipimo katika hospitali moja hapa Tanzania, niliambiwa nina kifua kikuu, hivyo nikaanza kutumia dozi kwa miezi sita. Hali ilivyoendelea kuwa mbaya nikaenda Nairobi Kenya ambako vipimo nilivyofanyiwa vilionyesha nina saratani na iko kwenye hatua mbaya nikaanza matibabu," alisema.

"Tangu wakati huo nimekuwa nikijitibu na nimetumia zaidi ya Sh. milioni 200 kutibu maradhi hayo ambayo niliambiwa na wataalamu wa hospitali Tanzania na Kenya kuwa ninayo, lakini mwaka 2016 nilipoenda India na kupimwa nilionekana sina hayo magonjwa niliyoambiwa awali wakaniambia nasumbuliwa na uti wa mgongo na nyonga," alisema.

Akisimulia zaidi, Saunaky ambaye ni baba wa watoto wawili na mke, alisema alianza kupata maumivu ya mgongo mwaka 1999 na awali alichukulia ni tatizo la kawaida hivyo akawa anameza dawa za kutuliza maumivu.

"Nilitumia dawa za kutuliza maumivu kwa muda lakini hali haikubadilika zaidi ilikuwa ikiongezeka,

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli akizungumza na wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi wanaosoma katika Shule ya St. William iliyopo Mbinga mkoani Ruvuma. Rais amewachangia watoto hao kiasi cha shilingi milioni tatu. **PICHA: IKULU**

## JPM aamuru msako waliofilisi benki

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuwasaka na kuwafikisha katika mikono ya sheria watu wote waliohusika katika kuifilisi iliyokuwa Benki ya Mbinga Community.

Amewataka viongozi wa mkoa wa Ruvuma, wakiwamo Mkuu wa Wilaya, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Mkuu wa Polisi wa Wilaya kulishughulikia suala hilo kwa kuhakikisha wahusika wanapatikana.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Mbinga wakati akiweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa mradi wa Barabara ya Mbinga-Mbamba Bay yenye urefu wa kilometa 66, inayojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 134.712.

"Nafahamu kwenye miaka ya nyuma kulikuwa na benki hapa, lakini niliambiwa walioimaliza ni watu wa hapa hapa. Wananchi walilima kahawa vizuri, mkaanzisha benki yenu, benki ikaisha hadi ikafilisika," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Ninachojiuliza, hawa walioifilisi benki hii wako wapi? Je, vyombo vya ulinzi na usalama vimechukua hatua gani? Je, kuna ukaguzi gani umefanyika kwa hawa watu waliowapa imani kubwa ya kuanzisha chombo hiki kilichokuwa kinawasaidia wakulima hadi kikawafia mikononi mwao?"

"Ninawaomba viongozi wa hapa DC (Mkuu wa Wilaya), wakuu wa vyombo vya Takukuru, OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa), Mkuu wa Mkoa, tuanze kushungulikia suala hili," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alilazimika kutoa maagizo hayo baada ya Mbunge wa Mbinga, Sixtus Mapunda, kumuomba Rais Magufuli kuwashughulikia watu waliohusika kuifilisi benki hiyo.

"Kwa sababu matatizo ambayo yanapaswa kutatuliwa na watu wa chini hayatatuliwi hadi Rais aje. Kwa hiyo mbunge nimekuachia wewe, ulifuatilie pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama kwa nini benki hii imefilisika, nani ameifilisi?" Alisema.

Rais Magufuli alisema ameyazungumza hayo ili kukata mzizi wa fitina kwa sababu kuna watu walifanya mambo ya ajabu nchini kwa kupata utajiri na kutembea kifua mbele, kumbe wametajirika kwa mali za maskini.

Alisema wakulima wa kahawa mkoani Ruvuma wanalima, wanahangaika kwa mwaka mzima, wanaweka mbolea, wanachuma kahawa yao, wanakausha, wanahangaika katika maisha ya umaskini, lakini wanapopeleka sokoni kuuza wanalanguliwa na wajanja.

"Ninafahamu kuna madaraja ya kahawa, daraja la kwanza, la pili, la tatu na bei haiwezi kufanana. Lakini kama kahawa ni bei moja kwa nini mmoja apewa bei ya juu mwingine bei ya chini, inamaana kahawa hii huwa inageuka bei? Ukienda mtu wa ovyo ovyo inakuwa bei ya chini, ukienda mtu wa daraja fulani bei inakwenda juu," alisema na kuongeza:

"Sasa nilitegemea mbunge an-

INAENDELEA UK. 8


## KUMBUKUMBU

TAREHE 5/4/2019 ULITIMIZA MWAKA MMOJA TANGU UITWE NA MWENYEZI MUNGU. INGAWA BABA YETU HAUPO NASI KIMWILI LAKINI KIROHO TUPO PAMOJA KATIKA SALA NA MAOMBI. ULIKUWA NGUZO IMARA KATIKA MAISHA YETU, ***HEKIMA NA BUSARA ZAKO TUTAZIKUMBUKA DAIMA.*** TUNAMSHUKURU MWENYEZI MUNGU KWA MAISHA YAKO KWETU, HAKIKA PENGO ULILOLIACHA HALITAZIBIKA KAMWE.



MZEE GERALD MGEUSA NYINGE
1939 – 2018

UTAKUMBUKWA DAIMA NA ***MAMA YETU ISABELLA, WANAO EVANS, REGINALD, LILIAN, ERIC, LEVINA, DEOGRATIUS, ANNACLETUS, IRENE, WAJUKUU ZAKO, NDUGU, MAJIRANI NA MARAFIKI ZAKO NA WAKWE ZAKO.***

**RAHA YA MILELE UMPE EWE BWANA NA MWANGA WA MILELE AKUANGAZIE, UPUMZIKE KWA AMANI**

115161802

# Waziri atumbua OC CID kwa tuhuma za rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, kumsimamisha kazi Mkuu wa Upelelezi wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Mbogwe (OC CID) mkoani Geita, pamoja na Mkaguzi wa Jeshi hilo kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata za Ilolangulu na Busabaga wilayani Geita, Lugola alidai polisi hao waliomba na kupokea rushwa ya shilingi milioni nne kutoka kwa wananchi wa kata hizo ambao walikuwa wanataka kuwaombea dhamana ndugu zao, ndipo polisi hao wakaomba fedha kiasi hicho ili watolewe mahabusu katika Kituo cha Polisi Mbogwe.

Wanadaiwa kupokea rushwa kutoka kwa wananchi hao ni OC CID wa wilaya hiyo, Luitiko Kibanda na Mkaguzi wa Polisi aliyetajwa kwa jina moja la Kessy ambao wananchi hao pamoja na mbunge wao walisema walikabidhi fedha kiasi hicho.

"Wananchi walipitisha mchango kila kaya ili kuwanusuru wenzao na viongozi wao haikutosha wakamwomba mbunge wao akawachangie shilingi laki tano pia wakachukua na hela yao iliyokuwa ni ya kujengea zahanati wakawapelekea polisi, bila hata aibu polisi hawa wakachukua fedha hizo, bila kujali hali za kiuchumi walizonazo wananchi hao," alisema Lugola.

Alisema ni kosa kuwaonea wananchi kwa kuwaomba rushwa kupitia kisingizio cha utoaji wa dhamana, huku sheria ikieleza kwa makosa yanayodhaminika dhamana itolewe kwa mujibu wa sheria na siyo kuwanyanyasa wananchi.

Aidha, Waziri Lugola alitoa onyo kwa Polisi nchini ambao wanawafanya wananchi mtaji kwa kuwabambikiza kesi kisha kuwaomba pesa, kuacha tabia hiyo mara moja na endapo watabainika hatawavumilia, hatawaonea huruma, hivyo sheria itafuata mkondo wake.

Diwani wa Kata ya Ikobe, wilayani humo, Costantine Kwezi, alimwomba waziri kuwasaidia kukamilisha kituo cha polisi katika kata yake na pia kuongeza idadi ya askari kituoni hapo, kwa sababu kituo hicho kina askari mmoja ambaye anazidiwa na majukumu.

Baadhi ya kinamama katika mkutano huo, nao walimwomba waziri huyo kuwasaidia waume zao waliokamatwa kwa kosa la kusingiziwa kuwa ni majambazi kuachiwa huru, kutokana na kukosa fedha za kuhudumia familia na wao wameachwa bila kazi na watoto wadogo.

# Viwanda vya uchenjuaji madini vyatiwa kufuli

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, amevifunga viwanda vya uchenjuaji wa madini 15 vilivyopo wilayani Kahama mkoani Shinyanga, baada ya kubainika kuwapo wizi mpya wa madini kwa kutumia steel wire na kuikosesha serikali mapato.

Pia, amemsimamisha kazi Kaimu Meneja wa Madini Mkoa maalumu wa madini Kahama, Abdurahamani Milandu, baada ya kushindwa kusimamia vema viwanda hivyo vya uchenjuaji wa madini, na kusababisha kuwaibia wateja pamoja na kuikosesha kodi serikali.

Nyongo alivifunga viwanda hivyo juzi baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika viwanda hivyo na kufanikiwa kukamata dhahabu gramu 102.9 ambayo ilikuwa katika mfumo usio rasmi. Baadhi ya wamiliki wa viwanda hivyo huweka steal ware katika mabomba ya mashine za kuchujia kaboni na kuwaibia wateja wao.

Aidha, Nyongo alisema baadhi ya watumishi wa ofisi za madini wilayani hapa sio waaminifu na amebaini kuhusika kuwaibia wachimbaji wadogo katika upimaji wa dhahabu iliyozalishwa katika zoezi la upimaji kwa kutumia mizani yenye ubora.

Pia alifafanua kuwa katika ziara hiyo amebaini uwapo wa mizani ambazo hazijathibitishwa na Wakala wa Vipimo wa Serikali (WMA), huku meneja huyo akiwa amekaa kimya bila kuchukua hatua stahiki dhidi ya baadhi ya wamiliki wa viwanda hivyo, na kusababisha serikali kukosa mapato.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wateja ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alisema baada ya kufikisha mzigo wake katika kiwanda kilichobainika kuweka steel wire, baada ya kupima kaboni zake matokeo yalionyesha atapata dhahabu nyingi, lakini baada ya kuichoma alipata dhahabu kidogo.

Alisema hatua hiyo ilimfanya atoe taarifa kwa maofisa wa serikali waliokuwapo katika kiwanda hicho kisha kuamu kuyakata mabomba ya mashine hizo na kufanikiwa kupata steel wire hizo zikiwa na dhahabu nyingi.




//KUWA UNSTOPPABLE. Benki popote na SC Mobile Tanzania App.
Benki ya kidigitali kiganjani

SC Mobile ni rahisi, haraka na salama kubenki mahali popote. Unaweza kuokoa kiasi kingi cha fedha kwa kupata punguzo la asilimia 50 katika gharama za miamala ya kibenki unayofanya kupitia SC App. Utapata taarifa za miamala yako bure kwa miezi 3.

Ipakue leo na ujionee njia mpya ya kubenki!

Download on the App Store | GET IT ON Google Play

sc.com/tz

Here for good

215162002

*Vigezo na Masharti Kuzingatiwa. Standard Chartered is regulated by the Bank of Tanzania.

# STANBIC BANK TANZANIA

## Tariff Guide Uhuru Banking

### Effective as of 8th May 2019

| TRANSACTION/SERVICE | | LOCAL CURRENCY | FOREIGN CURRENCY | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MONTHLY MANAGEMENT FEES** | **DESCRIPTION** | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Uhuru -Personal Current Account | Charged Monthly | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Hatua Account | Charged Monthly | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Pure Savings Account | NO management fee if minimum balance is maintained | NO management fees if balances is above TZS 50,000. Else, TZS 2,000 fee will apply. | NO management fees if balance is above $100. Else, $1.18 fee will apply. | NO management fees if balances is above EUR100. Else, EUR 1.18 fee will apply. | NO management fees if balances is above GBP 100. Else, GBP 1.18 fee will apply. | NO management fees if balances is above ZAR 300 Else, ZAR 17.7 fee will apply. |
| Cooperate and Investment banking | Charged Monthly | 48,000.00 | 20.00 | 18.01 | 16.00 | 290.01 |
| Commercial banking Tier 1 | Charged Monthly | 64,900.00 | 38.94 | 30.68 | 23.60 | 361.08 |
| Commercial banking Tier 2 | Charged Monthly | 35,400.00 | 21.24 | 16.99 | 12.74 | 196.82 |
| Biashara Direct | Charged Monthly | 15,000.01 | 10.62 | 8.26 | 7.08 | 97.94 |
| Private Banking | Charged Monthly PAYT | 29,500.00 | 17.70 | 14.16 | 10.62 | 164.02 |
| Private Banking | Charged Monthly BUNDLE | 53,100.00 | 31.86 | 24.78 | 18.88 | 295.00 |
| **TRANSACTION SERVICES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.)-CURRENT ACCOUNT | Fee could be a % charge on withdrawal (with min charge per withdrawal) or lat charge per transaction. | 4,088 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 125,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1 % min 8 | For FCY withdrawals 1% min 14.16 | For FCY withdrawals 1% min 14.16 | For FCY withdrawals 1% min 141.6 |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.) - PURE SAVE | One free cash withdraw per month, more than that charge will apply | 5,900 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 118,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1.18 % min 10.62 | For FCY withdrawals 1.18% min 21.24 | For FCY withdrawals 1.18% min 21.24 | For FCY withdrawals 1.18% min 212.4 |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.) - HATUA ACCOUNT | One free cash withdraw per month, more than that charge will apply | 10,000 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 118,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1.18 % min 10 | NA | NA | NA |
| Cash Deposit Charge | Fee to be charged to notes below $50 | FREE | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. For all FCY currency. | FREE | FREE | FREE |
| Cheque payments to other banks | When our customer pays through Cheques to third party banks | 950.01 | 0.96 | 0.96 | 0.96 | 6.34 |
| Cheque Deposit | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Unpaid Cheque(Insuficient Fund) | Flat fee per unpaid item | 100,000.01 | 100.01 | 100.01 | 100.01 | 666.68 |
| Account Closure | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Cheque Book | | 450 | 0.46 | 0.46 | 0.46 | 3.01 |
| **CARDS AND ATM FEES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Card expired | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card New | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card Not working | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card compromised | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| POS Purchase ( Domestic) | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Annual card fees | UHURU BANKING | 10,000 | 10.01 | 10.01 | 10.01 | 66.67 |
| Annual card fees | PRIVATE BANKING | 30,000 | 30.01 | 30.01 | 30.01 | 200.01 |
| Secondary Card fee | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Card Damaged | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Card lost/Stolen | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Card Name Change | | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| Cash withdrawal @ other bank ATM (in another country) | | 8,000.01 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 53.34 |
| Internationa card access fee | | 8,000.01 | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent |
| Uncollected cheque/CARDS fees ( Two month) | | 10,000 | 10.01 | 10.01 | 10.01 | 66.67 |
| POS Purchase ( International) | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Declined ATM cash withdrawal no funds - Stanbic/Standard Bank ATM (internationally) | | 2,500.01 | 2.50 | 2.50 | 2.50 | 16.67 |
| Cash withdrawal @ other bank ATM (in country) | | 1,000 - 400,000 = 2800 400,001-above=4000 | 1 - 170 = 2.8 171-above=4 | 1 - 170 = 2.8 171-above=4 | 1 - 170 = 2.8 171-above=4 | 1 - 2,000 = 28 2,001-above=40 |
| Declined ATM cash withdrawal no funds - other bank's ATM (in country) | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Balance enquiry on other Banks ATM/ CCC and at Branch | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Cash withdrawal @ own ATM (in country) | | 950.01 | 0.96 | 0.96 | 0.96 | 6.34 |
| Mini stat at own ATM | | 900.01 | 0.91 | 0.91 | 0.91 | 6.01 |
| Declined ATM cash withdrawal no funds (own ATM) | | 700.01 | 0.71 | 0.71 | 0.71 | 4.67 |
| Pin management | | 700.01 | 0.71 | 0.71 | 0.71 | 4.67 |
| Balance enquiry own ATM | | 300 | 0.31 | 0.31 | 0.31 | 2.01 |
| **USSD/WAP AND INTERNET BANKING** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Fee- Top-up Other | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee- Top-up Self | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee- Self Funds | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Biller Payment | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Monthly Subscription | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Bank To Wallet | | 1,000 - 25,000 =1500 25,001 - 100,000 = 2250 100,001 - 250,000 = 3000 250,001-500,000=3,750 500,000-1,000,000=4,500 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Transfers Of Money Outside Stanbic(Express) | | 8,000.01 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Transfers Of Money Outside Stanbic(Normal) | | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| Transfers Of Money 3rd party Within Stanbic | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Mini statement | | 500 | 0.51 | 0.51 | 0.51 | 3.34 |
| Balance Inquiry( wap and ussd charged) | | 350.01 | 0.35 | 0.35 | 0.35 | 2.34 |
| **OTHER FEES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Statement (Monthly) OTC | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| E statement | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| MT940 | Monthly Statement | 75,000.01 | 75.00 | 75.00 | 75.00 | 500.00 |
| Interim Statement (Over The Counter)( More Than One Month But Not Exceed 3 Month) | | 5,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| Certificate of Balance | | 42,000.01 | 42.01 | 42.01 | 42.01 | 280.00 |
| Introduction letters (international banks) | | 55,000 | 55.01 | 55.01 | 55.01 | 366.67 |
| Certificate covering interest paid | | 55,000 | 55.01 | 55.01 | 55.01 | 366.67 |
| Certificate of Balance | | 42,000.01 | 42.01 | 42.01 | 42.01 | 280.00 |
| Confirmation Auditor List | | 130,000.01 | 130.00 | 130.00 | 130.00 | 866.67 |
| Search Fees For Copies | | 60,000 | 60.00 | 60.00 | 60.00 | 400.01 |
| Fee- OTC History Statements | | 60,000 | 60.00 | 60.00 | 60.00 | 400.01 |
| **PAYMENTS** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Salary Payments EFT - Manual | per person | 5,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| Salary for TISS - Manual | per person | 10,000 | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent |
| Fee- Standing Instruction | SI ESTABLISHMENT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Standing Order Amendment | SI AMMENDMENT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI THIRD PART ACCOUNT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI -OTHER BANK ACCOUNT | 40,000.01 | 40.00 | 40.00 | 40.00 | 266.67 |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI-OWN ACCOUNT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI-UNPAID STANDING ORDER (FAILURE) | 50,000.01 | 50.01 | 50.01 | 50.01 | 333.34 |
| Stop Payment Orders | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Inter Account Transfer(3Rd Party) OTC | | 5,000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| Bank Cheque Issued | | 40,120 | 40.12 | 40.12 | 40.12 | 267.47 |
| Counter Cheque (OTC) | | 15,000 | 15.00 | 15.00 | 15.00 | 100.00 |

215162902

# ACT sasa yaibomoa ngome CUF

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIONGOZI wote wa Chama cha Wananchi CUF Wilaya ya Shinyanga Mjini, wakiwa na wanachama wao 200 wamekihama chama hicho na kujiunga cha ACT-Wazalendo, kwa madai ya kutokubali kuongozwa na Prof. Ibrahimu Lipumba.

Wamesema hawana imani na Prof. Lipumba kwa kuwa aliwakimbia siku chache kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Hayo yalibainishwa na aliyekuwa Katibu wa CUF Wilaya ya Shinyanga Mjini, Saidi Juma Issa, wakati wakijivua uongozi na kujiunga rasmi ACT-Wazalendo. Akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema wameamua kuondoka kwenye chama hicho kwa hiari yao bila ya kushawishiwa na mtu yeyote.

Alisema hawakuridhishwa na maamuzi yaliyotolewa ya Mahakama ya kukabidhiwa chama Prof. Ibrahimu Lipumba, kwa kuwa hana sifa tena ya kuwa kiongozi kwa kuwa aliwakimbia wakati wakiwa kwenye kipindi cha mapambano ya kushika dola, na kusababisha chama kuonekana hakina msimamo.

"Baada ya Lipumba kukabidhiwa chama tena, sisi kama viongozi wa CUF Shinyanga Mjini tukiwa na kamati tendaji ya watu 12, tukaona hatuna haja tena ya kuendelea kupigania chama ambacho kinaongozwa na kiongozi ambaye siyo shupavu kwenye mapambano, tukaona ni bora tuhamie upande wa pili," alisema Issa.

"Hivyo tunaomba chama cha ACT-Wazalendo mtupokee sisi viongozi pamoja na wenzetu ambao wapo 200, na wengine wengi watazidi kuja kwa kuwa kwa leo wamepata hudhuru, tushirikiane katika mapambano ya kisiasa ili tupate kushika dola na kuwatumikia wananchi," aliongeza.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Wilaya ya Shinyanga Mjini, Twaha Makani, aliwapokea wanachama hao wapya kutoka CUF, huku akiwataka waifuate misingi na katiba ya chama hicho, ili kukijenga chama ambacho kwa sasa ndicho kinaaminiwa na Watanzania kuwaletea ukombozi.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT-Wazalendo, Nyangaki Shilungshela, aliwatahadharisha wanachama hao wapya kutokuwa na majungu na makundi, akisema yamekuwa yakisababisha migogoro katika vyama.

## Karume akumbukwa kwa dua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZANZIBARI jana waliadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abedi Amani Karume, kwa kumwombea dua maalum wakiongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein.

Shughuli hiyo ya maadhimisho ya miaka 47 tangu kuuawa kwa kiongozi huyo, ilifanyika katika ofisi kuu za CCM Kisiwandui.

Dua hiyo hufanyika Aprili 7 ya kila mwaka tangu Mzee Karume alipouawa mwaka 1972.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa dua hiyo, mtoto wa marehemu Karume ambaye pia ni Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Zanzibar, Balozi Ali Abeid Karume, aliwataka viongozi kuongoza kwa kuzingatia maslahi ya wananchi kama alivyokuwa akifanya Mzee Karume.

Alisema baadhi ya viongozi huongoza kwa kuzingatia maslahi yao binafsi bila ya kuwajali wananchi.

Aliishauri serikali kutilia mkazo siku hiyo ya kumbukumbu ili vijana kuweza kujifunza historia ya kiongozi huyo pamoja na fikra na mtazamo wake chanya katika kuleta maendeleo ya nchi.

Aliwapongeza Rais John Magufuli na Dk. Shein kwa kutekeleza kwa vitendo falsafa ya Mzee Karume katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, alisema kitu cha msingi katika kumuenzi kwa vitendo mzee Karume ni kuimarisha Muungano wa Tanzania.

Dua hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali na wastaafu na baada ya dua hiyo waliweka mashada ya maua katika kaburi la kiongozi huyo.


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **INTERNATIONAL BUSINESS CENTRE** | | | | | | |
| **INWARD PAYMENT** | | | | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT | | $ 10 | $10 | | | |
| Drafts/Bills (Clean Bill Collection) | | $150 | $150 | | | |
| Bills and drafts negotiated and subsequently returned unpaid | | $150 | $150 | | | |
| **OUTWARD PAYMENTS** | | | | | | |
| SWIFT Charges for tracing remittances | | $50 | $50 | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT | Oversee charge is charged depending on made of payment customer has choose. | 0.3% of Value Min $50, Max 150 (excluding oversee charge of $29.5) | 0.3% of Value Min $50, Max 150 (excluding oversee charge of $29.5) | | | |
| Cancellation of TT/Recall of funds | | $75 | $75 | | | |
| Amendment TT | | $75 | $75 | | | |
| Transfers though TISS | | TZS10 000 | Equiv 10 000 | | | |
| MT101 Issuance | | 10,000.00 | 1.18% of the amount min $59, Max $236 | 1.18% of the amount min 50, Max $200 | 1.18% of the amount min 40, Max 160 | 1.18% of the amount min 560, Max 2240 |
| Drafts/Bills/Cheques | | 1.18% of the amount min 100 000, Max 400,000 | 1.18% of the amount min $59, Max $236 | 1.18% of the amount min 50, Max $200 | 1.18% of the amount min 40, Max 160 | 1.18% of the amount min 560, Max 2240 |
| **BILLS FOR COLLECTION** | | | | | | |
| **OUTWARD** | | | | | | |
| Documentary Bills for collection (Payment) | | SWIFT charge $35 | SWIFT charge $35 | | | |
| Doc handling fee | | $150 | $150 | | | |
| Courier Services | | $50 | $50 | | | |
| Tracer Fees | | $50 | $50 | | | |
| Clean bills for collection | | $150 | $150 | | | |
| **INWARD** | | | | | | |
| Documentary Bills for collection (doc handling) | | $125 | $125 | | | |
| Clean bills for collection | | $125 | $125 | | | |
| Delivery of documents free of payments, in terms of remitting bank's instructions | | $50 | $50 | | | |
| Avalizing | | 1% min $150 however subject to adequate Security and approval | 1% min $150 however subject to adequate Security and approval | | | |
| Negotiation fee | | $50 | $50 | | | |
| Confirmation | | $50 | $50 | | | |
| Courier charges | | $50 | $50 | | | |
| **BOL** | | | | | | |
| Telegraphic Transfers | | 0.3% of Value Min 50.00, Max 150.00 | | | | |
| Local Transfers (RTGS / TISS) | BOL | 8,000.01 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Local Transfers (EFT) | BOL | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| Internal Transfers | BOL | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Payroll On-Us (Within Stanbic) | BOL | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 6.67 |
| Payroll Off-Us - EFT | BOL | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| Payroll Off-Us - TISS | BOL | 8,000.01 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Mobile Bulk Payments | BOL | 1,500.00 | 1.51 | 1.51 | 1.51 | 10.01 |
| BOL Monthly Fee | BOL | 24,000.01 | 24.00 | 24.00 | 24.00 | 160.01 |
| BOL Token Fee (One-Off) | BOL | 65,000.01 | 65.01 | 65.01 | 65.01 | 433.34 |
| Till to bank | Merchant Services | 1.8% | | | | |

215162902

Stanbic Bank Moving Forward™
A member of Standard Bank Group

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tuungane Serengeti Boys nayo ifuzu Kombe la Dunia

JUMAPILI fainali za Mataifa ya Afrika kwa Vijana wenye umri chini ya miaka 17 (Afcon U-17) zitaanza kutimua vumbi nchini, hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwa michuano mikubwa kama hiyo Afrika kufanyika Tanzania.

Katika michuano hiyo ambayo itafanyika jijini Dar es Salaam ikipigwa katika viwanja vitatu, Uwanja wa Taifa, Uhuru na Chamazi, Serengeti Boys imepangwa Kundi A pamoja na Angola, Uganda na Nigeria.

Kundi B katika michuano hiyo ambayo itaanza Jumapili Aprili 14-28, linajumuisha timu za Cameroon, Guinea, Morocco na Senegal.

Bila shaka kila timu katika michuano hiyo imepania kufanya vizuri ili kukata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia kwa wachezaji wa umri huo Oktoba mwaka huu nchini Brazil.

Hiyo ni kutokana na timu zitakazoshika nafasi ya kwanza na ya pili kutoka katika kila kundi zitafuzu moja kwa moja fainali hizo za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Brazil.

Kuelekea michuano hiyo ya Afcon U-17, hatuna hofu na maandalizi ya muda mrefu ambayo Serengeti Boys imeyafanya na inayoendelea kuyafanya.

Ni wiki iliyopita tu Serengeti Boys imefanikiwa kuichapa timu bora na imara ya Cameroon U-17 kwa mabao 2-1 kwenye mechi ya michuano maalum nchini Rwanda kwa ajili ya kujiandaa na mashindano hayo ya Afcon.

Mbali na michuano hiyo ya maandalizi nchini Rwanda, pia licha ya kufanya vizuri na kutolewa kwenye michuano ya Uefa Assist iliyofanyika nchini Uturuki Februari mwaka huu, tunaamini ilipata uzoefu na mazoezi yanayostahili kwani ilikutana na timu imara na ngumu. Katika michuano hiyo, Serengeti Boys ilikutana na kupoteza dhidi ya Guinea na wenyeji Uturuki na kisha kuichapa Australia, hivyo kujikuta ikiishia hatua ya makundi.

Kikosi hicho kinachonolewa na Oscar Milambo, kilianza kwa kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Guinea na kisha kuichapa Australia mabao 3-2 kabla ya kukutana na mvua ya mabao 5-0 kutoka kwa wenyeji, Uturuki.

Hakika hayakuwa matokeo mazuri kwa Serengeti Boys ambayo Jumapili itafungua michuano ya Afcon U-17 kwa kucheza dhidi ya Nigeria Uwanja wa Taifa.

Lakini Nipashe tunaamini kupitia michuano hiyo na hii ya mwisho nchini Rwanda, imetoa nafasi kwa kocha Milambo kurekebisha makosa yake hivyo tunategemea matokeo makubwa sasa. Milambo na benchi lake zima la ufundi pamoja na wachezaji tunaamini wamejiandaa vema kuwapa Watanzania raha kwa kuiona Serengeti Boys ikifuzu michuano hiyo mikubwa duniani. Na si kufuzu tu fainali hizo za Kombe la Dunia, bali pia kuhakikisha Kombe hilo la Afcon U-17 linabaki hapa nchini, hiyo ndiyo kiu ya Watanzania wote.

Hivyo, wakati tukiwa na imani kubwa na Serengeti Boys kutekeleza ipasavyo majukumu yake, mashabiki wa soka na Watanzania kwa ujumla hawana budi kutumia vema faida ya michuano hii kufanyika nchini kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kwenda kuishangilia.

Kama ambavyo Uwanja wa Taifa ulijaa wakati Taifa Stars ikicheza mechi ya kuwania kufuzu Afcon 2019 dhidi ya Uganda, ndicho kinachotakiwa kufanyika katika mechi zote itakazocheza Serengeti Boys katika michuano hii.

Kwa kufanya hivyo, hakika Serengeti Boys watakuwa na morali ya hali ya juu wakiamini Watanzania wote wapo nyuma yao hasa ikizingatiwa shabiki wa soka ni mchezaji wa 12 uwanjani.

Matarajio na maombi yetu kama ilivyo kwa Watanzania wote ni kuona Serengeti Boys ikitwaa ubingwa huo wa Afcon na kufuzu Kombe la Dunia nchini Peru, hivyo tunaitakia kila la kheri kuanza na kumaliza kwa mafanikio makubwa katika michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Yanga haiwezi kuishi kwa harambee tu

Na Adam Fungamwango

**WIKI** hii Klabu ya Yanga imefanya harambee mjini Dodoma ya kuichangia timu hiyo ili kujiendesha kiuchumi.

Waheshimiwa wabunge, wanachama na mashabiki wa Yanga wamekuwa kwenye kampeni kabambe ya kuichangia klabu hiyo.

Klabu ya Yanga, moja kati ya klabu chache kongwe hapa nchini inapitia kipindi kigumu cha kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo kumekuwa kukitumika njia mbalimbali ili kuiwezesha klabu hiyo kuendelea kumudu kujiendesha.

Binafsi, sipingi kwa Yanga kuchangishana au kutembeza bakuli kwa sababu moja kati ya njia rahisi zaidi ya kusaidia mtu mwenye matatizo ni kumchangia kwanza amalize shida zake. Kutokana na hali hii Wanayanga popote pale walipo waendelee kuichangia klabu yao kwa hali na mali.

Lakini tuelezane ukweli kuwa klabu kubwa kama ya Yanga haiwezi kuendelea kuishi ama kujiendesha kwa harambee na michango siku zote. Nasema hivi kwa sababu inaweza ikachukuliwa na viongozi wengine kuwa hiyo ndiyo njia rasmi ya Yanga kujiingiza kipato.

Nashauri suala hili lichukuliwe kama la mpito na si la kudumu kwa kuwa halitoweza kuipeleka popote kule klabu kuwa kama hii.

Ni sawa na mtu anayechangiwa aoe au kuolewa na hawezi kuwa kila baada ya muda anachangiwa pesa, bali baada ya kuchangiwa huendelea na taratibu zake za kuiendesha familia yake na si kutegemea tena michango.

**Viongozi wa sasa wa Yanga na hao watakaokuja, wakumbuke kuwa mtaji wa klabu yao ni mashabiki, hivyo wawatumie vema kwa kutengeneza bidhaa na wao kuzinunua, lakini pia kutafuta wadhamini wengine zaidi ya mmoja waliyenaye ili kuzidi kupata pesa nyingi endelevu na zenye hadhi ya kuiwezesha klabu kubwa kama ya Yanga kujiendesha.**

Baada ya harambee na michango yote, wabunge, wanachama na mashabiki wa Yanga watengeneze mfumo ambao utasababisha klabu kuingiza pesa kisayansi na si kufanya mikutano kwa ajili ya kuchangishana.

Klabu ya Yanga si kama Ndanda, Mwadui au African Lyon ambazo hazihitaji kiasi kikubwa cha pesa na badala yake inaweza tu kujiendesha kwa pesa za michango.

Harambee na michango hii haitoweza kusajili wachezaji wenye uwezo wa hali ya juu, au kulipa mishahara minono na posho, hasa kipindi hiki ambacho soka kwa sasa ni ajira na wachezaji bora wamekuwa wakipatikana kwa gharama kubwa mno.

Viongozi wa sasa wa Yanga na hao watakaokuja, wakumbuke kuwa mtaji wa klabu yao ni mashabiki, hivyo wawatumie vema kwa kutengeneza bidhaa na wao kuzinunua, lakini pia kutafuta wadhamini wengine zaidi ya mmoja waliyenaye ili kuzidi kupata pesa nyingi endelevu na zenye hadhi ya kuiwezesha klabu kubwa kama ya Yanga kujiendesha.

Yanga kwa sasa inatakiwa iwe na bajeti angalau nusu ya watani zao wa jadi Simba na si vinginevyo na pesa hiyo haiwezi ikapatikana kwa michango kirahisi na hata kama ikipatikana basi haitakuwa endelevu kwa kuwa asili ya michango huwa ni mara moja au mbili, lakini inapokuwa kama utaratibu huwachosha watu na kuanza kuikwepa hata kama ni ndugu, achilia mbali klabu.

# MJADALA/BARUA

## Ni wakati wa matamasha ya kuwaenzi wasanii wa zamani

**Mhariri**

*TAFADHARI nipatie fursa katika gazeti letu ili niweze kutoa maoni yangu ambayo nina imani yatakuwa yenye manufaa kwa tasnia ya sanaa nchini.*

*Nchi yetu imebahatika kwa muda mrefu kuwa na wasanii maarufu ambao kihistoria walitoa mchango mkubwa wa kuitangaza Tanzania katika medani ya kimataifa, mbali na suala la kuburudisha wananchi wenzao na kutoa ajira kwa watu wa kada mbalimbali.*

*Kwa mfano katika eneo la muziki wa dansi, kuna wanamuziki waliofanya kazi kubwa ya kuitangaza nchi yetu, kama kina Mbaraka Mwinshehe, Marijani Rajabu, Juma Kilaza, Ngorimba wa Ngorimba, kina Mzee Mwinamila na wengineo wengi.*

*Pamoja na kwamba kumbukumbu zao zipo kupitia kazi mbalimbali za muziki walizozifanya, lakini ninaona kama taifa tunaweza kufanya vitu vingine vizuri zaidi vya kuwakumbuka.*

*Ninaomba kupitia kwako Mhariri, kuliomba Baraza la Sanaa Tanzania (Basata) kuwa na utaratibu wa kuandaa matamasha na majukwaa mbalimbali nchini ya kuwakumbuka na kuwaenzi wanamuziki wetu hao wa zamani na wasanii wengine waliofanya kazi kubwa ya kuitangaza nchi hii.*

*Nina imani kwamba hilo likifanyika hata vizazi vya sasa na vijavyo ambavyo havikupata fursa ya kuwaona, zitajifunza zaidi juu ya watu waliolifanyia mengi taifa hili kupitia medani ya sanaa.*

**Lukumayi Justine-Tegeta**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Anayemlaumu Bocco ni mamluki wa soka

**Na Adam Fungamwango**




YUPO rafiki yangu mmoja ambaye aliwahi kuniambia kuwa kuna baadhi ya mashabiki wameanza kupenda timu badala ya kupenda soka kwanza.

Nilipomuuliza ana maana gani, akaniambia kuwa ili mtu ajue mambo mengi kuhusu soka, inapaswa kwanza awe mwanamichezo au mpenda soka, halafu baadaye ndipo achague timu atakayoishabikia, iwe nchini au nje ya nchi.

Shabiki huyo anakuwa anajua vitu vingi kuhusu soka kwa sababu habebwi na mihemko ya ushabiki wake, bali uhalisia wa mchezo wenyewe.

Lakini kuna baadhi ya mashabiki ambao anadai wao walipenda kwanza timu badala ya mchezo wenyewe, ni wale ambao hawajui kitu chochote kuhusu soka, ila anachojua ni timu yake tu na anachotaka ishinde tu.

Hawa hawajui kama kuna siku wachezaji mpira unawakataa, hawajui kuna bahati kwenye soka, hajui kama mchezaji anaweza kufanya kosa lolote uwanjani. Anachotaka yeye ni mchezaji wa timu pinzani tu afanye makosa, lakini si wa timu yake.

Hili limeonekana baada ya mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ya Simba dhidi ya TP Mazembe iliyopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Straika wa Simba, John Bocco alikosa penalti dakika ya 59 na timu yake kutoka sare ya bila kufungana.

Baadhi ya mashabiki wa Simba wameonekana kumtupia lawama straika huyo kutokana na kukosa mkwaju wa penalti kana kwamba alifanya makusudi.

Mashabiki hao wanashindwa kukumbuka kuwa Bocco ndiye mpigaji penalti namba moja wa Simba na hajawahi kukosa tangu aingie kwenye klabu hiyo akitokea Azam FC. Hata huko nako alikuwa ndiye mpigaji wa penalti mkubwa.

Ni Bocco huyu huyu ndiye aliyefunga penalti zote za Simba kwenye Ligi Kuu, lakini pia kwenye michuano hii hii dhidi ya Mbabane Swallow jijini Dar es Salaam na Nkana FC nchini Zambia. Na ndiyo maana hakuna mtu yeyote aliyekuwa na wasiwasi alipokwenda kupiga.

Lakini baada ya kukosa imekuwa nongwa, kwa kuwa kila mtu anaongea lake. Wengine wanadai angempa Erasto Nyoni, wengine angepewa Haruna Niyonzima, lakini wapo wanaosema kuwa ile penalti angepewa Meddie Kagere.

Mashabiki hao hao wanaosema hayo, kama ingetokea hao wakakosa, wangegeuka tena na kusema ni kwa nini wamepewa wachezaji hao wakati siku zote mpiga penalti rasmi anaeleweka kuwa ni Bocco.

Ifike wakati mashabiki wa soka hasa wa Tanzania waache lawama zisizokuwa na kichwa wala miguu na badala yake wawatie moyo wachezaji wao hasa wanapokuwa kwenye wakati mgumu kama huu.

Tunaona hata kwenye Ligi za Ulaya wachezaji maarufu na tegemeo wakikosa mikwaju ya penalti.

Hata kwenye Kombe la Dunia, kina Asamoah Gyan wa Ghana na Roberto Baggio wa Italia waliwahi kukosa penalti na kuzikosesha nchi zao nafasi ya kusonga mbele pamoja na taji.

Hata Lionel Messi na Cristiano Ronaldo nao wameshawahi kukosa penalti, lakini pamoja na kukosa bado wanaendelea kupewa nafasi ya kubeba jukumu hilo la penalti na wanafunga.

Kwa maana hiyo, Bocco si mchezaji wa kwanza duniani kukosa penalti na hatokuwa wa mwisho, lakini pia hatokuwa akikosa zingine atakazokuwa akipiga siku za usoni.

Je, kama huyo huyo Bocco wanaomlaumu leo, akawa ndiye mfungaji wa bao huko Lubumbashi mwishoni mwa wiki timu hizo zitakaporudiana, litakaloipeleka Simba nusu fainali watafanyaje?

Ndiyo watageuka sasa na kumsifia? Ndiyo watambeba juujuu timu itakapowasili Uwanja wa Ndege na kumwita shujaa wakati wiki moja iliyopita walikuwa wakimshutumu? Na huo utaitwa unafiki.

Na hata yeye hatojisikia vizuri. Mashabiki wa kweli wa soka wanatakiwa wakishinda wafurahi kwa pamoja na wachezaji na viongozi wao na wakifungwa wanaungana pia kuhuzunika pamoja na si kuanza kunyosheana vidole kwa kutupiana lawama.

Mashabiki wa klabu za soka Bongo wanatakiwa wakubaliane na matokeo yoyote wanayopata kwenye timu zao na kuchukulia kama ni kawaida tu kwenye mchezo na si kupeleka lawama nyingi kwa wachezaji au viongozi kwa sababu hakuna timu yenye haki ya kushinda kuliko nyingine.




## Wiki ngumu kwa mafisadi

INATOKA UK. 2

Hoja nyingine zinazotarajiwa kuwa gumzo kwenye ripoti hiyo ya CAG ni ukuaji wa Deni la Taifa na uwezo wa nchi kukopesheka, uwapo wa 'mchwa' wa fedha za maendeleo katika halmashauri mbalimbali nchini na hali ya ununuzi na madeni kwenye taasisi za serikali.

**DENI LA TAIFA**

Kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikimtaka CAG kufanya ukaguzi maalum (special audit) wa Deni la Taifa na kupeleka taarifa ya ukaguzi huo bungeni ili kujadiliwa baada ya kubaini deni hilo limekua maradufu kutoka 2010 hadi 2015.

Wakati wa Bunge la Bajeti mwaka jana, Naibu Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, David Silinde, alidai hali ya Deni la Taifa inatisha na Bunge linapaswa kushtuka.

**MIFUKO YA HIFADHI**

Kumekuwa na madai ya kuwapo kwa ufisadi wa fedha katika mifuko ya hifadhi ya jamii kutokana na uwekezaji kwenye miradi isiyo na faida na matumizi mabaya ya fedha yanayodaiwa kufanywa na bodi za mifuko hiyo. Ripoti ya CAG ya mwaka 2017/18 inatarajiwa kuanika ukweli kuhusu tuhuma hizo.

**MCHWA FEDHA ZA MAENDELEO**

Tuhuma za kukosekana kwa uadilifu katika matumizi ya fedha za maendeleo zimezikumba halmashauri nyingi, huku baadhi ya watendaji wake wakitumbuliwa.

Mchwa wa fedha za maendeleo walibainika katika ripoti zilizopita za CAG kuhusu halmashauri mbalimbali, hivyo macho na masikio ya wengi yanatarajiwa kuelekezwa kwenye changamoto hiyo.

**MALIPO, MIRADI HEWA**

Ripoti ya CAG pia inatarajiwa kuwa na taarifa za malipo yaliyofanywa kwa miradi ambayo ama haipo au haijatekelezwa.

Katika ufuatiliaji wake, Wizara ya Maji imekuwa ikibaini malipo ya mamilioni ya shilingi kwa kazi ambazo hazijatekelezwa.

**NANI ATATOA MUKHTASARI?**


Wakati ripoti ya CAG ikitarajiwa kuwasilishwa mwanzoni mwa wiki hii, bado haijafahamika kama CAG atatoa mukhtasari wa ripoti yake kwa waandishi wa habari kama ambavyo alikuwa anafanya miaka iliyopita.

Ilikuwa imezoeleka kuwa, mara baada ya mawaziri husika kuiwasilisha ripoti bungeni, CAG alikuwa anakutana na waandishi wa habari na kueleza kwa kifupi kilichomo ndani ya ripoti yake.

Kutokana na Bunge kuazimia kutofanya kazi na CAG Assad, mwaka huu kukawa na utaratibu tofauti wa utoaji mukhtasari wa ripoti hiyo.

Lakini, Spika Job Ndugai ameshaweka wazi kuwa Bunge litaendelea kufanya kazi na Ofisi ya CAG isipokuwa haliko tayari kushirikiana na Prof. Assad ambaye ni mkuu wa ofisi hiyo.

## JPM aamuru msako



INATOKA UK. 2

geniambia waliokuwa wanawadhulumu wakulima kahawa yao, lakini anataka mimi nianze kufuatilia ambaye nilikuwa Dar es Salaam, wakati yeye anaishi huku huku."

Rais Magufuli (pichani), alimtaka mbunge huyo kuwataja watu waliohusika kuwadhulumu wananchi kwa kununua kahawa kwa bei ya chini.

Kuhusu barabara hiyo, Rais Magufuli alisema itagharimu Sh. bilioni 134.712 na itakuwa na urefu wa kilometa 66.

Alisema barabara hiyo imekuwa ya gharama kubwa kwa sababu ya kona katika milima, ambapo baadhi ya milima itapasuliwa, itachongwa ili barabara iwe nzuri, magari yapite na ajali zipungue.

## Asimulia alivyotumia milioni 200/-

INATOKA UK. 2

nilikwenda hospitali tofauti tofauti na mwisho wa siku nilipata majibu kutoka hospitali moja kuwa nina tatizo la TB kwenye uti wa mgongo ndipo nilipoanza kunywa dawa kwa muda wa miezi sita," alisema.

Alisema baada ya miezi sita kuisha, hali haikubadilika kwa kuwa aliendelea kupata maumivu makali kwenye uti wa mgongo na mwili ulivimba na kukosa nguvu na mwisho wa siku alishindwa kutembea na ndipo alipoamua kwenda Kenya kwa matibabu zaidi.

"Wataalam wa hospitali ya Nairobi, Kenya waliponifanyia vipimo vya TB na vingine vilionyesha sina TB, bali nina saratani ambayo ilikuwa imeshasambaa mwilini na mara moja nikaanza matibabu ya ugonjwa huo," alisema.

Alisema alikaa Kenya kwa miezi mitatu akiendelea na matibabu ikiwamo kupigwa mionzi na baada ya hapo alirudi Tanzania na akawa anahudhuria kliniki ya saratani kila mara Nairobi, ambako aliendelea na matibabu ya saratani kuanzia mwaka 2002 hadi 2005.

"Niliona hali haibadiliki na ukiwa mgonjwa hasa kwa magonjwa makubwa kama haya, maumivu makali niliyokuwa nayapata niliona nitafute tiba mbadala nikaanza kutumia dawa za asili za kichina za aina tofauti ili kuondoa sumu mwilini kwa sababu kinga ya mwili kwa mujibu wa wataalam wa afya, zilikuwa zimeshuka sana," alisema.

Alisema wakati wote akiugua alikuwa ni mfanyakazi kwenye kampuni binafsi iliyopo Arusha na mwaka 2012 akiwa kazini alidondoka na kuvunjika nyonga ya kushoto na baada ya muda aliachishwa kazi.

"Imekuwa ni mikosi juu ya mikosi wakati natafuta ufumbuzi wa maradhi yaliyokuwa yakinikabili kipindi hicho, nyonga ya kushoto ikavunjika hivyo nilifanyiwa opresheni na kuwekewa chumba ambacho hadi sasa kipo ingawa siwezi kutembea nacho kwa sababu kinaniumiza," alisema.

Alisema mwaka uliofuata nyonga ya mguu wa kulia nayo ilipata shida na vipimo vilivyofanyika Nairobi vilionyesha imesababishwa na saratani.

"Nilianza tiba ya mionzi ambayo iliendelea hadi mwaka 2014, wakati wote nikawa ni mtu wa kulala kitandani kwa sababu dawa nilizokuwa nazitumia zilisababisha matatizo mengine ya mifupa," alisema.

Alisema baada ya hali kuwa mbaya mwaka 2015, aliamua kwenda India na alivyofanyiwa vipimo, ilionekana hakuwa na saratani wala TB bali tatizo liko kwenye pingili za uti wa mgongo na nyonga.

"Kwa kweli wakati napewa majibu hayo nilikuwa nimeshatumia Sh. milioni 200 za matibabu ya magonjwa ya awali niliyoambiwa ninayo, nilikuwa nimeuza mali zangu yakiwamo magari mawili niliyokuwa nayo," alisema.

Alisema safari ya kuelekea India alichangiwa na wasamaria wema kutokana na hali aliyokuwa amefikia baada ya matibabu yote aliyoyafanya Tanzania na Kenya kumgharibu kiasi kikubwa cha fedha.

"Kutokana na fedha kidogo nilizokuwa nazo wakati nikiwa India, wataalamu walinitengeneza nyonga moja. Nilikaa huko miezi mitatu na kurudi Tanzania kwa sababu fedha ziliniishia," alisema.

Alisema alitakiwa kurudi India mwaka 2016, lakini kutokana na kukosa fedha ameshindwa hivyo amemuomba Rais John Magufuli kumsaidia ili akamalizie matibabu ikiwamo kufanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo, nyonga ya mguu wa kushoto na kuondolewa sumu mwilini.

"Kiasi kinachohitajika kwa matibabu yaliyobakia ni Dola za Marekani 25,000, ninamuomba Rais Magufuli anisaidie niweze kwenda kumalizia matibabu yangu na kurudi kuisadia familia na Tanzania.

"Nina Shahada ya Uzamili katika Sayansi, Uwekezaji na Fedha lakini kutokana na hali niliyonayo taaluma yangu imelala kwa muda wa miaka 20. Ninakuomba Rais Magufuli unisaidie niweze kumaliza matibabu yangu, ninajua unawasaidia wengi naomba nami unisaidie," alisema.

Saunaky alisema yeye ni mtaalam wa mahesabu na hutoa mafunzo kwa wajasiriamali wakubwa na wadogo lakini ugonjwa umefanya taaluma ilale.

Alisema anaamini baada ya matibabu yake atakuja kuitumikia nchi kusaidia azma ya Rais Magufuli kuipeleka nchi kwenye uchumi wa kati wa viwanda kwa kutoa elimu kwa wajasiriamali hao.

Kuhusu familia, alisema ana mke na watoto wawili na mtoto wa kwanza anafanya shughuli ndogo ndogo na wa mwisho yupo shule ya kutwa akiendelea na masomo.

Aliomba kwa yeyote atakayeguswa kumsaidia atume mchango wake kwenye namba ya simu 0755 48 58 30, 0787 48 58 30, 0653 58 48 30 au atume kwenye akaunti ya Benki ya Standard Chartered 0150514480900 tawi la Arusha kwa jina Baltazar Medadi Saunaky.




# Utapiamlo watesa watoto 782 Kigoma

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

WATOTO 782 wenye umri wa miezi 7 mpaka miaka 2 wanakabiliwa na utapiamlo katika halmashauri nne za Mkoa wa Kigoma.

Akizungumza kwenye kikao cha wajumbe wa Kamati ya Lishe Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kaimu Ofisa Lishe Mkoa wa Kigoma, Naomi Rumenyela, alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa ambayo ina chakula cha kutosha, lakini tatizo la utapiamlo bado lipo na sababu ni wazazi kutowapa matunzo watoto hususan kutokuwapa chakula.

Rumenyela alisema utapiamlo sugu unasababisha udumavu, na kwa Kigoma kiwango cha udumavu ni asilimia 37.9.

Alizitaja halmashauri hizo kuwa ni Buhigwe, Kibondo, Kasulu Vijijini na Kigoma Vjijini, na kwamba kuna kazi moja ambayo wanaifanya ya kuhamasisha mabadiliko ya tabia kwa njia ya ushuhuda, ambapo watoto wenye umri wa miezi saba mpaka miaka miwili wanapimwa na kutathminiwa hali yao ya lishe.

Alisema mpaka sasa jumla ya watoto 2,782 kutoka halmashauri hizo wamepimwa.

Rumenyela alisema Halmashauri ya Kibondo ni watoto 752, Kasulu Vijijini 830, Kigoma Vijijini 595 na Buhigwe 555. Kati ya hao watoto ambao walipatikana na utapiamlo ni 782.

Aidha, alisema kazi ambayo wanaifanya kwa sasa ili kuhakikisha tatizo la utapiamlo linapungua ni kuendelea kuhamasisha wananchi umuhimu wa kuwapa chakula watoto ambacho kina makundi yote matano kinachoweza kutia nguvu mwili ambayo ni jamii ya mizizi kama mihogo na viazi na jamii ya nafaka mahindi na mchele.

Pia chakula cha kujenga mwili ambacho ni cha protini jamii ya kunde pamoja na samaki na mazao yake pamoja na nyama.

Aidha, Rumenyela aliwataka kinamama wa mkoa wa Kigoma kuhakikisha kwamba utunzaji wa watoto ni muhimu sana kuliko kuangalia mambo ya kilimo, kwa sababu mtoto akiugua utapiamlo kumtibia inachukuwa muda na shughuli zake zinakwama.

# Tanzania kuwa kitovu biashara ya chai Afrika

**Na Mwandishi Wetu,** NAIROBI

TANZANIA ina sifa duniani ya kuzalisha chai bora kutoka Nyanda za Juu Kusini, lakini kwa muda mrefu uzalishaji na uchakataji wa chai nchini imegubikwa na matatizo.

Kutokana na hali hiyo, mwekezaji wa kampuni ya DL Group amejitosa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na ulimaji wa chai

Afrika. Chai ni kati ya mazao mkakati saba ya Tanzania.

Mwenyekiti Mtendaji wa DL Group, Dk. David Langat, amesema jambo hili linawezekana kwa sababu wakulima wa Tanzania wana uzoefu wa kulima chai na serikali inathamini sekta binafsi na mapendekezo yake.

"Naelewa utekelezaji wa dhamira hii si nyepesi, lakini jambo hili linawezekana na tumechukua hatua zinazoonyesha hivyo na kutupa matumaini makubwa. Isitoshe serikali inatoa ushirikiano wa kutosha kwa sekta binafsi na mapendekezo yenye ubunifu," alieleza mwenyekiti huyo mtendaji.

Kampuni ya DL Group katika miaka mitatu ya nyuma imewekeza katika zao la chai nchini na kupambana na matatizo ambayo yamekuwa yakiwakatisha tamaa wakulima.

Langat alieleza kuwa kampuni yao imenunua mashamba na viwanda vilivyotelekezwa na wawekezaji na kulipa madeni ambayo wakulima wadogo walikuwa wakiwadai wawekezaji waliotoweka.

DL Group imefufua mashamba na kupanda chai upya katika mikoa ya Njombe na Arusha. "Huko Arusha tumenunua shamba na mali za Chai Tausi ili kuinua na kuboresha uzalishaji wa zao la chai," alifafanua na kuongeza kuwa kwa mara ya kwanza mwaka huu Tanzania imeipiku Kenya katika bei ya zao la chai.

"Haya ninayoeleza ni ushahidi kwamba lengo letu la kuifanya Tanzania kuwa "tea hub" (kiini cha kilimo na biashara ya chai) hapa Afrika linawezekana na liko jirani kama kila mdau atatimiza wajibu wake maana uzalishaji unaongezeka," alifafanua na kuongeza kwamba kampuni yake hivi karibuni imewakutanisha wanachama wa chama cha wafanyabiashara ya chai Afrika Mashariki na wamejadili kwa upana vikwazo vya usafirishaji wa zao la chai na vikwazo wanavyokutana navyo wakulima wa chai wa Tanzania.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wawakilishi wa Wizara ya Kilimo.

Katika kuchangia juhudi ya kuinua uzalishaji na ubora wa chai, ameeleza Langat, kampuni yao imetoa mchango katika kufufua kituo cha utafiti wa chai.

Katika hotuba ya bajeti ya mwaka huu wa fedha, Wizara ya Kilimo iliyataja mazao ya asili ya biashara nchini kuwa ni pamba, chai, pareto, korosho, mkonge, sukari, kahawa na tumbaku. Wizara imesema kwamba Tanzania inatarajia kuzalisha tani 35,000 za chai katika mwaka wa fedha wa 2018/19.

Langat alisema kampuni yake inafanya kazi kwa karibu na serikali ya Tanzania kuhakikisha wakulima wadogo wa chai wananufaika na kilimo kwa kuondoa vikwazo visivyo vya lazima.

"Tunaunga mkono juhudi na hatua anazozichukua Mheshimiwa Rais John Magufuli katika kuwekeza mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji na hasa kujenga uchumi wa viwanda ambao msingi wake mkubwa ni kilimo," alisema.



Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya DL, Dk. David Langat (kushoto), akisalimiana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, walipokutana jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 1.3/- kuvipatia maji vijiji kumi

**Na Salome Kitomari**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, imesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji 10, yenye thamani ya Sh. bilioni 1.3.

Mikataba hiyo imesainiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi, na makandarasi watano watakaotekeleza miradi hiyo kwa mwaka huu.

Taarifa ya mkurugenzi huyo ilieleza kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 41.25 hadi 57.1.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/19 halmashauri hiyo itakamilisha usambazaji wa miundombinu ya maji katika vijiji nane na kwamba upatikanaji wa maji utafikia asilimia 71.

Alisema baada ya kukamilika kazi ya uchimbaji wa visima kutakuwa na kazi ya kutandaza mtandao wa mabomba ili kufikisha huduma ya maji karibu na wananchi. "Serikali imetoa fedha hizi ili kufikisha huduma ya maji kwa wananchi kwa urahisi, haitarajiwi kabisa mkandarasi kwenda kinyume cha mkataba, ni lazima tuone thamani ya fedha kupitia miradi hii, tutafuatili kwa karibu ili kodi za wananchi zitumike vizuri," alisema Kijazi.

Akizungumza baada ya kusainiwa kwa mikataba hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Miraji Mtaturu, alisema kukamilika kwa miradi hiyo ni neema kwa wananchi hao kwa kuwa kutapunguza umbali wa upatikanaji wa maji, muda wa kufuata maji na sasa wanakwenda kumtua mama ndoo.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ally Mwanga, alisema Ikungi ahitaji kuona majina mazuri ya kampuni bali utekelezaji wa ufanisi wa miradi ya maji utakaokuwa na tija kwa mwananchi wa kawaida.

# Mamalishe wasusia jengo la mil. 173/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JENGO la mamalishe lililojengwa na Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga kwa shilingi milioni 173, limesusiwa na wajasiriamali hao kutokana na kukosa wateja.

Hali hiyo imetokana na halmashauri kuhamisha kituo cha mabasi kilichokuwa karibu na jengo hilo.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, mamalishe walioandamana hadi Ofisi ya Mkuu wa wilaya kutafuta suluhu juu ya kuhamishwa kwa kituo hicho na kusababisha kushuka kwa biashara, walisema wateja wao walikuwa wakitegemea abiria ambao walikuwa wakisubiri usafiri wa kuelekea vijijini.

Rehema John, mwenyekiti wao, alisema awali jengo hilo lilikuwa na wajasiriamali 24 waliokuwa wakifanyabiashara zao na biashara ilikuwapo kabla ya kuhamishwa kwa kituo cha mabasi, lakini sasa wamebaki 14 kutokana na biashara kudorora.

Alisema wameshindwa kumudu gharama za kulipa bili za maji, umeme, ushuru, mlinzi na mikopo ambayo walikuwa wamekopa katika taasisi za kifedha.

Katibu wa mamalishe hao, Victoria Mwita, alisema kabla halmashauri kuwamishia katika jengo hilo walikuwa wakifanya biashara vizuri katika sehemu mbalimbali, na kuongeza ili kuendelea kufanya biashara katika jengo hilo, ni bora halmashauri ikirejesha kituo hicho.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema malalamiko hayo ameyapokea, na kuwa atakaa na uongozi wa halmashauri kuona jinsi ya kutatua changamoto hiyo.



Kaimu Ofisa Lishe Mkoa wa Kigoma, Naomi Rumenyela (kulia), akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Lishe ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji jana eneo la Mnarani mkoani Kigoma. Habari Uk. 9. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Maelfu wajiunga CHF iliyoboreshwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Manispaa ya Shinyanga wamehamasishwa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF iliyoboreshwa), ili kuwaokoa wanapokuwa hawana pesa ya matibabu.

Kwa Manispaa ya Shinyanga waliojiunga na bima hiyo ni kaya 7,871 kati ya 33,623, waliotarajiwa kuungwa kuanzia mwaka 2016 hadi mwishoni mwa mwaka huu (2019) sawa na asilimia 23.4.

Rai hiyo ilitolewa na Mratibu wa CHF Manispaa ya Shinyanga, Octavian Kiwone, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema wananchi wanapaswa kutambua umuhimu wa kujiunga na CHF ili iwasaidie kuokoa maisha yao hasa pale wanapougua na kukutwa hawana pesa ya matibabu.

Alisema jamii bado haina uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kuwa na kadi CHF iliyoboreshwa, ambayo inakatwa kwa Sh. 30,000 na kutibiwa watu sita katika familia moja ndani ya mwaka mmoja badala ya kutoa pesa mfukoni ambayo itamgharimu fedha nyingi za matibabu.

"Mikakati iliyopo kwa sasa ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kujiunga na bima ya CHF iliyoboreshwa kwa kutembelea kwenye masoko, stendi za mabasi, minadani, viwandani, vyumba za ibada, ili kuwahamasisha wajiunge na kutokuwa na wasiwasi wa matibabu hasa pale watakapo ugua," Kiwaone alisema.

"Licha ya kuendelea kutoa hamasa ya wananchi kujiunga na bima ya afya CHF, tunaboresha na utoaji wa huduma kwa wananchi ambao wanakadi hizi, ili waweze kupatiwa matibabu ya haraka pamoja na upatikanaji wa dawa na manispaa huwa tunatoa pesa mapema kwenye vituo vyetu vya afya," aliongeza.

Mmoja wa wanufaika wa bima hiyo, Venant Lyamukama, mkazi wa Kambarage Manispaa ya Shinyanga, alisema bima hiyo imemsaidia kipindi alipokuwa hana hela, licha ya yeye kupatiwa matibabu, mkewe alilazwa hadi chumba mahututi (ICU) na hawakutoa pesa yoyote. Kwa upande wake ofisa mradi wa HPSS mkoani Shinyanga, John Richard, alizitaka halmashauri mkoani humo kuandikisha idadi kubwa ya wananchi ili wapate matibabu licha ya kuwa na ukosefu wa fedha.

# Joyce Shebe Mwenyekiti mpya Tamwa

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), kimemchagua Joyce Shebe, kuwa mwenyekiti mpya wa chama hicho kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Uchaguzi huo ulifanyika juzi baada ya kumalizika kwa mkutano mkuu wa mwaka huu wa chama hicho, uliowaleta pamoja wanachama kutoka Tanzania Bara na Visiwani.

Aidha, wanachama hapo pia wamechagua wajumbe wa bodi ambao ni Leah Mushi, Raziah Mwawanga kwa upande wa Bara na Halima Mselem anayewakilisha Zanzibar.

Akizungumza na wanachama baada ya ushindi huo, Joyce aliwataka wanachama kuwa mstari wa mbele kuijenga Tamwa kwa manufaa endelevu ya chama hicho na taifa kwa ujumla.

Alisema Tamwa inategemewa na Watanzania kutokana na majukumu yake ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Aidha, alisema Tamwa ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kidemokrasia na haki za binadamu na kwamba yote yatawezekana iwapo wanachama watatumia vyema kalamu zao kuibua habari mbalimbali za kuleta mabadiliko katika jamii.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu yake, wataendeleza maono na mipango ya Tamwa kwa kuzingatia malengo endelevu ya millennia ambayo Tanzania imeyaridhia.

Awali, Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Alakok Mayombo, alisema Tamwa itajengwa na wana Tamwa na daima waandishi wa habari wanatakiwa kuzitumia kalamu zao kuelimisha, kuburudisha na kukosoa ili kuwa na maendeleo.


Baadhi ya wanachama walisema mchango wa Tamwa kwa kutumia kalamu umeleta mabadiliko chanya katika mapambano dhidi ya mila kandamizi za wanawake na watoto wa kike.

Walisema Tamwa imekuwa mstari wa mbele kupiga vita ukeketaji, ndoa za utotoni, mila potofu za ngoma za unyago ambazo humwandaa mtoto wa kike wa kuanzia umri mdogo wa miaka mitatu.

Kadhalika, unyanyasanyi wa wanawake kama vipigo, kukeketwa na kutokuwa na nguvu ya kiuchumi kumeumiza fikra za wanawake wengi na kuishi maisha tegemezi ambayo huwa ni mateso kwao na watoto wao.

Naye Mkurugenzi wa Tamwa, Rose Ruben, alisema moja ya mradi unaofanywa na Tamwa ni kuibua matukio ya ukatili wa kijinsia katika wilaya 10 nchini na kuandika habari kwenye vyombo vya habari.

Aidha, aliwaomba wadau mbalimbali kushirikiana na Tamwa ikiwamo kutoa taarifa za matukio yao na kutumia vyema dawati la msaada wa kisheria pamoja na kusukuma mabadiliko ya sheria mbalimbali ambazo zinaonekana kuwa kikwazo cha maendeleo ya mwanamke na mtoto wa kike.



## HABARI ARUSHA

# Shirika laipongeza serikali huduma watoto wenye usonji

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

SHIRIKA la Connects Autism Tanzania (CAT), limeipongeza serikali kwa kutoa huduma ya walimu wataalamu, chakula, vifaa na afya kwenye vitengo vinavyohudumia watoto wenye ulemavu ikiwa pamoja na usonji.

Aidha, limekipongeza Chuo cha Ufundi Stadi (Veta), Oljoro kwa kukubali kuwapokea wanafunzi 10 wenye ulemavu wa akili na usonji kupata mafunzo ya ufundi stadi na kuweza kujiajiri au kuajiriwa na kupata kipato kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

Mkurugenzi na mwasisi wa CAT, Graceanna Lyimo, alisema hayo wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya usonji yaliyofanyika jijini hapa mwishoni mwa wiki.

"Huduma hizo zimewezesha kuwapo na ongezeko kubwa la watoto wanaoandikishwa kwenye vitengo...tunaomba serikali iendelee kutoa huduma hizo na ikiwezekana kuziboresha zaidi," alisema.

Alisema kutokana na ongezeko la watoto wanaoandikishwa shuleni, kumekuwa na upungufu wa walimu wataalamu, vifaa vya kutolea huduma pamoja na vyumba vya madarasa.

Aliishauri serikali na wadau ikiwezekana kujenga bweni au kuwapatia watoto hao usafiri wa uhakika wa kutoka nyumbani na kuja shuleni kwa kuwa baadhi yao wanaishi mbali na vituo hivyo.

Alisema lengo la maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya 'Tuwalinde Tuwapende' ni kuelimisha jamii kuhusu watoto wenye usonji na kuondoa dhana ya kuwaona watoto hao kama hawawezi, hivyo, jamii inatakiwa kuwapa nafasi ya kufanya mambo mbalimbali.

Alisema usonji ni hali inayomwathiri mtoto katika mishipa ya fahamu na hali hii huleta changamoto kubwa katika maeneo makuu matatu ambayo ni mawasiliano, mahusiano na kijamii na utambuzi na hujidhihirisha zaidi mtoto anapofikia umri wa miaka mitatu.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Omary Kwesiga, alisema serikali ilifanya utambuzi wa watoto wote wenye ulemavu/ mahitaji maalum na kupewa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na huduma za kiafya na kuandikishwa kwenye shule zenye vitengo vya kuwahudumia kulingana na mahitaji yao.

Alisema serikali inatambua hatua hiyo imesababisha kuwapo kwa ongezeko kubwa la wanafunzi kwenye vitengo na kusababisha uhitaji wa walimu wataalamu.

Alisema Chuo cha Ualimu Patandi kimepewa jukumu la kuandaa walimu wataalamu hivyo changamoto hiyo itaendelea kupungua.

"Natoa wito kwa wazazi, wadau na jamii kuendelea kuwabaini na kuwaelekeza wazazi kuwapeleka watoto wenye ulemavu kwenye vitengo vinavyowahudumia ili nao wapate fursa za elimu...watoto wenye ulemavu wanapopata fursa za elimu inawasaidia sana kuondoa au kupunguza hali yao ya ulemavu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi, Emmanuel Munisi, aliipongeza serikali kwa kuendeleza huduma kwa watoto wenye mahitaji maalumu.

Aliwaomba wazazi wenye watoto wa aina hiyo wasiwafiche ndani bali wawaonyeshe upendo wa hali ya juu na wasiwanyime haki zao kama elimu, michezo ili kukuza ufahamu wao.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiongea kwenye uzinduzi rasmi wa Siku ya Nyumba ya NMB iliyofanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Siku ya Nyumba ya NMB ni maonyesho yenye lengo la kuwaleta pamoja wateja na kampuni za kuuza nyumba ili kuona miradi waliyonayo na gharama kabla ya kununua kupitia benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lukuvi ataka NMB kushirikiana na NHC

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametoa wito kwa Benki ya NMB kuungana na Shirika la Nyumba la Taifa, (NHC), ili kusaidia utatuzi wa changamoto ya umiliki wa nyumba bora na za kisasa miongoni mwa Watanzania.

Lukuvi alitoa wito huo wakati wa uzinduzi wa NMB Nyumba Day Expo 2019, maonyesho yanayolenga kuwakutanisha wadau wa sekta ya ujenzi na kutoa elimu na uelewa kwa wananchi juu ya mikopo ya nyumba na namna sahihi ya kumiliki nyumba bora.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, kumekuwa na changamoto kubwa kwa Watanzania wa kada mbalimbali katika kumiliki viwanja, kupata hati za viwanja hivyo pamoja na vibali vya ujenzi na kwamba ushirikiano wa kikazi baina ya NMB na NHC, utasaidia kumaliza changamoto hiyo.

Kupitia maonyesho hayo yanayofanyika jijini Arusha, Waziri Lukuvi alibainisha kuwa serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 421 kwa taasisi za fedha nchini kupitia Sheria ya Fedha za Mikopo ya Makazi ya Mwaka 2008, kwa lengo la kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuwezesha upatikanaji wa makazi ya kutosha.

Mapema, akizindua maonyesho hayo, Mkuu wa Wateja Wadogo na wa Kati wa NMB, Salie Mlay, aliahidi kuufanyia kazi wito wa Waziri Lukuvi, huku akibainisha kuwa katika kipindi cha miaka miwili, wametoa mikobo ya zaidi ya Sh. bilioni 17.

Mlay alibainisha kuwa mikopo hiyo imetolewa kwa zaidi ya wateja 139 kote nchini, huku akiahidi kuwa benki yake kwa kushirikiana na NHC watajikita katika kuwawezesha wananchi wa Arusha kumiliki viwanja na nyumba kwa gharama.

Aliongeza kwa kuanzia watahakikisha wakazi wa Arusha wanamiliki viwanja na kupata makazi kwa gharama nafuu katika mradi wa ujenzi wa makazi wa Safari City, unaofanyika huko Mateves, nje kidogo ya jiji la Arusha.

kwa lengo la kuwezesha wateja kumiliki makazi bora na nafuu, kulingana na kasi ya ongezeko la watu mijini na vijijini.

# Watahadharisha mwendo kasi mbuga za wanyama

**Na Novatus Makunga,** SERENGETI

WATAALAMU wa mradi wa utafiti wa duma nchini wametaka mwendokasi wa magari yanayobeba watalii udhibitiwe ndani ya hifadhi za taifa kwa madai ya kusababisha kugongwa mara kwa mara kwa wanyamapori hasa adimu waliopo hatarini kutoweka.

Ushauri huo ulitolewa na timu ya wanasayansi waliopo katika mradi unaoratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, (Tawiri), ambao kwa sasa wanaendelea na utafiti wa kupungua kwa duma katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mratibu wa mradi huo, Denis Minja, alisema kati ya mwaka 2016 na 2018 duma wapatao nane walikufa kutokana na kugongwa na magari ya watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Minja alieleza pamoja na adhabu ya faini ya dola za Marekani 5000 (zaidi ya Sh. milioni 11) na kuzuiwa kuingia katika hifadhi ya taifa kwa miezi mitatu kwa dereva wa gari, lakini alisisitiza bado ajali hizi ni janga kubwa kwa utalii.

"Jaribu kupiga hesabu nyepesi tu, kasi ya duma ni kilometa 105 kwa saa na ana uwezo wa kuchanganya kasi hiyo kwa muda mfupi tu, hivyo kugongwa kwao mara kwa mara kunaashiria kuna tatizo," alisema Minja.

Alishauri ni vyema sasa ukawapo mfumo ama vifaa vya kudhibiti mwendo kasi wa magari hususani katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Minja alisema duma ni kati ya wanyama 10 adimu aina za paka mwenye kasi duniani na pia ni hatari, asilimia tisa pekee ya aina hiyo ya mnyama ndiyo wamebakia katika historia ya wanyama hao duniani.

Aidha, wataalamu hao wa watafiti walitaja sababu nyingine za kupungua kwa duma ni kwa watoto wake kuliwa na wanyama wakali ambao wamewataja kuwa ni pamoja na fisi, simba na chui.

"Kimsingi kati ya watoto 100 wa duma wanaozaliwa ni asilimia tatu tu ndiyo wanaoweza kuendelea kuishi," Minja alifafanua.

Watafiti wanasayansi hao wanataja sababu nyingine ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, ujangili, ongezeko la shughuli za kibinadamu na kasi ya ujenzi wa hoteli ndani ya hifadhi za taifa.

"Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba kuna hatari kwa duma kutoweka duniani iwapo hatua za kumlinda hazitachukuliwa na katika nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania," Minja aliongeza.

Allibainisha katika mfumo wa Ikolojia ya Selous-Mikumi, duma wametoweka tangu miaka ya 1980.

Minja alisema kuwa Tawiri inatarajia kuanza utafiti mwingine wa duma katika mfumo wa Ikolojia ya Ruaha-Rungwa pamoja na ikolojia ya Tarangire-Manyara.

Katika nchi za Afrika ya Mashariki takwimu zinaonyesha kuwapo kwa duma 2,572 wanapatikana katika hifadhi za Serengeti na Ngorongoro pamoja na mbuga ya Maasai Mara na Tsavo nchini Kenya.





## KESI MAUAJI YA MWANAFUNZI:

# Jamhuri yaombwa kuongeza mashahidi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UPANDE wa mashtaka katika kesi ya mauaji ya mwanafunzi wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari ya Scholastica inayowakabili watu watatu akiwamo mfanyabiashara maarufu wa Moshi, Edward Shayo 'king size' na wenzake wawili umeongeza idadi ya mashahidi kutoka 34 hadi kufikia 39.

Hoja ya kutaka kuongezwa kwa idadi ya mashahidi hao ilitolewa mwishoni mwa wiki na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, mbele ya Jaji Firmin Matogolo anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi.

Kesi hiyo namba 48 ya mwaka 2018, inamkabili mmiliki wa shule hiyo Edward Shayo, mwalimu wa nidhamu wa shule hiyo Labani Nabiswa na mlinzi wa shule hiyo Hamisi Chacha.

Akitoa hoja hiyo, Wakili Chavula aliieleza: "Mheshimiwa Jaji, naomba kuitaarifu mahakama yako kwamba siye wa upande wa mashtaka tuna nia ya kuongeza idadi ya mashahidi kutokana na baadhi ya mashahidi tuliowaandaa kushindwa kufika kutoa ushahidi kutokana na sababu mbalimbali."

Wakili Chavula alitoa hoja hiyo wakati alipokuwa anaiomba mahakama hiyo iahirishe shauri hilo hadi leo, mahakama itakapoendelea kusikiliza mashahidi wa upande wa mashtaka.

Kabla ya kuwasilisha ombi hilo, wakili huyo alimweleza Jaji Matogolo kwamba wakati wanaendelea na usikilizwaji wa mashahidi hao, kulikuwa mashahidi ambao hawajafika na wako njiani.

Alidai mashahidi hao ni askari polisi ambao waliwasiliana nao na wakatoa taarifa kwamba wanajiandaa kuja leo.

"Mheshimiwa Jaji tunaiomba samahani mahakama hii kwa kuwa tulishawaandaa mashahidi wetu lakini hawajafika, tunaiomba radhi tukija Jumatatu hali hii haitajirudia tena kwa kukwamisha kesi isiendelee," alidai.

Katika kesi hiyo, Chavula amedai wamejiandaa vyema, hivyo wanaiomba mahakama hiyo kuongeza idadi ya mashahidi watano ambao ni askari polisi H.1469 DC John, F 3988 PCP Kibwana Luis,G 5865 DC Abdul, Insekta Leonce Mwamunyi na E 9022 Enock.

Baada ya kuwasilishwa ombi hilo, jopo la mawakili wa utetezi likiongozwa na Wakili Elikunda Kipoko, lilipinga ombi hilo likiiomba mahakama isikubaliane na hoja ya upande wa mashtaka.

Hata hivyo, Jaji Matogolo alihoji iwapo upande wa mashtaka kama mashahidi hao walipata wito wa mahakama na kuagiza upande wa mashtaka kuhakikisha mashahidi na vielelezo katika kesi hiyo havikwamishi usikilizaji wa kesi hiyo.

Awali, wakati mahakama hiyo ikiendelea na usikilizwaji wa shauri hilo la mauaji ya kukusudia, shahidi wa sita wa upande wa mashtaka, PC Shabani (askari polisi) ambaye anatoka katika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kilimanjaro (RCO), aliieleza yeye ndiye aliyehusika kusafirisha sampuli mbali mbali za vipimo vya DNA (sampuli za vinasaba) hadi Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dar es Salaam Oktoba 20, 2017.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Joseph Pande, shahidi huyo alidai alipeleka kwa Mkemia Mkuu wa serikali, vipimo vya Joyce Makundi, Jackson Makundi ikiwamo damu na jino la mwili wa marehemu, Humphrey Makundi (16).

Alidai alipitia na sampuli hizo katika ofisi ya DCI (Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai) na kuomba kibali cha kupeleka vipimo hivyo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, baada ya kupata barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kilimanjaro.

Alidai aliondoka Novemba 19, 2017 akitokea katika mjini wa Moshi na kwenda hadi Uwanja wa Ndege Kisongo, Arusha na kuondoka na ndege ndogo ya Coast Line kupitia Zanzibar na saa 8:00 mchana ikatuwa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere (JNA).

Zaidi aliieleza mahakama sampuli hizo zilikuwa zimehifadhiwa na kufungwa kwa kutumia 'lakiri' na kuhifadhiwa katika kisanduku ndani ya jokofu katika Ofisi ya DCI na kukabidhiwa funguo na kwenda zake kupumzika na ilipofika Oktoba 21, 2017 alielekea Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na kukabidhi sampuli hizo.

Aliendelea kudai alipofika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali alikabidhi sampuli hizo na nyaraka kutoka Ofisi ya RCO Kilimanjaro na Ofisi ya DCI. Shahidi huyo (PC Shaban) alidai Mkemia Mkuu wa Serikali, kabla ya yeye kuondoka alizikagua nyaraka na sampuli hizo kisha kuchukua namba zake za simu kwa mawasiliano na ilipofika Oktoba 29, 2017 alipokea simu kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu ikimtaka afike katika ofisi hizo kuchukua majibu.

Alisema alitoa taarifa ofisini kwake juu ya wito huo na kujiandaa na safari, ambapo alifika Dar es Salaam na kukabidhiwa vipimo hivyo Oktoba 30, 2017 alirudi Kilimanjaro na kuzikabidhi kwa RCO na Januari 30,2018 alikabidhiwa tena simu saba na kuzipeleka Ofisi za Cyber Crime (kitengo cha uchunguzi wa makosa ya kimtandao) Dar es Salaam kufanyiwa uchunguzi.



Baada ya maelezo hayo, wakili wa utetezi, David Shilatu, wakati anamhoji shahidi huyo mambo yalikuwa hivi:

Wakili Shilatu: Ili Sampuli zitoke kwa mtunza vielelezo ni lazima ujaze fomu namba 16?

**Shahidi:** Hapana, nilijaza kwenye clearance book.

**Wakili:** Umeileta hapa mahakamani kama ushahidi?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Ni kweli ulipewa barua na RCO Kilimanjaro?

**Shahidi:** Ni kweli nilipewa

**Wakili:** Umeileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Ulipewa fomu namba 180?

**Shahidi:** Ndiyo

**Wakili:** Umeileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili :**Ulipewa barua na DCI?

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:**Umeileta mahakamani?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Barua ya RCO umeileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:**Umeleta mahakamani ripoti toka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ama barua?

**Shahidi:** Hapana sijaleta

**Wakili:** Ulipewa simu 7 na Hashimu?

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Umeleta hapa mahakamani vielelezo vya makabidhiano ya simu hizo?

**Shahidi:** Hapana sijaleta mahakamani hapa

**Wakili Sambo:** Ni document zipi umesainishwa wakati wa makabidhiano na Mkemia Mkuu?

**Shahidi:** Nilisaini dispatch book na sio fomu ya polisi

**Wakili:** Haukusafiri siku ya tarehe 29/11/2017 na sampuli hizo ulizitoa wapi?

**Shahidi:** KCMC

**Wakili:** Simu 7 alizokukabidhi ulisaini?

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:**Zilirudi kwa Hashimu?

**Shahidi:** Mimi nilikabidhi Ofisi za DCI, Kitengo cha Cyber Crime

**Wakili:** Ulisaini chochote?

**Shahidi:** Sikusaini

**Wakili Eliakunda Kipoko:** Hapa mahakamani umeonyesha ushahidi wowote ulisafiri kwenda Dar es Salaam?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Hapa mahakamani umeleta ushahidi wowote kuna kitu ulipokea Dar es Salaam kwa Mkemia Mkuu?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili Paul:** Wewe ulisafiri bila kupewa bording pass ya kusafiria?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Umeileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Hapana

Wakili wa serikali: Hapa mahakamani umeulizwa maswali mengi kwamba hujaleta ushahidi hapa mahakamani ni kweli?

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Ushahidi wako ni nini?

**Shahidi:** Haya niliyokueleza.

**Shahidi** wa tano wa kesi ya mauaji ya kukusudia, Anastazia Lutumula, aliieleza mahakama alipokea maiti isiyojulikana akiwa kazini, lakini hakuiangalia.

Anastazia Lutumula alikuwa muuguzi wa zamu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), wakati mwili wa mwanafunzi huyo Humphrey Makundi unaingizwa chumba cha kuhifadhia maiti, Novemba 10, 2017.

Akitoa ushahidi wake kwa kuongozwa na wakili wa upande wa mashtaka, Lucy Kyusa, shahidi huyo alidai siku hiyo akiwa kazini, Inspekta wa Polisi (Mkaguzi Msaidizi), aliyemfahamu kwa jina moja la Juma alifika hospitali hapo akiwa na gari la polisi na kumwambia ameleta maiti isiyojulikana kwa ajili ya kuhifadhi mochwari lakini ni ya jinsia ya kiume ambayo imeokotwa eneo la Himo.

Aliendelea kudai baada ya kuelezwa ni mwili usiotambulika umeokotwa Himo na kuuandikia taarifa yake, alimwita mlinzi wa zamu katika Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi kwa ajili ya kuihifadhi.

Shahidi huyo aliieleza alilazimika kumwita mlinzi huyo kwa sababu wakati huo mhudumu wa chumba cha kuhifadhia maiti alikuwa ameshatoka hospitali na kwenda kupumzika nyumbani.

Alidai alimkabidhi mlinzi funguo za chumba hicho cha kuhifadhia maiti na yeye kuendelea na majukumu yake, lakini alishuhudia kwa mbali wakishusha na kuingiza mwili huo mwochwari na yeye aliondoka kazini Novemba 11, 2017.

Baada ya kumaliza kutoa ushahidi wake na kuanza kuhojiwa na jopo la mawakili wa upande wa utetezi, Wakili Elikunda Kipoko, David Shilatu, Gwakisa Sambo na Patrick Paul, shahidi huyo alidai sio wajibu wake kuona mwili wa marehemu na kwamba Novemba 10, 2017 hakuona maiti, bali aliandikisha taarifa za kupokelewa maiti hiyo.

Alidai baada ya siku kadhaa aliitwa polisi na kuandika maelezo yake ambayo yamepokelewa na mahakama hiyo kama ushahidi wa upande wa utetezi, huku upande huo ukidai shahidi huyo ameshindwa kuwasilisha rejesta ya majina ya watu walioingiza maiti hiyo mwochwari wala gari lililobeba maiti.

Shahidi wa tano wa upande wa mashtaka ambaye ni Daktari wa Meno kutoka Hospitali ya Rufani ya KCMC, Dk. Samweli Mwita, alidai Novemba 19, 2017 akiwa kazini alikuta mwili wa mtu asiyejulikana ukiwa kwenye mfuko wa plastiki umeharibika na unahitaji kufanyiwa uchunguzi ili kukisia umri wake.

Alidai mwili huo ulianza kuharibika na ni vigumu kutambulika kwa wepesi mwili ulioharibika na nyama huwa zinatangulia kuanza kuoza na katika kumbukumbu zake siku hiyo waliufanyia uchunguzi mwili huo akiwa na madaktari wenzake wane.

Alidai kabla ya kufanya uchunguzi hakuna mtu aliyeweza kutambua mwili bila kufanya vipimo vya DNA na kwamba baada ya uchunguzi wake alitambua mwili huo unaweza kuwa na umri wa kati ya 14 na 17 kutokana mfumo wa meno yake ulivyokuwa.

Alisema baadhi ya meno ya marehemu hajui yalipotelea wapi na kwamba baada ya uchunguzi wake pia alitoa maelezo yake polisi, ambapo nayo yalipokelewa na mahakama hiyo kama kielelezo cha ushahidi upande wa mashtaka.

Mshtakiwa wa kwanza ni mlinzi wa shule hiyo Hamisi Chacha. Upande wa mashtaka unaongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, John Pande, Wakili Mwandamizi wa Serikali Abdalah Chavula, Wakili wa Serikali, Omary Kibwana na Wakili wa Serikali Lucy Kyusa.

Jopo la mawakili wa utetezi linaongozwa na mawakili Elikunda Kipoko, David Shilatu, Gwakisa Sambo na Patrick Paul.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU APRILI 8, 2019



**SABABU SIMBA KUTOKA SARE NA TP MAZEMBE** **UK.18**

## KIMGONGOMGONGO...




### ISIKUPITE

Lionel Messi ameipiku rekodi ya Iker Casillas kwenye La Liga wakati akiisaidia Barcelona kuichapa Atletico Madrid mabao 2-0 Jumamosi. Kwa kipindi kirefu kipa huyo wa zamani wa Real Madrid, Casillas aliyeichezea kwa miaka 16, alikuwa akishikilia rekodi ya kushinda mechi 334 kwenye La Liga tangu alipotimkia Porto mwaka 2015, lakini Messi, sasa amempiku ikiwa ni baada ya kuifikia rekodi hiyo wiki moja iliyopita wakati waliposhinda mechi ya Catalunya 'dabi' dhidi ya Espanyol.

Mshambuliaji wa Real Madrid, Gareth Bale, akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa Eibar, Jose Angel "Cote", wakati akiwania kumiliki mpira wa juu kwenye mechi ya La Liga iliyopigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi na vijana hao wa Zinedine Zidane kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **HABARI UK. 30**

## MICHEZO



# KWA NINI RONALDO NI BORA KULIKO MESSI KIMATAIFA?

**MADRID,** Hispania

WACHEZAJI Cristiano Ronaldo na Lionel Messi wamekuwa na mjadala unaoonekana kutokuwa na mwisho juu ya nani ni mchezaji bora zaidi duniani. Hata hivyo, wote wana ubora wa aina yake.

Messi, kwa mfano, ameshinda mataji mengi zaidi ya Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kuliko Ronaldo na msimu huu, raia huyo wa Argentina amefunga mabao mengi zaidi kuliko mwenzake huyo anayecheza pale Juventus katika ligi ya ndani na ile ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo, kwa upande mwingine, ameonekana kama mmoja wa wachezaji bora zaidi baada ya kushinda mataji katika nchi tofauti, na Messi ametumia muda wake karibia wote kwenye Ligi ya Hispania. Hapa tutaangalia sababu tatu kwa nini Ronaldo ni bora zaidi ya Messi katika Ligi ya Mabingwa na kwa timu ya taifa.

**1. Uzoefu**

Ronaldo bila shaka amepata sifa za kipekee katika ligi tofauti kuliko Messi. Alikuwa na miaka mingi ya kupata uzoefu kwenye ligi ya nchini kwao Ureno kabla ya kujiunga na Manchester United. Alikaa miaka sita katika Ligi Kuu ya England na baadye akajiunga na Real Madrid; ambako alikaa misimu tisa.

Hivi karibuni alifungua sura mpya katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A na vinara wenye kutawala soka la nchini hiyo kwa sasa, Juventus. Ujuzi wake mkubwa wa ligi na wachezaji wengine umemsaidia kuwaelewa wapinzani wake vizuri. Katika mashindano kama vile Ligi ya Mabingwa na mashindano ya kimataifa, mchezaji atakuwa na wachezaji wengi tofauti kutoka kwa ligi kadhaa na timu za taifa.

Wote wana sifa tofauti na kucheza mitindo yao. Hivyo, Ronaldo anaweza kuwa na faida zaidi kuliko Messi hata kabla ya mchezo kuanza.

Nyota wa Barcelona, hata hivyo, ametumia maisha yake yote katika La Liga, ambayo inajumuisha wachezaji wa Hispania. Inaeleweka kwamba Messi pia amezifunga timu nyingi kutoka ligi tofauti.

**2. Mawazo ya kipekee**

Mbali ya uhodari wake, shabiki yeyote wa soka lazima akiri kwamba Ronaldo pia ana mawazo mazuri. Nyimbo za chuki kutoka kwa mashabiki zilikuwa kama kifungua kinywa chake cha kila siku wakati Mreno huyo akicheza Real Madrid.

Sio siri kwamba pale 'Los Blancos' kulikuwa na matukio mengi ambapo wafuasi wao walikuwa wakiwazomea wachezaji wao wenyewe kutokana sababu binafsi. Hali hii mbaya inahamasisha na kufundisha nguvu za akili za Ronaldo kwa kiwango ambacho atakuwa na nguvu wakati wapinzani wake wanapomvuta.

Mtazamo wa nguvu ni moja ya funguo muhimu katika ligi zote na michuano ya Ligi ya Mabingwa na mashindano ya kimataifa kama hatima ya timu imeamua katika mechi moja au mbili.

Uwezo wa Ronaldo wa kutamani kushinda mara zote umemsaidia kuharibu hali ngumu, na hata wakati aliposhambuliwa wakati wakifungwa na Atletico Madrid hakuonyesha kuchukia sana.

Wakati Juventus ilipopoteza kwa mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa hatua ya mtoano wa timu 16, yeye ndiye aliyepindua matokeo kwenye mchezo wa pili.

Messi, kwa upande mwingine, ni mara chache mno amekuwa akizomewa na mashabiki, kwani wale wa Barcelona wanamwamini zaidi.

**3. Uongozi wa ubora**

Mbali na mawazo yake yasiyoweza kuzunguka, Ronaldo anaweza kuhamasisha wachezaji wenzake kuwa na tamaa ya kushinda. Labda wengi wa mashabiki wa mpira wa miguu wanaweza kusema kuwa nyota huyo wa zamani wa Real Madrid ana maneno mazuri zaidi kwa wenzake akiwa chumba cha kubadilishia nguo kuliko Messi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, mara zote huwa hasiti kuwahamasisha wenzake. Lakini kwa upande wa Messi yeye mara zote si mzungumzaji na hivyo sio mtu wa kuhamasisha wenzake.

**JE, WAJUA?**

HII ni mara ya 11 kwa Manchester City kutinga fainali ya Kombe la FA, na ya kwanza tangu mwaka 2013 wakati ilipochezea kichapo dhidi ya Wigan, lakini pia City inakuwa timu ya tisa tofauti kutinga fainali za makombe yote makubwa England kwa msimu mmoja, baada ya Arsenal, Chelsea, Everton, Liverpool, Manchester United, Middlesbrough, Sheffield Wednesday na Tottenham Hotspur.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA




## SALAH AJIVUNIA REKODI LIVER

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amesema anajisikia furaha na fahari kuvunja rekodi Liverpool baada ya kuhitimisha ukame wake wa mabao Ligi Kuu England kwa kutupia bao muhimu dhidi ya Southampton Ijumaa iliyopita.

Salah aliiweka Liverpool mbele ndani ya dakika 10 kwenye mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa St Mary', na Jordan Henderson akaongeza lingine katika dakika za mwisho na kuifanya timu yao kuibuka na ushindi wa mabao 3-1.

Ushindi huo uliirejesha Liverpool kileleni juu ya Manchester City katika mbio za ubingwa, na 'Wekundu' hao wakiwa mbele kwa pointi mbili, lakini wakicheza mechi moja zaidi ya mabingwa hao watetezi.

Na kwa mabao yake tisa katika mashindano yote, Salah anakuwa mchezaji aliyefikisha mapema zaidi mabao 50 kwenye Ligi Kuu England, EPL kwa Liverpool.

Na ahueni hiyo kutoka kwa Salah ilikuwa wazi kufuatia kutania kuhusu kiwango binafsi cha nahodha Henderson kufuatia bao lake.

"Nadhani hilo bao ni namba 50 kwa Liverpool kwenye EPL, hivyo hiyo ni ya kipekee," Salah aliiambia Sky Sports baada ya kutupia bao lake la 18 kwenye ligi msimu huu.

"Baada ya mechi tisa ni mwenye furaha na najisikia fahari, lakini kwa timu na pointi tatu muhimu zaidi. Bao langu la kwanza katika mechi tisa, bao la kwanza la [Henderson] katika mechi 20!"



Wachezaji wa Mbao FC, wakishangilia bao lao kwenye mechi dhidi ya Yanga, wakati ikilala 2-1. Mbao ni moja kati ya timu 17 zilizo kwenye hatari ya kushuka daraja msimu huu.

# HAZIPO SALAMA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni, ukiondoa timu tatu tu, hakuna timu yoyote iliyoonekana kuepuka janga la kushuka daraja.

Katika ya timu 20 zinazoshiriki Ligi Kuu, ni Yanga, Simba na Azam pekee ndizo zinazoonekana hazina tishio la kushuka daraja, lakini 17 zote zilizobaki kama hazikuchanga karata zao vizuri basi zinaweza kujikuta zikikata tiketi ya kucheza Ligi Daraja la Kwanza msimu ujao.

Msimu huu ni timu nne zinazoshuka daraja, na hali imekuwa ngumu kutokana na timu nyingi kulingana pointi na pia hata zilizokuwa juu yao kutokuwa na tofauti kubwa ya pointi.

Hii inaonyesha kuwa msimu huu umekuwa na ligi ngumu iliyokuwa na timu zilizojipanga vema kutoa ushindani mkali, licha ya changamoto mbalimbali ya ukata, ikiwamo kutokuwa na mdhamini.

Tayari kuna timu zimeshabakisha mechi tano kabla ya kumalika kwa msimu huu Ligi Kuu na hazipo kwenye mazingira mazuri. Zifuatazo ni timu zote ambazo inabidi zipambane kwenye mechi zao zilizosalia, la sivyo zinaweza kujikuta shimoni...

**1. Lipuli**
Pamoja na kwamba inakamata nafasi ya nne ikiwa na pointi zake 48, lakini kimahesabu bado inaweza kushuka daraja. Lipuli imebakisha mechi tano tu ili imalize ligi na pointi ilizonazo zinaweza kupitwa na timu zilizo nyuma yake. Kwa maana hiyo inabidi mechi zake zilizobaki zisifanyiwe masihara.

**2. Mtibwa Sugar**
Iko nafasi ya tano ikiwa na pointi 45, ikiwa imecheza mechi 31. Imebakisha mechi saba tu kuweza kuhitisha mechi zake. Nayo inabidi ifanye kazi ya ziada kwani pointi ilizonazo kama haikufanya vizuri zinaweza kupitwa na timu zilizopo chini na kuipa wakati mgumu.

**3. Tanzania Prisons**
Timu hii ya maafande ilianza kinyonge ligi na kuonekana huenda ikashuka daraja mapema. Lakini imejipapatua na kuwa kwenye nafasi ya sita hadi jana. imekusanya pointi 42, ikiwa imebakisha mechi sita tu kumaliza ligi. Hata hivyo, kutokana na pointi ambazo timu za nyuma yake zinazo, bado haiko salama.

**4. KMC Kinondoni**
Timu hii imepanda daraja msimu huu, lakini inashika nafasi ya saba ikiwa na pointi 41. KMC imebakisha mechi nane kumaliza ligi, lakini pia inaweza kushuka kama itapoteza baadhi ya mechi zake na timu zilizo chini yake zikafanya vizuri.

**5. Coastal Union**
Nayo ina pointi 41 kama KMC, pia imebakisha mechi nane. Jana ilitarajia kucheza dhidi ya Ndanda. Mfuatano huu wa pointi unaonyesha kabisa kuwa timu yoyote ile itakayoteleza kwenye Ligi Kuu, basi Ligi Daraja la Kwanza inaihusu.

**6. JKT Tanzania**
Imebakisha mechi saba tu kumaliza Ligi Kuu, imevuna pointi 39, hivyo iko katika hatari ya kushuka daraja kama haitajizatiti kwa mechi zake zilizobaki, lakini kama itachanga karata zake vizuri, basi inaweza kuzipita timu zilizo juu.

**7. Singida United**
Kama ilivyo kwa JKT, imebakisha mechi saba na ina pointi 39, ambazo nazo bado zinatia wasiwasi kama inaweza kubaki endapo haitafanya vema kwenye mechi zake ilizobaki nazo mkononi.

**8. Mbeya City**
Imebakisha mechi nane kabla ya kumaliza mechi zake msimu huu, lakini ina pointi 37. Ni pointi ambazo zinaitaka kufanya kazi ya ziada kwenye mechi zilizobaki kwani inaweza kujikuta ikishuka daraja.

**9. Mwadui FC**
Nayo ina pointi 37, lakini kwa bahati mbaya sana imebakisha mechi tano tu ili kumaliza ligi, hivyo inatakiwa kufanya kila njia kuhakikisha inafanya vema kwenye mechi zake zilizobaki, huku ikiangalia na za wenzake.

**10. Alliance FC**
Pia ina pointi 37. Imebakisha mechi sita kumaliza ligi. Inabidi icheze kufa au kupona kama inataka kubaki Ligi Kuu, la sivyo itakwenda na maji.

**11. Kagera Sugar**
Imecheza mechi 30, hivyo imebakiza mechi nane ili kumaliza mechi zake za ligi na imevuna pointi 36 mpaka sasa. Haiko sehemu nzuri kwa hiyo juhudi zinahitajika kufanyika ili kunusurika kushuka daraja.

**12. Ruvu Shooting**
Jana ilitarajiwa kucheza dhidi ya Stand United. Kabla ya mechi hiyo ilikuwa na pointi 36 kama Kagera Sugar. Itakuwa imebakisha mechi tano ili imalize ligi, lakini pointi ilizo nazo itabidi ifanye kitu ili kuendelea kusalia Ligi Kuu.

**13. Ndanda FC**
Baada ya sare dhidi ya Yanga jana ilitarajiwa tena kucheza dhidi ya Coasta Union. Kabla ya mechi ya jana ilikuwa na pointi 36 na imeanzisha kampeni kabambe kuhakikisha haipotezi mechi nyumbani ili kubaki salama kwenye Ligi Kuu.

**14. Stand United**
Jana ilitarajiwa kucheza dhidi ya Ruvu Shooting, lakini kabla ya hapo ilikuwa na pointi 36 tu. Ni pointi ambazo bado haziipi uhakika wa kubaki Ligi Kuu, na itakuwa imebakisha mechi tano baada ya mchezo huo.

**15. Mbao FC**
Ilitarajiwa kucheza dhidi ya Azam jana, lakini imekuwa haina mwendelezo mzuri kwenye mechi zake za hivi karibuni. Itakuwa imebakisha mechi tano. Kabla ya mechi ya jana ilikuwa na pointi 36. Kama ikiendelea na mwenendo usioridhisha msimu huu unaweza kuwa wa mwisho kucheza Ligi Kuu.

**16. Biashara Mara**
Ina pointi 34 tu. Iko kwenye mstari wa hatari wa kushuka daraja kama isipochukua hatua. Imebakisha mechi saba kumaliza ligi, hivyo ina mtihani mkubwa ili isirudi ilikotoka.

**17. African Lyon**
Ni timu inayoburuza mkia kwenye Ligi Kuu. Ina pointi 22 tu. Imebakisha mechi sita tu. Kimahesabu inaonekana kama ikipambana kwenye mechi zake zilizobaki haitoshuka, lakini kimtazamo inaonekana ni moja kati ya timu zitakazoshuka daraja msimu huu.

## Extra Time


# Watano wenye nafasi kutwaa PFA England

### NUKUU

"Ubingwa wa Ligi Kuu England ndilo tunalowaza kwa sasa, kunyanyua kombe ndilo jambo muhimu kwetu, tunataka kurejesha hali hiyo japokuwa siyo kazi nyepesi. Nataka nikiondoka niwe nimeshinda mataji, likiwamo la Premier League, ikiwa hivyo nitakuwa najivunia uwapo wangu klabuni hapa," **kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, alisema baada ya kutangazwa rasmi kuinoa timu hiyo huku akiongeza:** "Nina furaha na ni mtu ninayepambana, nataka siku nikiondoka niwe na heshima."



"Sijafunga katika michezo michache, lakini kuna baadhi ya wachezaji ambao wana mabao sawa na mimi, na hakuna mtu anayezungumza kuwahusu wachezaji hao watatu ama wanne ila watu wanasema wachezaji hao wana msimu mzuri katika maisha yao, ninachotaka ni kutwaa tu ubingwa wa Ligi Kuu hicho ndicho kitu muhimu kwangu," **Mohamed Salah aliiambia Sky Sports kabla ya kuziona nyavu wiki iliyopita dhidi ya Southampton.**



"Nitoe wito kwa viongozi, wachezaji na walimu wa [Taifa Stars] kufanyia kazi upungufu uliojitokeza kwenye michezo iliyotangulia ili kujiweka sawa na michuano ya Juni mwaka huu [Afcon 2019 nchini Misri]. Napenda mtambue kwamba lengo letu ni kwenda kushindana na si kushiriki. Niwatakie maandalizi mema na mafanikio katika michuano hiyo inayokuja," **Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwasilisha hotuba yake bungeni mjini Dodoma wiki iliyopita.**





David Silva



Sergio Aguero



Raheem Sterling



Virgil Van Dijk

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England imeingia kwenye awamu yake ya mwisho, huku Manchester City na Liverpool zikiwa kwenye mbio moja ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo. Zikiwa zimebaki mechi tano ligi hiyo kufikia mwisho, kuna vitu vingi vinaendelea kwenye kuwania ubingwa.

Ukiacha mbio za ubingwa wa Ligi Kuu kwa timu, lakini pia wachezaji nao wapo kwenye mbio zao za kutaka kupata mafanikio binafsi wakati kila mmoja akiwa na lengo la kuhakikisha anakuwa katika ubora wake.

Tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka wa Ligi Kuu ina ushindani mkubwa baina ya wachezaji na kila mchezaji anajiweka kwenye nafasi ya kutaka kuibeba tuzo hiyo.

Mohamed Salah ni mchezaji ambaye alishinda tuzo hiyo msimu uliopita, lakini sasa ni wazi kwamba kutakuwa na ushindani mkubwa wa mbio ya kuitwaa tuzo hiyo.

Wachezaji kama Eden Hazard, Paul Pogba, Harry Kane, Son na Aubameyang wanaonekana kuwa kwenye kiwango cha kuvutia.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wana nafasi kubwa ya kuitwaa tuzo hiyo mwishoni mwa msimu, maarufu kama PFA:

**5. Mohamed Salah**

Mohamed Salah anapigania kutetea tuzo yake hiyo ya PFA kwa mwaka huu. Ni mchezaji ambaye anatafuta kufikia mafanikio ya nyota wa zamani wa ligi hiyo kama Thiery Henry na Cristiano Ronaldo ambao waliitwa tuzo hiyo mfululizo. Mchezaji huyo raia wa Misri alishinda tuzo hiyo baada ya kuvunja rekodi yake akiwa anacheza kwa msimu wake wa kwanza pale Liverpool.

Nyota huyo wa zamani wa AS Roma amecheza mechi 32 kwa 'Wekundu' hao kwenye Ligi Kuu msimu huu na akifunga mabao 17. Ukiacha mabao 18 aliyofunga, raia huyo wa Misri ametoa pasi za mwisho nane kwa jina lake. Nyota huyo wa Liverpool anayevaa jezi namba 11 ana takwimu ya kufunga bao kila baada ya dakika 161.

Salah alianza msimu huu taratibu, lakini ameweza kurudi kwenye kiwango chake kadri msimu unavyokwenda. Amezifunga kwa urahisi timu za chini, lakini ameshindwa kufunga dhidi ya timu nne kubwa za juu. Salah kiwango pekee alichokionyesha ni dhidi ya Arsenal wakati alipofunga moja na kutengeneza moja.

**4. David Silva**

David Silva kwa miaka mingi amekuwa mmoja wa viungo wasioshuka kiwango duniani na amekuwa kwenye ngazi zilezile kama Modric, Kroos, De Bruyne na Pogba.

Raia huyo wa Hispania amekuwa mmoja wa nguzo muhimu zaidi kwa wachezaji wa Pep Guardiola wakati Manchester City ikipigania kutetea taji la Ligi Kuu. Silva amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi na kuisaidia Man City wakati ambao inahitaji msaada wake.

Ukiacha uwezo wake wa kuubadilisha mchezo, kiungo huyo amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho sita. Katika umri wake wa miaka 33, ametengeneza nafasi nzuri kubwa za kufunga kwa wachezaji wenzake mara 13, ikiwa ndiye mchezaji wa pili wa kutengeneza pasi nzuri ukiacha, Ryan Fraser ambaye anaongoza kwa kutengeneza pasi hizo mara 21.

Mchezaji huyo wa zamani wa Valencia alikuwa ndiye nguzo ya safu ya kiungo kwa Man City wakati Kevin De Bruyne alipokuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi kadhaa. Silva amekuwa mmoja wa viungo bora kwenye Ligi Kuu mwaka huu.

**3. Sergio Aguero**

Sergio Kun Aguero amekuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani kwa sasa na amejiimarisha yeye mwenyewe.

Raia huyo wa Argentine kwa sasa anaongoza katika safu ya ufungaji akiwa na mabao 19 kwa jina lake. Ukiacha uwezo wake wa kufunga mabao 19, ametoa pasi za mwisho saba. Mkongwe huyo ana jicho nzuri zaidi akiwa kwenye lango la goli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, awali alionekana kama angepata ushindani baada ya ujio wa Gabriel Jesus, lakini akaweza kujiimarisha yeye mwenyewe na kujikuta akipata nafasi nyingi zaidi za kucheza na kufunga mabao.

Amekuwa nguzo muhimu kwa Kocha Pep Guardiola na alikuwa mwiba kwa timu kama Arsenal na Chelsea wakati akifunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi yao katika dimba la Etihad.

Na kiwango hicho kinamfanya jina lake kuonekana kuwa kwenye orodha ya wachezaji ambao wanapewa nafasi kubwa ya kuwania tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu, PFA.

**2. Raheem Sterling**

Raheem Sterling yupo kwenye kilele cha juu kwa sasa. Winga huyo wa Manchester City anatengeneza nafasi nyingo na kufunga kila anapopata nafasi. Amejiimarisha na kuwa mmoja wa mabingwa bora duniani kwa sasa chini ya kocha Guardiola. Sterling amekuwa mmoja wa nguzo ya mafanikio ya Man City msimu huu. Kwa sasa Sterling amepevuka vya kutosha zaidi hasa wakati alipoonyesha uwezo wa hali ya juu wakati Sergio Aguero na Kevin De Bruyne wakiwa nje ya dimba kutokana na majeraha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amefunga mabao 15 kwa jina lake na amepitwa mabao manne tu na Aguero ambaye anaongoza kwenye ufungaji bora. Ukiacha kufunga mabao 15, ametoa pasi za mwisho 11 kwa jina lake. Raheem Sterling pamoja na Aguero wametengeneza upatina mzuri zaidi kwenye kufunga mabao. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa na rekodi ya kufunga bao kila baada ya dakika 149.

Kama Man City wakitwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, Aguero na Sterling ndio watakuwa chachu kubwa zaidi.

**1. Virgil Van Dijk**

Virgil Van Dijk anaonekana amekamia zaidi katika kuwania tuzo ya PFA kama ilivyo kwa Raheem Sterling, Aguero na wachezaji wenzake pale Liverpool, Sadio Mane na Salah. Van Dijk amekuwa beki wa kwanza kuwania tuzo hiyo baada ya John Terry ambaye aliitwa tuzo hiyo mwaka 2005. Tangu hapo N'golo Kante aliitwa mwaka 2017.

Liverpool ilivunja rekodi ya usajili kwa kumsajili Van Dijk wakati walipolipa ada ya pauni milioni 70 kumsajili Mholanzi huyo. Na sasa Van Dijk amekuwa akilipa fadhila zake kwa Wekundu hao.

Van Dijk pamoja na Alisson ndio wachezaji pekee wameanza kwenye mechi zote 32 na kuwa historia akiwa amecheza mechi 17 bila kuruhusu nyavu zake kutingishwa. Mholanzi huyo amecheza katika kila dakika 90 kwenye Ligi Kuu.

## Michezo



Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akijaribu kuwatoka mabeki wa TP Mazembe ya DRC kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ilichezwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na timu hizo kutoka sare ya bila kufungana.

# SABABU SIMBA KUTOKA SARE NA TP MAZEMBE

**Na Adam Fungamwango**

KINACHOTAKIWA sasa kwa Simba ni kwenda ugenini na kushinda angalau bao 1-0 au kutoka sare yoyote ya mabao ili kuweza kusonga mbele kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ni baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni mechi kali, iliyosubiriwa na watu wengi na kutazamwa na idadi kubwa ya mashabiki kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Hii ni mara ya kwanza kwa Simba kutoka sare kwenye uwanja wake wa nyumbani baada ya kucheza mechi tano na kushinda zote.

Ilishinda mabao 4-1 dhidi ya Mbabane Swallow, ikaifumua Nkana FC mabao 3-1, kabla ya kuitwanga Saoura mabao 3-0.

Baada ya hapo ikainyuka Al Ahly bao 1-0, na AS Vita akafa mabao 2-1, kabla ya mechi ya sita kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya TP Mazembe.

Lakini kwa nini Simba imelazimishwa sare kwenye mechi hii? Mwandishi wa makala haya anaeleza baadhi ya sababu alizoziona kwenye mechi hiyo na pia jinsi mechi ilivyokuwa...

1. TP Mazembe walipoozesha mechi
Simba waliingia kwenye mtego wa kucheza soka la taratibu la TP Mazembe.

Wachezaji wengi wa TP Mazembe wana miili mikubwa, na si watamu sana kwa soka la kasi, hivyo walikuwa wakicheza taratibu kila wanapopata mpira na kwa bahati mbaya sana, Simba nayo iliiga mchezo wao na hapo ndipo walipopotea kwani ndicho walichokuwa wakihitaji.

Kama Simba ingeanza kucheza mchezo wa kasi kama ilivyocheza dhidi ya AS Vita, nadhani TP Mazembe ingekuwa kwenye wakati mgumu.

Vile vile kutokuanza tangu mwanzo kwa Emmanuel Okwi pia kuliiathiri Simba kwa sababu hakukuwa na mchezaji mwenye kasi ambaye angeweza kuwapeleka mbio na kuwavuruga mabeki wa timu pinzani.

**2. Viungo hawakuwa kwenye kiwango**

Baadhi ya wachezaji wa Simba hasa viungo hawakuwa kwenye viwango vyao vya kawaida.

Hii iliwafanya kushindwa kutengeneza nafasi kwa washambuliaji ambao walikuwa wamekabwa vema na walinzi warefu na wenye miili iliyoshiba wa TP Mazembe.

Chama na Haruna Niyonzima hawakuwa wale ambao mashabiki wamewazoea, kwani walishindwa kabisa kupenya ngome ya wapinzani na kuwafanya walinzi kutetereka kiasi cha kuwapa mwanya mastraika kufanya vitu vyao, badala yake muda mrefu walikuwa wakiuchezea mpira katikati ya uwanja na kucheza pasi fupifupi zisizokuwa na sababu wala malengo na hivyo kunyang'anywa kiurahisi na wapinzani.

Mwingine ni kiungo wa kukaba, Jonas Mkude naye pia alikuwa hafanyi majukumu yake ipasavyo ya kukaba, lakini pia hata anapopata mpira hakuwa na jicho la mbali la kupeleka mpira sehemu ambayo inaweza kuwa hatari kwa wapinzani, badala yake kutoa pasi za papo kwa hapo. Kiungo pekee ambaye siku zote huwa hajawahi kuonekana akicheza chini ya kiwango ni James Kotei. Huyu ndiye roho ya Simba pale katikati kwa sasa, kwani alifanya kazi kubwa ya kuwasaidia mabeki wa timu yake wasipate kashikashi nyingi.

**3. Penalti ya Bocco iliwatoa mchezoni**

Baada ya nahodha wa Simba, John Bocco kukosa mkwaju wa penalti dakika ya 59, wachezaji wa timu hiyo walionekana kutoka mchezoni. Ile hali ya upambanaji ikapotea na walikuwa wakicheza ili mradi tu sasa chochote kitokee, tofauti na mwanzo ambapo angalau ilionekana kuwa kitu kinatafutwa.

Iwapo kama Bocco angepata mkwaju ule, wachezaji wa Simba wangepata ari kubwa ya kupambana, lakini hata TP Mazembe pia wangefunguka kutafuta bao la kusawazisha na hapo ndipo mashabiki wangeweza kuona burudani zaidi, tofauti na walivyoiona.

**4. Tofauti kati Simba na TP Mazembe**

Kulionekana utofati mkubwa kati ya wachezaji wa Simba na TP Mazembe. Kwenye hatua kubwa kama hizi ndipo unapoweza kuona tofauti kati ya wachezaji wenye viwango vya juu na wale wa chini, pia wa gharama kubwa na wa bei ya chini.

Wachezaji wa TP Mazembe wote walionekana wako vizuri kwenye utimamu wa mwili, lakini pia uwezo wa kumiliki mpira kwa mchezaji mmoja mmoja. Wachezaji wengi wa TP Mazembe walikuwa na uwezo wa kukaa na mpira kwa muda mrefu, lakini pia kuupeleka sehemu husika na kwa wakati sahihi.

Ni tofauti na wachezaji wa Simba wengi walionekana hawakuwa na utimamu kimwili kuwashinda wenzao, lakini bado walionekana kulazimisha kushindana ubavu na wenzao badala ya kucheza soka la haraka. Pia wengi hawakuwa na uwezo wa kuumiliki mpira na kukaa nao muda mrefu, lakini vile vile hata pasi zao zilikuwa mbovu, kwa sababu hazikuwa na malengo, hazikuwa zikienda eneo husika kwa wakati sahihi, huku baadhi ya wachezaji wakikaa na mpira bila sababu.

**5. Uzoefu uliwabeba Mazembe**

Kucheza michuano hii kwa muda mrefu pia kuliibeba TP Mazembe kupata sare dhidi ya Simba.

Wachezaji wa timu hiyo wanaonekana kuwa wamezoea kucheza mechi za ugenini zenye presha kali ya wapinzani ndani ya uwanja pamoja na mashabiki wao majukwaani. Walionekana kutulia wakicheza bila papara na kwa nidhamu ya hali ya juu.

Hili ndilo linalowashinda Simba wanapokwenda kucheza ugenini. Nadhani ni kwa sababu ya ugeni wao.

**6. Mashabiki Simba kushindwa kuifaidisha timu yao**

Pamoja na wingi wa mashabiki wa Simba uwanjani, lakini walishindwa kuifaidisha timu yao kwa wingi wao hususan kushangilia kwa nguvu ili kuwapa presha kubwa wapinzani na kuongeza morali kwa wachezaji wao.

Mashabiki wa Simba wamekuwa wakikosa sifa hiyo katika michuano hii kwenye mechi zote Simba imekuwa ikicheza nyumbani, kwani wamekuwa wakishangilia tu pindi wanapofunga ama kuvutiwa na mchezaji fulani kumlamba mpinzani kanzu, na ikitokea kutangulia kufungwa hunywea kama wamemwagiwa maji baridi.

Kama wangetumia wingi wao kuzomea wapinzani wanapogusa mpira kwa aidha, kusema "buuu" na wachezaji wao wanapogusa mpira hata kwa kupiga tu makofi, ingewapunguza nguvu wapinzani na kuongeza morali kwa Simba, hilo ni jambo wanapaswa kujifunza kwa siku zijazo.

**NAJUA WAJUA**

KADI nyekundu mwamuzi Mike Dean aliyomwonyesha Ashley Young dhidi ya Wolves wiki iliyopita, ni ya 100 kutolewa na refa huyo kwenye michuano ya Ligi Kuu England, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuwahi kutolewa na refa yeyote katika historia ya ligi hiyo. Aidha, kadi zote nyekundu alizowahi kuonyeshwa Young kwenye Ligi Kuu, ameonyeshwa na Dean nyingine ikiwa ni (Januari 2009 katika mechi ya Aston Villa vs Sunderland).



MAKALA

# MABEKI WA3 WANAOWEZA KUWA VAN DIJK WA UNITED




Kalidou Koulibaly

**LONDON,** England

VIRGIL van Dijk ni mchezaji muhimu zaidi katika mafanikio ya hivi karibuni ya Liverpool. Beki huyu wa kati akiwa yupo kwenye klabu hiyo si zaidi ya mwaka mmoja sasa, lakini tangu nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi alipojiunga na 'Wekundu' hao, wamepoteza michezo minne tu kwenye Ligi Kuu, wakifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na hivi sasa ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England.

Salah, Firmino na Mane pengine wanafunga vizuri mabao kule mbele, lakini Van Dijk ndiyo sababu Liverpool imeruhusu mabao 20 tu msimu huu kwenye Ligi Kuu na kuifanya kuwa moja ya timu yenye beki bora EPL.

Yeye si tu anayeongoza timu, lakini pia ndiye anayeimarisha ulinzi wa timu hiyo na mchezaji huyo wa zamani wa Southampton yupo kweye kiwamgo bora kabisa. Yeye hakuwahi kupigwa chenga msimu huu, mafanikio yaliyofikiwa na Alessio Romagnoli na Omar Colley kule kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Ameonekana kuwa mchezaji muhimu zaidi katika kila mchezo. Virgil ana wastani wa usahihi wa pasi kwa asilimia 89.6.

Manchester United, kwa upande mwingine haina beki wa kati mwenye daraja la Van Dijk. Kuanzia kutoka kwa Victor Lindelöf, hakuna beki wa 'Mashetani Wekundu' hao ambaye anaweza kufikia kwenye kiwango chake.

Lakini sasa Man United imekuwa ikiwania kutaka kumsajili beki wa kati ambaye yupo kwenye daraja la Van Dijk.

Katika makala haya tunakuchambulia mabeki ambao wanaweza kuwa kwenye kiwango sawa na Van Dijk...

**3. Matthijs De Ligt**

De Ligt ndiye mchezaji kijana zaidi katika orodha hii. Katika umri wa miaka 19, yeye ndiye mchezaji mwenye uzoefu mkubwa zaidi katika orodha hiyo. Zao hili la timu ya Ajax, tayari ameonyesha umuhimu wake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwenye Ligi ya Mataifa ya Ulaya. Ana kipaji cha hali ya juu na kisichochuja kati ya mabeki bora Ulaya kwa sasa.

Kutokana na umri wake, Mholanzi huyo sio tu kiongozi, lakini pia ni nahodha wa Ajax. Na De Ligt pamoja na umri wake ana nafasi ya kuweza kuwa beki kiongozi kwenye timu ya Ligi Kuu.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 anaweza kuizoea haraka Ligi Kuu ya England iwapo atatua pale Manchester United.

Unaweza kuona kijana huyo kwa kiasi fulani ni kama anamfikia kitakwimu Dijk. Na ataweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho. Hata hivyo, nyota huyo anaweza kuigharimu fedha nyingi zaidi Man United, kwa kuwa bei yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 80. Lakini pamoja na yote, klabu kama Barcelona na Liverpool nazo zinainyatia saini yake.

**2. Toby Alderweireld**

Alderweireld ndiye mchezaji pekee kwenye orodha hiyo ambaye ana uzoefu wa kucheza kwenye Ligi Kuu. Staili yake ya uchezaji kwa kiasi kikubwa inafanana na Van Dijk. Pia ni mzuri zaidi kwenye kuwapanga wachezaji wenzake kwa ajili ya mashambulizi ya mbele. Ni mchezaji asiyechuja kiwango, akiwa pia si mtu wa kufanya makosa mara kwa mara.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ndiye mwenye umri mkubwa zaidi katika orodha hiyo. Katika umri wake wa miaka 30, anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwa Man United.

Pamoja na yote Alderweireld mara zote hajawa kiongozi wa safu ya ulinzi, kwani mara nyingi amekuwa akicheza kama nahodha. Hiyo imechukuliwa kama tatizo kwa Manchester United kuweza kujijenga zaidi. Lakini kwa uwezo wa wachezaji kama Shaw na Lindelöf, wanaweza kuwa msaada wa uongozi kwake.

Ukiangalia kwa takwimu, inashangaza kwamba, Alderweireld ni bora zaidi kuliko Van Dijk, linapokuja suala la mipira mirefu. Huyu anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwa kikosi cha Manchester United hasa kutokana na staili yake ya uchezaji. Lakini katika umri wake wa miaka 30 bei yake inaweza kuwa sio kubwa na thamani yake ni dola milioni 25.

**1. Kalidou Koulibaly**

Koulibaly yupo kwenye kilele cha mafanikio ya juu kwa sasa. Beki huyu kiongozi wa Napoli yuko fiti na ana kazi zaidi, na hilo alilithibitisha kwa kuweza kuwazuia Mbappé na Salah kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ni mrefu zaidi kuliko Van Dijk. Raia huyo wa Senegal ni mtengenezaji wa pasi nzuri na zenye macho.

Kwa kitu kingine ni kwamba, hajawahi kucheza kwenye Ligi Kuu ya England, EPL na pengine anaweza kuzoea haraka staili na mfumo wa soka la Ligi Kuu ya England. Lakini tatizo lake kubwa ni mtu wa kutengeneza faulo nyingi zaidi akiwa na takwimu ya kutoa kwa asilimia 1.4 kwa mchezo mmoja.

Koulibaly ni mpole kama ilivyo kwa Van Dijk. Kuwa bora kwa kuzoea haraka mchezo linaweza kuwa tatizo kubwa kwake.

Hata hivyo, raia huyu wa Senegal kiuchezaji anafanana na Van Dijk na anaweza kuongoza safu ya ulinzi. Ana uwezo wa kuwatisha wachezaji washambuliaji wa timu pinzani kutokana na kiwango chake.

Lakini atawagharimu zaidi Man United kwani thamani yake ni kati ya pauni milioni 90 hadi 140.

**NDANI YA 18**

WOLVES ndiyo timu iliyovuna pointi nyingi zaidi dhidi ya timu sita kubwa ['big six'] kwenye Ligi Kuu England msimu huu kuliko timu nyingine 14 zinazoshiriki kinyang'anyiro hicho (imeshinda- 13, sare nne, na kupoteza tatu).





LIGI Kuu ya England imeingia kwenye awamu yake ya mwisho, huku Manchester City na Liverpool zikiwa kwenye mbio moja ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo. Zikiwa zimebaki mechi tano ligi hiyo kufikia mwisho, kuna vitu vingi vinaendelea kwenye kuwania ubingwa.
Uk. 16-17

# WA5 WANAOTISHA KWA MISHAHARA EPL



Alexis Sanchez

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England ni moja ya ligi inayotazamwa zaidi duniani, huku wadhamini na matangazo ya kwenye televisheni yakipaa kwa mabilioni ya pauni kila mwisho wa msimu.

Kutokana na ligi hiyo kuingiza kiasi kikubwa cha fedha, hata wachezaji nao wanakuwa sehemu ya manufaa hayo, kwani wanajikuta wakilipwa kiasi kikubwa cha fedha kama mishahara yao.

Klabu kama Manchester United, Chelsea, Manchester City na Arsenal mara kwa mara zimekuwa zikiingia kwenye orodha ya timu ambazo zinaingiza fedha nyingi zaidi kwa kupata mapato makubwa.

Sasa kutokana na hilo, makala haya inawatazama wachezaji watano ambao wanalipwa mishahara mikubwa zaidi kwa sasa katika ligi hiyo ikilinganishwa na wachezaji wengine...

**5. Gonzalo Higuain (Chelsea) - Pauni 270,000 kwa wiki**

Mshambuliaji huyu wa kimataifa wa Argentina alisajiliwa kipindi cha majira ya baridi kuchukua nafasi ya Alvaro Morata aliyetimkia Atletico Madrid ili awe patina wa Olivier Giroud.

Chelsea ilimchukua kwa mkopo ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu akitokea AC Milan na walikuwa na matarajio naye makubwa zaidi.

Kwa kuwa aliwahi kucheza chini ya kocha wa sasa wa Chelsea, Maurizio Sarri pale Napoli kwa misimu miwili yenye mafanikio makubwa, walikuwa na imani kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, angekuwa na wakati mzuri zaidi hapo.

Hadi sasa Higuain amefunga mabao matatu katika mechi 10 alizoshuka dimbani na anavuta mkwanja mrefu, kwani kwa wiki yeye anaingiza kiasi cha pauni 270,000.

**4. Paul Pogba (Man United) - Pauni 290,000 kwa wiki**

Baada ya awali kujikuta kwenye wakati mgumu wa kupata namba katika kikosi cha kwanza wakati akiwa kinda hapo Manchester United, Paul Pogba aliondoka na kwenda Juventus kwa uhamisho huru mwaka 2012 na akajikuta kwenye wakati mzuri zaidi katika soka la Italia.

Baada ya miaka minne, Man United wakaamua kumrudisha kwenye dimba la Old Trafford mwaka 2016 na akaanza kwa mafanikio mazuri kwenye safu ya kiungo na alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 89.6.

Chini ya kocha, Jose Mourinho mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, akajikuta akikosa nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi hicho.

Lakini baada ya kuondoka kwa Mourinho Desemba mwaka jana Pogba amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia mno hapo Man United.

Na kwa sasa Pogba analamba kiasi cha pauni 290,000 kila wiki.

**3. N'Golo Kante (Chelsea) - Pauni 290,000 kwa wiki**

Kante ni mmoja wa viungo bora kabisa kwenye Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha miaka mitano sasa, akiwa ametwaa mara mbili mataji ya Ligi Kuu England, huku pia akiwa kwenye kikosi cha Ufaransa kilichotwaa Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka jana.

Katika umri wake wa miaka 27, amekuwa mwenye kiwango kizuri pale Chelsea akicheza kama mhimili mkuu wa kikosi hicho.

Huku akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu kubwa kama Real Madrid, Mfaransa huyo aliamua kuongeza mkataba wake hapo Chelsea Novemba mwaka jana na sasa Kante anatia mfukoni kiasi cha pauni 290,000 kwa wiki.

**2. Mesut Ozil (Arsenal) - Pauni 350,000 kwa wiki**

Mesut Ozil alivutia macho ya wengi kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil wakati Ujerumani ikilitwaa taji hilo. Kipindi hicho alikuwa ana umri wa miaka 22 tu, lakini uwezo wake dimbani ulikuwa gumzo kubwa, na kwenye mchezo wa nusu fainali ya michuano hiyo wakati Ujerumani ikiimwagia mvua ya mabao saba Brazil, yeye ndiye alikuwa mpishi mzuri pale kwenye dimba la kati.

Kiwango chake hicho kule Brazil, kikavuta hisia za Real Madrid na wakamsajili na kutua pale kwenye dimba la Bernabeu, akicheza pamoja na Cristiano Ronaldo.

Baada ya kuwa na mafanikio makubwa na Los Blancos hao, kocha wa Arsenal wa wakati huo, Arsene Wenger akavutiwa naye na akamsajili kwa pauni milioni 40 mwaka 2013, na kumfanya Ozil kuwa mchezaji ghali zaidi katika historia ya Arsenal.

Kwa kipindi cha miaka mitano, Ozil ametoa mchango mkubwa kwa 'Washika Bunduki' hao.

Hivi sasa akiwa amebakiza miezi sita katika mkataba wake, bado hajasaini mkataba mpya. Hata hivyo, mkataba wake wa sasa unamfanya Ozil kutia mfukoni kiasi cha pauni 350,000 kwa wiki.

**1. Alexis Sanchez (Man United) - Pauni 400,000 kwa wiki**

Mashabiki wa Manchester United walishangilia mno wakati klabu yao ilipofanikiwa kuinasa saini ya Alexis Sanchez na kuwazidi kete wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City.

Mashabiki hao waliamini kwamba, mchezaji huyo raia wa Chile atakuwa na msaada mkubwa kwao, lakini mambo yamekwenda kinyume chake.

Kwa kipindi cha miaka minne, mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 30, ameshindwa kufikia mafanikio aliyoyapata kule Arsenal na kujikuta akiwa na wakati mgumu zaidi hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Hadi sasa Sanchez amecheza mechi 41 kwa Man United, lakini amefunga mabao matano tu katika mashindano yote, lakini ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu ya England. Sanchez analipwa kiasi cha pauni 400,000 kwa wiki.

**USILOLIJUA**

LIVERPOOL imekuwa timu ya saba kwenye historia ya Ligi Kuu England kuruhusu mabao 5,000 baada ya Everton, Manchester City, Aston Villa, Newcastle, Sunderland na Arsenal.







## Wazazi CCM yaanzisha miradi ufugaji nyuki shule za sekondari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, imeanzisha mradi wa somo la nyuki ambao hautaingiliana na masuala ya taaluma, katika shule zote za sekondari zinazomilikiwa na jumuiya hiyo.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Dk. Edmond Mndolwa, wakati wa ziara ya kutembelea baadhi ya shule za sekondari za jumuiya hiyo.

Alisema mradi wa nyuki shuleni utamsaidia mwanafunzi kuondokana na utegemezi kwa kuwa atajifunza mbinu mbalimbali za namna ya kuendeleza mradi huo ili kujiongeza kipato akiwa shuleni na baada ya kumaliza shule.

Alisema somo la nyuki litafundishwa muda wa ziada ili kuepusha mwingiliano na masomo mengine na kupitia somo hilo wadau mbalimbali watajitokeza kuwapata maarifa ya kuongeza uzalishaji.

"Hii ni miongoni mwa mipango kabambe ya kuhakikisha Chama Cha Mapinduzi kinasaidia jamii, tunaanzisha mradi wa somo la nyuki shuleni ili kuwaisaidia wanafunzi kujitegemea na kujiingizia kipato ambacho kitawasaidia kutatua changamoto zinazowakabili," alisema Mndolwa.

Alizipongeza shule zinazomilikiwa na jumuiya hiyo hususani Sekondari ya Ivumwa kwa kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa na kukipa sifa Chama Cha Mapinduzi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi kutoka jijini Dar es salaam, Frank Kamugisha alisema tayari ameshaanza maandalizi ya kuhakikisha shule zote zinaanza kufundisha somo la nyuki.

Hata hivyo Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Solomoni Itunda, alimhakikisha Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo taifa kuwa mradi wa somo la nyuki utatolewa kwa shule zote za sekondari zinazomilikiwa na jumuiya hiyo.

Alisema kupitia mradi huo wanategemea mambo makubwa ikiwamo kuzalisha ajira kwa wingi kupitia mradi huo kwa kuwa vijana watajiajiri na kuajiriwa.

# Umakini unahitajika uandikishaji Daftari la Mpigakura

**Na Grace Mwakalinga** MBEYA

VIONGOZI wa serikali mkoani Mbeya wametakiwa kusimamia kwa karibu uandikishaji wa Daftari la Mpigakura litakapoanza ili kuepuka udanganyifu kwa baadhi ya watu.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, James Mwampondele, wakati wa sherehe za maadhimisho ya Wiki ya Wazazi yaliyofanyika kimkoa katika Kata ya Lufingo, wilayani Rungwe.

Mwampondele alisema katika chaguzi zilizopita kulitokea udanganyifu mkubwa kwa watu ambao siyo makazi yao kujiandikisha na kuwataka viongozi wa serikali kutorudia makosa na kuwa makini wakati wa uandikishaji wa wananchi kwenye daftari hilo.

"Tunapojiandaa na mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa inabidi tuwe makini katika uandikishaji wa daftari la wapigakura, hii itasaidia kukabiliana na wimbi la udanganyifu ambalo miaka ya nyuma limekuwa likiharibu uchaguzi, tuhakikishe wanajiandikisha watu sahihi katika maeneo yao," alisema Mwampondele.

Aidha, aliwasisitiza wananchi kuzingatia kanuni na taratibu za uchaguzi ambazo zinataka kila mwananchi aliyefikia umri wa miaka 18 akajiandikishe ili apate haki yake ya msingi ya kupiga kura au kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Katibu Tawala Wilaya ya Rungwe, Nkondola Bendera, alisema wamejipanga kuahakikisha wananchi wanaojiandikisha kwenye daftari la wapiga kura wanatoka maeneo husika na mchakato ukatakapoanza rasmi watatoa elimu ya mpigakura kwenye maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Maadhimisho hayo yalifanyika kwa upandaji wa miti na kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo, ikiwamo kituo cha afya Isongole pamoja na kuwasha umeme katika Shule ya Sekondari Lufingo.

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mbeya, Yahaya Zakaria, alisema jumuiya hiyo imejiwekea mkakati wa kiushindani katika sekta ya elimu lengo likiwa ni kuongeza kiwango cha ufaulu.



Mfanyabiashara wa viatu vya mitumba Soko la Ilala Mchikichini akivisafisha katika banda lake Barabara ya Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Baadhi ya wanawake wamekuwa wakijishughulisha na biashara ya mitumba ili kuongeza pato la familia. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Wadau mtandao wa kijamii wasaidia shule ya wasichana

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WADAU wa maendeleo kupitia jukwaa la mtandao wa kijamii la WhatsApp lijulikanalo kwa jina la 'Rungwe Yetu' wametoa misaada mbalimbali kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kandete iliyopo katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe mkoani Mbeya kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi hao kusoma kwa utulivu.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi misaada hiyo, Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Kenny Lawrence, alisema umekuwa ni utamaduni kwao kushikiri katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika jamii kama vile sekta ya elimu na afya.

Alisema Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kandete imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali hali inayosababisha walimu kushindwa kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Alisema pia watoto wa kike wanashindwa kufurahia elimu kutokana na vikwazo wanavyovipata ikiwamo uhaba wa vifaa vya kujifunzia.

"Jukwaa hili la Rungwe yetu lilianzishwa kwa ajili ya kuisaidia jamii yetu licha ya kuwa kila mwanajukwaa anaishi maeneo tofauti, lakini kupitia Whatsapp tunaungana katika kutatua kero zinazojitokeza tumekuwa na utaratibu wa kusaidia mambo mengi na lengo ni kuhakikisha Busokelo inapiga hatua katika masuala mbalimbali ya maendeleo," alisema Lawrence.


Miongoni mwa wana jukwaa hilo, Ezekiel Gwatengile, alisema msaada huo utasaidia kupunguza adha kwa walimu na kuendelea kuisaidia shule hiyo kutengeneza mazingira rafiki ili mtoto wa kike asome kwa furaha na kufaulu masomo yake.

Naye Suma Mwakasitu aliahidi kutoa Sh. 250,000 kwa ajili ya kununulia taulo za kike na kuahidi kufanya hivyo mara kwa mara ili wanafunzi wasome kwa amani na utulivu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, aliwashukuru wadau wa maendeleo kwa misaada yao ambayo alisema itasaidia kupunguza changamoto ya vifaa shuleni hapo.

Alisema halmashauri imejitahidi kujenga miundombinu rafiki kwa ajili ya wanafunzi, lakini kuna changamoto ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na chumba maalum kwa ajili ya watoto wa kike wanapokuwa kwenye hedhi.

Aliwaomba wadau hao kuendelea kutoa misaada ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uzio kwenye mabweni ya watoto wa kike ili kuwalinda na vitendo vya ukatili kama vile ubakaji.





# Mwarobaini wa ukosefu wa ajira wapatikana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema vijana wengi walikuwa wanakosa ajira kwa kigezo cha kutokuwa na uzoefu.

Hata hivyo, kupitia mradi wa kujenga stadi na uwezo chini ya ofisi yake wameweza kutatua changamoto hiyo.

Mhagama alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika semina ya wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, jijini hapa.

"Kwa sasa tumekubaliana na sekta binafsi kwamba tunataka ifike mahali kila mmoja aone anao wajibu wa kumchukua kijana wa Tanzania aliyehitimu kumpeleka kwenye kampuni yake apate uzoefu na ujuzi na hatimaye aweze kuajirika," alisema.

Alisema kupitia mradi huo wengi wameshaanza kuchukuliwa na wanapata ajira.

Akitoa mada katika semina hiyo Mkurugenzi wa Chama cha Ushirika cha Wahitimu wa Chuo cha Kilimo Sokoine (SUGECO), Joseph Masimba, alisema waliamua kuanzisha ushirika huo ili kusaidia vijana wanaotaka kujiajiri wenyewe.

"Sisi tunaamini kilimo lazima kifanywe na watu wenye maarifa, msingi wa mafanikio kwenye kilimo ni maarifa sahihi, shida kubwa tuliyoiona katika hili ni mind set ya vijana katika maeneo mengi, sisi tunasema ukiwa na ardhi isiyo na rutuba hata upande mbegu bora hutapata mazao," alisema Masimba.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kamati hiyo Mohammed Mchengerwa, aliishauri serikali kutoa elimu kwa wahitimu wanaomaliza vyuo vikuu ili waweze kujiajiri kupitia teknolojia ya kitalu nyumba.

"Mtoe elimu hii (ya teknolojia ya kitalu nyumba) kwa wahitimu wanaomaliza vyuo. Kuna vijana wamehitimu degree (shahada) zao wapewe elimu kuhusu kilimo hiki," alisema.

Kadhalika, Mkurugenzi wa Ajira, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Alli Msaki, alisema serikali inatarajia kufikisha utaalamu wa teknolojia ya vitalu nyumba na ulimaji wa mazao ya bustani kibiashara kwa vijana 18,800 nchini ili wapate ujuzi na uwezo wa kuweza kujiajiri wao wenyewe.

Alisema mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa serikali katika kutatua changamoto za ajira kwa vijana na kuboresha kipato cha Watanzania.

"Mradi huu umekusudiwa kutekelezwa kwenye halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na kwamba katika awamu ya kwanza mikoa 12 na halmashauri 83 zitahusika," alisema.

Alisema malengo ya mradi huo ni pamoja na kuwawezesha vijana kuwa na stadi za kazi na stadi za maisha ambazo zinatolewa na mafunzo ya kilimo.

Ili kufanikisha hilo, alisema wataandaa mwongozo wa mamlaka za mikoa, halmashauri za wilaya, manispaa na majiji katika kusimamia utekelezaji wa mafunzo hayo yanatolewa na kusambazwa katika mikoa yote.

# Huduma afya ya mama na mtoto yaimarika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTEKELEZAJI wa Mradi wa Afya ya Uzazi ya Mama na Mtoto mkoani Kigoma umeongeza kinamama kujifungulia kwenye vituo vya afya kwa asilimia 24 ndani ya miaka sita.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Thamini Uhai, Dk. Nguke Mwakatundu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya majadiliano ya wadau wa afya katika kikao kilichofanyika jijini Dodoma.

Mradi huo ambao umefadhiliwa kwa miaka 13 na Taasisi za Bloomberg Philanthropies na Foundation H&B, uliokuwa ukitekelezwa na asasi zisizo za serikali za EngenderHealth na Thamini Uhai na unatarajia kumalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Dk. Mwakatundu alisema asilimia ya wanaojifungulia katika vituo vya afya imeongezeka hadi kufikia 72 kwa mwaka 2017 kutoka asilimia 48 mwaka 2011.

"Takwimu zilizopo sasa zaidi ya watoto 70,000 wamezaliwa katika vituo vya afya vilivyoboreshwa, jambo ambalo pia limesaidia kuzuia takribani vifo 1,100 vya wajawazito na huduma za dharura za uzazi kwa upasuaji katika Mkoa wa Kigoma umeongezeka na kuboresha matokeo ya uzazi salama ya mama na mtoto kutoka asilimia 2.7 mwaka 2011 hadi kufikia asilimia 4.1 mwaka 2017," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi Msaidizi wa Taasisi ya EngenderHealth, Prudence Masako, alisema changamoto ya vifo vinavyotokana na uzazi zinatokana na mambo mbalimbali ikiwamo upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi.

Alisema kupitia Mradi wa Afya ya Uzazi ya Mama na Mtoto kwa Mkoa wa Kigoma umesaidia kuelimisha watoa huduma ya afya na kuboresha vituo ili kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya.

Naye Mwenyekiti wa wabunge wa Mkoa wa Kigoma ambaye pia Mbunge wa Kasulu Mjini, Daniel Nsanzugwako, alikiri kuwa mradi huo umesaidia kupunguza vifo vya wajawazito, takwimu za mwaka 2015 za vifo vimepungua kutoka asilimia 39 hadi 72.

"Mkoa wa Kigoma ulikuwa na matatizo makubwa ya kiafya na ulikuwa nafasi za mwisho mwisho kwenye huduma za afya, na kupitia programu hii sasa tunaanza kuwa ni mikoa ambayo inafanya vizuri," alisema.

Pamoja na hayo, Mkurugenzi Msaidizi Wizara ya Afya, Dk. Ahmad Makuwani, alishauri kuwapo na mtaalamu wa huduma ya usingizi aliyepata mafunzo sahihi kabla ya kuanza shughuli za upasuaji ili kupunguza vifo wakati wa upasuaji kwenye vituo hivyo.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa vifo vya wajawazito 1,747 vilivyotokea mwaka jana nchi nzima asilimia 3.3 vimechangiwa na suala la dawa ya usingizi.



Aliyekuwa mwenyekiti wa wilaya ya Dodoma kupitia Chama cha Demakrasia na Maendeleo (CHADEMA) Yona Kusaja (kushoto) akipokea kadi ya CCM kutoka kwa Mwenyekiti wa chama cha Mapinduzi Dodoma Robert Mwinje baada ya kuamua kujiunga. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mwenyekiti Chadema Dodoma atimkia CCM

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dodoma mjini, Yona Kusaja, amejiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai kuwa amekunwa na utendaji wa Rais John Magufuli.

Diwani huyo alitangaza uamuzi huo jana alipo katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Soko la Majengo mapya jijini hapa.

Kusaja alisema ameamua kuondoka Chadema kutokana na kukunwa na utendaji wa Rais katika miradi ya maendeleo kama vile ya ujenzi wa reli ya kisasa (Standard gauge) umeme, maji, uwanja wa michezo upatikanaji wa ndege za kisasa.


"Kwa kweli sina haja ya kung'ang'ania sehemu ambako kunakwamisha maendeleo ya Watanzania walio wengi, nimeamua mimi mwenyewe bila kupewa kitu chochote kujiunga na Chama tawala Cha Mapinduzi na ninamwakikishia Rais nitaungana naye katika kuhimiza maendeleo bila itikadi yoyote kwa faida ya wananchi," alisema.

Kwa upande wake, Diwani wa kata hiyo Dotto Gombo, aliwataka waliorejea na kujiunga na CCM kuunga juhudi zinazofanywa na serikali za kimaendeleo badala ya kujadili masuala ya vyama walivyotoka.

"Mmejiunga na CCM ambacho kimekuwa kikitenda haki kwa Watanzania katika kuhakikisha maendeleo yanapatikana chini ya Rais Magufuli ambaye haangalii chama chochote kwenye upande wa maendeleo," alisema.

Alisema kuwa ni imani yake kubwa na Watanzania wote kuona kwa upande wao wanahimiza maendeleo kwa wananchi badala ya kuweka mikakati ya kudhoofisha.

Mwenyekiti wa CCM Dodoma, Robert Mwinje, aliwataka kufanya kazi kwa masilahi ya Watanzania wote na kuondokana na dhana waliyokuwanayo ya huko walikotoka kwenye vyama vya upinzani.






Meneja Mauzo wa Vodacom Kanda ya Pwani, Yusuph Ning'angi, akimkabidhi mfano wa hundi ya shilingi 500,000 mmoja wa washiriki wa kampeni ya Vodacom M-Pesa Tuzo Points, Lydia Mwanga, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kupitia kampeni hii wateja 140 wa Vodacom walizawadiwa shilingi 25,000 kila mmoja na baada ya kampeni kumalizika wateja 10 wa Vodacom nchi nzima watazawadiwa shilingi 500,000 kila mmoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake Pangawe watakiwa kujifunza dini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wa Jimbo la Pangawe wametakiwa kujiunga na madrasa ili kujifunza dini ya Kiislamu badala ya kukaa vibarazani kupiga soga.

Wito huo ulitolewa na Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe, Khamis Juma Maalim, Kimara Mkoa wa Mjini Magharibi, alipokuwa akizungumza na kinamama hao.

Alisema elimu ni jambo la msingi ambalo halina umri na hivyo kila mmoja anapaswa kujiendeleza kwa maslahi yake hapa duniani na ahera.

Alisema baadhi ya wanawake hutoa visingizio vya kutokwenda katika madrasa kwa madai kuwa wameshakuwa watu wazima na badala yake kukaa vibarazani na kuzungumza mambo yasiyokuwa na maana.

"Suala la kusoma ni wajibu kwa Muislamu awe mwanamume au mwanamke wote wana haki sawa, hivyo baadhi ya wanawake kutojiunga na madarasa ya watu wa wazima kwa madai ya kuwa hawafahamu kutokana na umri ni kuenda kinyume na maamrisho ya dini ya Kiislamu," alisema.

Aidha, aliwataka wanawake hao kufuata maamrisho ya dini ili kuimarishana mambo mema na kukatazana maovu.

Mwakilishi huyo ambaye pia ni Waziri wa Katiba na Sheria alisema serikali kupitia ofisi ya Mufti imeratibu ziara nchi nzima ya kukagua madrasa ili kubaini mafanikio na upungufu unaokwamisha maendeleo ya madrasa hizo.

# UNFPA yafurahishwa mradi wa mama na mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, limesema mpango kazi wa mradi wa pamoja wa mama na mtoto unaojulikana kama afya bora waliowekeza visiwani Zanzibar unazidi kuleta mafanikio katika lengo la kuhakikisha wajawazito na watoto wanapata huduma bora kabla na baada ya kujifungua.

Akizungumza katika hafla ya kukagua miradi hiyo ambayo waliambatana na wanamawasiliano wa shirika hilo wa Tanzania katika Kituo cha Afya cha Fuoni, Meneja Mawasiliano wa UNFPA, Waren Bright, alisema maendeleo ya mradi huo wa afya bora katika kituo hicho unaridhisha kutokana na kujitokeza idadi kubwa ya wajawazito kujifungua ikilinganishwa na hapo awali kabla ya kuwapo mradi huo.

Kituo cha Afya cha Fuoni ni moja ya kituo kinachotekeleza mradi huo ambao unafadhiliwa na Umoja wa Mataifa pamoja na Shirika la Kuwahudumia Watoto (Save the Children), kwa ufadhili wa watu wa Canada, ulizinduliwa rasmi, mwaka jana ili kuhakikisha wajawazito wanajifungulia katika vituo vya afya na kupata huduma zote anazohitaji.

Alisema maendeleo ya mradi huo ambao katika kituo hicho unajulikana kama afya bora, yatasaidia kupunguza au kutokomeza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Alisema kuwa mbali na kituo cha afya cha Fuoni ambacho kinahudumia zaidi ya shehia tano, pia UNFPA inaangalia mpango wa kupeleka huduma hiyo katika maeneo mengine ya Zanzibar ili kuhakikisha lengo la kutokomeza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua linafikia kwa asilimia kubwa.

"Moja ya malengo ya UNFPA kupitia mradi huu ni tunafanikisha kutokomeza vifo vya mama na mtoto wakati wa kijifungua, hivyo huduma hii pia inahitajika katika maeneo mengine na sisi bado tupo katika malengo yetu kuhakikisha kwa kiasi kikubwa mradi huu unaokoa maisha ya wajawazito, hivyo tutaendelea kupanua mradi huu katika maeneo mengine ya hapa Tanzania na Zanzibar kwa ujumla," alisema.

Mkuu wa Kituo cha Afya cha Fuoni, Abdallah Issa, alisema kutekelezwa kwa mradi huo kumeleta mafanikio makubwa kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wanaofika ikilinganishwa na hapo awali.

Alisema walianza na wagonjwa 700 na sasa wanapokea zaidi ya 1,000 kwa mwezi, kuongezeka kwa idadi hiyo kunatokana na huduma bora inayotolewa katika kituo hicho.

# Karume alisimamia usawa na umoja – Balozi Iddi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema falsafa aliyokuwa nayo Mzee Abeid Amani Karume wakati akipigania ukombozi ilikuwa inaelekeza uhuru, usawa na umoja mambo ambayo baada ya Mapinduzi aliendelea kuyasimamiwa kwa nguvu zake zote na wakati wote wa uhai wake.

Balozi Iddi aliyaeleza hayo wakati akilifungua kongamano la kumuenzi mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar marehemu Mzee Abeid Amani Karume lililofanyika mjini Zanzibar.

Alisema mbegu aliyoipanda mwasisi huyo ya kuheshimu haki za binadamu kwa kufanya mageuzi makubwa ya sera ya magereza hivi sasa mmea wake umechipua vyema na kutoa matunda ya demokrasia sahihi nchini.

Alisema Januari 12, mwaka 1972, Mzee Karume, alitoa amri kwa wafungwa wote waliokuwa kifungoni waachie huru kwa lengo la kuvunjwa kwa magereza na badala yake kuwekwa chuo cha mafunzo ambacho hadi sasa kipo kwa nia ya kumrekebisha tabia mtu anayefungwa ili anapotoka gerezani awe na tabia inayokubalika katika jamii.

Alisema mageuzi hayo yalikuwa ya aina yake kufanyika barani Afrika yamewezesha baadaye kuundwa kwa wizara inayoshughulikia utawala bora, kuwapo kwa sheria na sera tofauti zinazolinda haki za wazee, wanawake na watoto.

Aliwaeleza wanakongamano hao kwamba mbinu alizokuwa akizitumia marehemu mzee Karume zilimsaidia kubadilisha mwonekano wa Zanzibar kutoka kwenye umaskini wa kudhulumiwa na kuelekea kwenye maendeleo ya kudumu kwa wote.

Alieleza kwamba katika kipindi chake cha uongozi marehemu mzee Karume alionekana akitumia muda wake mwingi kutembelea miradi aliyoianzisha ili kuhakikisha kwamba inatekelezwa kwa mafanikio makubwa.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka huu imeamua kuziendeleza kumbukumbu za mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar marehemu mzee Karume katika wiki nzima hadi kilele Aprili 7, kila mwaka.

Shaaban alisema wiki hiyo ya kumbukumbu ya mzee Karume ilibeba mambo mbalimbali yenye masuala ya historia ya ukombozi wa visiwa vya Zanzibar na mtazamo wa baadaye wa kustawisha maisha bora ya wananchi wake. Aprili 7 kila mwaka imetengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa siku maalum ya kumbukumbu ya kuenzi kifo cha marehemu mzee Abeid Amani Karume, ambaye alikuwa jemedari wa Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964 yaliyomng'oa mkoloni katika visiwa vya Zanzibar.

## HABARI KIMATAIFA

# Upinzani Uganda waungana kumng'oa Rais Museveni uchaguzi ujao

**KAMPALA, Uganda**

VYAMA vitatu vya upinzani nchini Uganda vimetia saini mkataba wa ushirikiano kuelekea uchaguzi mkuu mwakani, vikiwa na lengo la kumpata mgombea mmoja atakayepambana na Rais Yoweri Museveni.

Vyama hivyo vilivyotia saini mkataba huo ni pamoja na kile cha DP, kinachoongozwa na Nobert Mao, chama cha People`s Progressive party na chama cha Social Democratic party.

"Sasa tumeungana kwa ushirikiano ikiwa ni pamoja na Alliance for National Transformation, Robert Kyagulanyi (Bobiwine) na People Power. Tutakuwa na mgombea mmoja ambae atapeperusha bendera yetu," alisema Nobert Mao, mmoja wa makada wa chama kimoja cha upinzani kilichoshiriki muungano huo.

Hatua hiyo imesifiwa na Bobi Wine, mwanasiasa kijana nchini Uganda ambaye amepata umaarufu hivi karibuni, huku akibaini kwamba muungano huo wa wapinzani ni tishio kwa Rais Museveni.

"Nimefurahi tumeanza kuungana. Kila saini inaonyesha Museveni leo hii ataondoka madarakani kwa sababu tuko wengi sana na Museveni hana tena nguvu za kuongoza nchi. Wakiomba nipeperushe bendera ya muungano nitafanya hivyo," alisema Robert Kyagulanyi. Hata hivyo, Mike Mukula, naibu kiongozi wa chama tawala NRM, alisema muungano huo hauwatishi.

"Si muungano wakutisha na watu bado wanaona, kwa kweli Rais Museveni bado anazo nguvu, amesimama imara wanampa heshima, huyo mzee atashinda kabisa bila wasiwasi," alisema Mukula.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya siasa wanaona kuwa muungano huu utakuwa na nguvu zaidi iwapo chama kikuu cha upinzani FDC kitaungana na wengine kuongeza nguvu kutokana na umaarufu wa Kiiza Besigye.

Hii ni mara ya tatu kwa vyama vya upinzani kuungana nchini Uganda kuelekea uchaguzi mkuu.

Mwaka 2016, kuliundwa muungano uliofahamika kama Democratic Alliance, lakini haukufaulu kuingia Ikulu ya Entebe. ***RFI***



Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, ambaye amekiri mikakati ya serikali kuidhinisha mpango wake wa Brexit bungeni umefeli. **PICHA: ALLIANCE**

# May akiri Brexit ni ngoma ngumu

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Theresa May, amekiri kuwa mikakati ya serikali kuidhinisha mpango wake wa Brexit bungeni umefeli.

Amesema kuna matarajio madogo kwa wabunge kuunga mkono makubaliano yaliokataliwa mara tatu.

Wakati Uingereza kwa mara nyingine ikibakisha siku chache tu kutoka tarehe ya mwisho ya kuondoka Umoja wa Ulaya (EU), May aliwashinikiza wabunge wa upinzani kusaidia kupatikana kwa makubaliano ya muafaka.

Baada ya makubaliano ya May na EU kukataliwa kwa mara ya tatu na bunge, waziri mkuu huyo alikialika chama cha upinzani cha Labour kujadili mikakati mbadala.

Lakini siku tatu za mazungumzo zilizisha bila makubaliano, chama hicho cha Labour kikiishutumu serikali ya May kwa kutotoa mabadiliko ya kweli.

"Sijaona mabadiliko yoyote makubwa katika msimamo wa serikali mpaka sasa," alisema kiongozi wa Labour Jeremy Corbyn.

Chama cha Labour kinapendelea mchakato mwepesi wa Brexit kuliko ilivyopendekezwa na serikali.

Chama hicho kinasema Uingereza inapaswa kubakia ikiongozwa na sheria za EU kwenye masuala ya biashara na kuendeleza viwango vya kanda hiyo katika maeneo ya haki za wafanyakazi na ulinzi wa mazingira.

Uingereza inatarajiwa kujiondoka EU siku ya Ijumaa iwapo May hatopata makubaliano ya kurefusha tena mchakato kutoka EU, ambao tayari ulikubali kurefusha siku ya Brexit iliyopangwa awali kuwa Machi 29.

May sasa anaomba muda wa kuondoka Uingerea urefushwe hadi Juni 30, akitumai kufikia muafaka na chama cha Labour na makubaliano kupitishwa na bunge katika muda wa wiki chache.

"Kadri hii inavyochukuwa muda mrefu, ndivyo hatari inavyoongezeka ya Uingereza kuondoka kabisa," alisema May katika taarifa.

Mwezi uliopita, EU uliipa muda zaidi Uingereza hadi Aprili 12 kuidhinisha makubaliano ya kujiondoa katika jumuiya hiyo uliofikia na serikali ya May. ***DW***

# Waandamana mbele ya makao makuu ya jeshi

**KHARTOUM, Sudan**

MAELFU ya waandamanaji nchini Sudan kwa mara ya kwanza juzi waliandamana hadi katika makao makuu ya jeshi jijini Khartoum, wakiendelea kushinikiza kujiuzulu kwa Rais wa nchi hiyo, Omar Al Bashir.

Waandamanaji hao wakiwa wamebeba mabango huku wakiimba nyimbo mbalimbali za kushinikiza Rais Al Bashiri kuachia madaraka, hata hivyo maandamano hayo yaliendelea licha ya serikali kutangaza hali ya hatari nchini humo.

Wakiwa wameshika mabango, waandamanaji hao walisikika wakisema lengo la kufika katika makao makuu ya jeshi ni kutuma ujumbe mzito kwa wanajeshi kuamua iwapo wanasimama na wananchi au hapana.

"Bado hatujatimiza lengo letu, lakini ujumbe wetu umefikia uongozi wa jeshi, tunamtaka Rais Bashir ajiuzulu," mmoja wa waandamanaji Amir Omer alisikika akisema.

Maandamano hayo pia yalifanyika katika mji mwingine wa Omdurman na kusababisha mtu mmoja kupoteza maisha.

Rais Omar Al-Bashir mwenye umri wa miaka 75, amekuwa akiongoza nchi hiyo kwa miaka 26.

Hivi karibuni, Rais Al-Bashir alinukuliwa akisema anaelewa baadhi ya malalamishi ya waandamanaji hasa suala la ukosefu wa ajira kwa vijana, na kuahidi kuja na mpango wa kutekeleza hilo. Hata hivyo, anawashatumu wapinzani wa kisiasa kwa kuchochea maandamano hayo.

RFI

**"Bado hatujatimiza lengo letu, lakini ujumbe wetu umefikia uongozi wa jeshi, tunamtaka Rais Bashir ajiuzulu," mmoja wa waandamanaji Amir Omer alisikika akisema.**

# Idadi ya wazee duniani ni kubwa kuliko watoto

**WASHINGTON, Marekani**

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema kwa mara ya kwanza katika historia, kuna idadi kubwa ya wazee duniani kuliko watoto.

Takwimu zinaonyesha kuwa watu wenye umri wa miaka 65 ni wengi ukilinganisha na wale walio chini ya miaka mitano mwishoni mwa mwaka 2018.

Kwa sasa kuna watu takriban milioni 705 wenye miaka zaidi ya 65 duniani, wakati wenye umri kati ya miaka 0-4 ni takriban milioni 680.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti na Tathmini ya masuala ya Afya ya Chuo Kikuu cha Washington, Christopher Murray, alisema kutakuwa na watoto wachache sana na watu wengi sana walio na umri wa miaka zaidi ya 65, hali itakayowia vigumu dunia kuendelea.

"Fikiria kuhusu athari za kisosholojia na kiuchumi kwa jamii yenye watu wenye umri mkubwa wengi kuliko watoto," alisema Murray.

Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia (WB) mwaka 1960, uwiano wa uzao ulikuwa karibu watoto watano kwa mwanamke mmoja. Miaka 60 baadaye uwiano huo umeongezeka kwa 2.4 tu.

Tatizo la uwapo wa wazee wengi ni kubwa katika nchi zilizoendelea.

Kuna kasi ndogo ya kuzaliwa watoto kwa sababu kadhaa ikiwamo sababu za kiuchumi, idadi vifo vya watoto ni ndogo, njia za kupanga uzazi zinapatikana kwa urahisi na kulea watoto ni gharama.

Katika nchi hizo, wanawake hupata watoto wakiwa na umri mkubwa, hivyo huwafanya kuwa na watoto wachache.

Mazingira mazuri ya maisha yao inamaanisha kuwa watu huishi maisha marefu kwenye nchi zilizoendelea, mfano Japan, watu huishi mpaka karibu miaka 84 ambao ni umri mkubwa zaidi duniani.

Hali hiyo imeiogopesha Japan kwa miongo kadhaa na mwaka jana serikali ilitangaza ongezeko la umri wa kustaafu kutoka miaka 65 mpaka 70. ***BBC***

# Wasiojulikana wapora nyaraka, fedha TRA

**Na Shaban Njia na Mohab Dominick, KAHAMA**

WATU wasiojulikana wamevamia na kuvunja dirisha la ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa maalumu wa kikodi Kahama na kuiba baadhi ya nyaraka.

Mbali na nyaraka, pia watu hao wamepora vitendea kazi ikiwamo kompyuta mpakato na fedha taslimu shilingi milioni mbili.

Wezi hao walivamia ofisi hiyo usiku wa manane wa kuamkia Jumamosi kumfunga kamba mlinzi mmoja aliyekuwapo na kuvunja dirisha kisha kuingia ndani ya ofisi, hivyo kufanikiwa kuiba baadhi ya nyaraka, zikiwamo fedha za uendeshaji wa ofisi na kompyuta mpakato, ambayo ni mali ya mhasibu.

Kamishna Mkuu wa TRA, Charles Kichere, alithibitisha kutokea kwa uvamizi wa ofisi hiyo, na kusema ametuma maofisa wake wa kitengo cha mambo ya ndani kwenda kuchunguza tukio hilo.

"Sisi tuna kitengo cha mambo ya ndani, ambacho kwa sasa tumekiagiza kwenda Kahama kuchunguza juu ya wizi uliojitokeza na kutoa taarifa, na hii taarifa ninayokupatia ni taarifa ya awali," alisema Kichere na kuongeza:

"Taarifa kamili zitatolewa pindi uchunguzi utakapokamilika, kwa kuwa tumeshatoa taarifa katika Jeshi la Polisi."

Kuhusu kuibwa kwa baadhi ya nyaraka, Kamishna Kichere alisema hajapata taarifa, na kuongeza kuwa Jeshi la Polisi linamshikilia mlinzi mmoja wa zamu aliyekuwapo siku hiyo kwa mahojiano na taarifa kamili zitatolewa baadaye.

Hata hivyo, Kichere alisema wizi ulitokea katika ofisi hizo ni wizi kama wizi mwingine, na kutoa wito kwa maofisa wa TRA kuwa makini katika kutunza nyaraka za serikali ili kuweka kumbukumbu sahihi za mapato ambayo yanalipwa na walipakodi.

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kueleza kuwa Jeshi la Polisi linamshikilia mlinzi aliyekuwa akilinda ofisini hiyo kwa mahojiano zaidi.

"Tunaendelea na upelelezi ili tutambue ni kwa nini wamevamia na kubomoa dirisha na kuiba nyaraka, fedha, kompyuta mpakato, na upelelezi utakapokamilika na wahusika kubainika tutawafikisha mahakamani mara moja," alisema Kamanda Abwao.




Meneja Bidhaa Kitengo cha EzyPesa cha Zantel, Leonard Kameta (katikati), akiongea kwa simu na mmoja wa washindi wa promosheni ya "Tumia EZYPESA Ushinde" wakati wa droo ya nane iliyofanyika jijini Dar es Salaam, akishuhudiwa na mkaguzi kutoka Bodi ya Taifa ya Michezo ya Kubahatisha, Emanuel Ndaki (kushoto) na Meneja wa Chapa ya Zantel, David Maisori (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT-Wazalendo bila ruzuku miezi 11

**Na Enock Charles**

ZIKIWA zimebaki siku tano tangu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini alipotoa siku 14 kwa chama cha ACT-Wazalendo kujieleza kwanini kisifutiwe usajili wa kudumu, chama hicho kinakabiliana na hali ngumu ya kiuchumi kutokana na kuzuiliwa kwa ruzuku kwa takriban miezi 11 sasa.

Katibu wa Uenezi wa chama hicho, Ado Shaibu, aliiambia Nipashe kuwa ruzuku kwa chama chao imezuiliwa kwa miezi 11 sasa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini kwa maelezo kuwa hakikuwasilisha hesabu zake za mwaka 2013/2014.

"Ni kweli ruzuku yetu ilizuiliwa miezi 11 iliyopita mpaka sasa na sehemu inayoleta ubishi ni hesabu ya mwaka 2013/14 zingine za mwaka 2015/16 na 2016/17 tumepata hati safi ila hiyo ya mwaka 2013/14 ndio inayobishaniwa," alisema na kuongeza:

"Lakini tulipata usajili wa kudumu Mei 5, 2014 na hesabu za mwaka 2013/14 na 2014/15 ziliunganishwa katika ripoti moja baada ya kupata ushauri wa CAG na kumwandikia barua msajili na hayo yote tumeyajibu kwenye barua tuliyompelekea msajili."

Akijibu swali hilo katika kipindi cha moja ya televisheni jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, lililomtaka kueleza watatoa wapi fedha za kuendesha chama hicho, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema chama hicho hupokea ruzuku ya Sh. milioni nne kwa mwezi ambayo kwa sasa imezuiliwa miezi 11 iliyopita.

"Fedha za siasa huwa zinatoka kwa wananchi wenyewe na wananchi ndio wanaotaka mabadiliko na lazima wayagharamie hayo mabadiliko, tutarudi kwao tutawaomba wahakikishe ndoto hii ya kwenda kuleta mabadiliko katika nchi yetu inafanikiwa," Zitto aliongeza.

Akitoa uzoefu wake katika chama cha wananchi (CUF) kuhusu masuala ya kifedha, mwanachama wa ACT Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema kuwa wanachama wao wapo tayari kugharamia shughuli za chama hicho.

"Tuna uzoefu sisi tuliotoka CUF kwenda ACT-Wazalendo, kwa muda mrefu tumezuiwa ruzuku na badala ya kupewa sisi akawa anapewa bwana mkubwa (Prof. Ibrahum Lipumba), lakini hiyo haikuzuia shughuli zetu zisiendelee. Siri yake ni moja tu, tunashirikisha wanachama," Maalim alisema.

Wiki iliyopita Msajili wa Vyama vya Siasa alikiandikia barua chama cha ACT -Wazalendo yenye kumbukumbu namba HA.322/362/20/98 ya Machi 25 akiwapa siku 14 kujieleza kwanini isifutiwe usajili wa kudumu kwa vitendo vya uvunjifu wa sheria ikiwamo kutowasilisha hesabu za ukaguzi 2013/14.

Hata hivyo, Zitto ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini amenukuliwa na gazeti moja nchini akidai amewasilisha barua ya maelezo juzi, yenye majibu ya hoja walizoulizwa na msajili katika ofisi hiyo.

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, hakuweza kupatikana alipotafutwa kujibu iwapo barua hiyo kutoka kwa Zitto imefika katika ofisi yake ama la.

# Shule UDSM yajitathmini

**Na Gwamaka Alipipi**

SHULE Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS) imeanza kujitathmini endapo imetoa mchango wowote wa kulisaidia taifa kwenye sekta ya elimu na uchumi, tangu ilipoanzishwa mwaka 1979.

Hivyo inatarajia kuwaita viongozi wa serikali, waajiri, wafanyabiashara wakubwa, wajasiriamali waliowahi kusoma katika shule hiyo watoe maoni yao kama imefanikiwa kuzalisha wahitimu walioisaidia nchi.

Mkuu wa UDBS, Prof. Ulingeta Obadia, aliyesema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa maandalizi ya maadhimisho hayo na kwamba kilele kitakuwa Septemba mwaka huu.

"Tunaadhimisha miaka 40, mwezi ujao tutawaita waliosoma kwenye shule hii, tutaangalia wapi tumefanya vizuri, kwenye soko la ajira tumetoa mchango gani tangu shule ilipoanzishwa," alisema Prof. Obadia.

Alisema UDBS itajitathmini kwa kujilinganisha na vyuo vingine duniani kama wanafanya vizuri katika kuchangia uchumi wa nchi pamoja na kuwaandaa wahitimu kuja kuwa viongozi wa baadaye.

"Tanzania tulitoka kwenye uchumi wa kilimo na sasa tunaingia kwenye uchumi wa viwanda, hivyo na sisi UDSB hatutaki tuwe watazamaji tunatakiwa kufanya utafiti wa namna gani kuisaidia serikali katika kufanikisha uchumi wa viwanda," alisema Prof. Obadia.

Naye Mhadhiri wa UDBS, Dk. Theresia Dominic, alisema yatakuwa ni maadhimisho ya kuonyesha umuhimu wa kufanya biashara na kufanya utafiti.

Alisema UDBS itatoa semina, makongamano kuhusu namna bora ya Watanzania waweze kufanya biashara, ujasiriamali pamoja na kuisaidia nchi kufanikisha uchumi wa viwanda.

"Tutawaalika waajiri ambao wamewaajiri wanafunzi wetu waliowahi kusoma hapa, na maandalizi yameanza sasa na tutamaliza Septemba mwaka huu, pia tutaonyesha shughuli zetu mbalimbali tunazozifanya," alisema Dk. Dominic.

Alisema kwa kipindi cha miaka 40 tangu kuanzishwa kwa UDBS, mafanikio mengi yamepatikana ambapo kampuni nyingi nchini zinaongozwa na watu waliowahi kuwa wanafunzi wa shule hiyo.

Alisema lengo kuu la UDBS ni kumwandaa mwanafunzi kuwa na umahili katika kuanzisha biashara, wanafunzi wengi wanaomaliza katika shule hiyo wanakuwa na ndoto za kuanzisha biashara zao na siyo kuajiriwa.

## MATANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### CHETI KIMEPOTEA



**MUHSIN KAMALUDIN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.1246/0729** kilichotolewa na MIDLANDS HIGH SCHOOL mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/RB/4912/2017**

115160702


### CHETI KIMEPOTEA



**JOHN P. MTWENA** amepotelewa na cheti cha elimu ya Secondari,alichosomea ktk shule ya secondari AABUY JUMAA.Alichomaliza mwaka 2015.Chenye **index namba S2778-0123.** Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi,Taarifa ya polisi; **MOR/RB/2300/2019.**

215163702

### CHETI KIMEPOTEA



**MAXMILIANI KALUMNA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S:0367-0081** kilichotolewa na KILOSA SEC SCHOOL mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **STK/RB/3019/2019**

115160702

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**

**MAOMBI NA. 39/2018**

**EPHIRAIM HIPPOLITE LYARUU............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**PASCAL CHARLES MOSHI**
**DONATA PASCAL MOSHI**
**EMMANUEL LYIMO..........................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: PASCAL CHARLES MOSHI & DONATA PASCAL MOSHI**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 8/5/2019 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J.Sillas,,hivyo unatakiwa kufika mahakamani nyie au mawakili wenu .
**ANGALIA :** Kama hamtahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 mwezi, April 2019.

215163602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA MAGU MJINI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**

**SHAURI NA. 15/2019**

**CALVERT S. SINDATO..........................................MDAI**
**DHIDI YA**
**JOHN WAZIRI MPANGA......................................MDAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: JOHN WAZIRI MPANGA, WA MTAA WA BENKI, MAGU MJINI**

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Mahakama ya Mwanzo, Magu mjini

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 18/04/2019 saa 2:00 asubuhi kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea.

**Angalia** kama hukuhudhuria siku iliyotajwa, Mahakama itaweza kutoa hukumu.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 05/04/2019.

215163902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAKOYE MADUHU**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina MISTUBISHI yenye namba **T.823 AQR** yenye enjini namba 4D35F82256, Chasis namba **530564**.Yoyote atakayeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya jeshi la polisi, **MBG/RB/891/2019.**

215164302

### MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara magari ya wadaiwa. Ndugu **NAYAZ NIAZIM BHANJI (T 893 DJV TOYOTA MARK X) na Ndugu JOVIN DEODATUS RUTECHURA (T.370 ASY TOYOTA RAV4).** Magari yote yapo katika yard ya Makumbusho. Lengo ni kufidia/kupunguza madeni ya mikopo wanayodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 15/04/2019, mahali dhamana zilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. ***Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi. Raissa Company Ltd: 0652 113 262;*** **Tujijenge: 0718068335/ 0717956315.**

*Kwa Habari Motomoto usikose*

*Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ALLEGRI AKUBALI JUVE KUSHINDA KWA MBINDE

**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri ameelezea namna presha ilivyokuwa kubwa kwa Juventus katika kipindi cha pili wakati wakitoka nyuma kuifunga Milan mabao 2-1 kwenye dimba la Allianz juzi, Jumamosi.

Bao la dakika za mwisho la mchezaji chipukizi, Moise Kean liliiwezesha 'Bianconeri' kupata pointi zote tatu, baada ya Paulo Dybala kusawazisha lile la Milan lililofungwa na Krzysztof Piatek.

Ushindi huo sasa umeifanya Juventus kushinda mechi nane mfululizo kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Allegri aliiambia Sky Sport kwamba, aliridhishwa na kiwango cha wachezaji wake walichokionyesha hasa kwa kuweza kupata bao dakika za majeruhi.

"Ulikuwa ni ushindi muhimu, kama ambavyo mara zote mchezo kati ya Juventus na Milan unavyokuwa mgumu.

"Ilionyesha tunashinda au tunatoka sare. Wachezaji walionyesha kiwango cha kuvutia, hasa kutokana na ukweli kwamba wengi wao hawakucheza kwa muda mrefu.

"Kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri, kwani tulizidiwa, lakini baada ya mapumziko tulijipanga vizuri na kucheza kwa hamasa kubwa zaidi."

# VALVERDE: BARCA HAIJAMALIZA MBIO ZA UBINGWA LA LIGA

**BARCELONA, Hispania**

ERNESTO Valverde amesisitiza kwamba, mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, bado hazijaisha licha ya Barcelona kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Atletico Madrid katika Uwanja wa Camp Nou.

Wageni hao walihitaji kuwapa presha vinara hao kama wangeshinda, lakini mambo yakawa tofauti, huku Diego Costa akitolewa nje kwa kadi nyekundu.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Valverde alisema kwamba jambo la msingi ni kwamba timu yake ilishinda, lakini akasema mbio za ubingwa bado hazijaisha licha ya kubakiwa na mechi saba ligi hiyo kumalizika.

Alisema: "Jambo la msingi ni pointi tatu. Tumekaribia kwenye ubingwa, lakini bado hatujautwaa, tunatakiwa kumaliza kazi ili tuweze kutwaa ubingwa mwishoni mwa msimu, lakini kazi bado.

"Leo (juzi), ilikuwa ni muhimu kushinda kwa sababu ilikuwa na maana kubwa. Hatukuwa na furaha kwa sababu katika kipindi cha pili walikuwa na timu nzuri zaidi na walipigana kuhakikisha wanashinda."

Baada ya kuongeza ushindi kwenye uongozi wake kwenye La Liga, Barcelona sasa itageukia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakiwa wanajiandaa kwenye mchezo wao wa kwanza wa robo fainali dhidi ya Manchester United Jumatano wiki hii.



# Simeone asema Costa alistahili kadi nyekundu

**MADRID, Hispania**



DIEGO Simeone amesifia jitihada za wachezaji wake wa Atletico Madrid, lakini amebainisha kwamba, Diego Costa pengine alistahili kuonyeshwa kadi nyekundu wakati wakifungwa mabao 2-0 na Barcelona katika dimba la Camp Nou.

Kuelekea mchezo huo, Atletico Madrid walikuwa wanahitaji ushindi ili kupunguza gepu la pointi na vinara Barcelona, hata hivyo, mambo yalikwenda tofauti na matarajio wakati Costa alipotolewa nje kwa kadi nyekundu kipindi cha kwanza.

Licha ya kucheza wakiwa 10 uwanjani, Atletico walionekana kama wameikamata Barcelona, lakini katika dakika ya 85, Luis Suarez alifunga bao kwa shuti kali akiwa umbali wa yadi 20.

Na dakika moja baadaye Lionel Messi akaihakikishia pointi zote tatu kwa kufunga bao la pili na kufanya matokeo kuwa 2-0.

Wakati alipoulizwa kuhusu kadi nyekundu ya moja kwa moja ya Costa, Simeone alisema, kama ni kweli, kile ambacho mwamuzi alidai, basi alistahili kutolewa nje ya uwanja.

"Katika mechi 11 tumekuwa na kadi nyekundu saba, inaonyesha kwamba kuna kitu fulani kibaya tumekifanya," alidai.

"Nilimuuliza mwamuzi na aliniambia kitu ambacho Costa hakuniambia. Kuna wachezaji wengine wanasema vitu, lakini hawatolewi nje, lakini hilo haikuwa sababu kwa Diego.

"Kama mwamuzi alitafsiri kile alichoambiwa kuwa ni matusi, hivyo kadi nyekundu alistahili."

# HABARI MICHEZO

## Gattuso alia bahati kuibeba Juventus

**MILAN, Italia**

KOCHA wa AC Milan, Gennaro Gattuso, amedai kuwa timu yake ilionyesha kiwango bora zaidi kwa kipindi cha mwaka huu wakati wakifungwa mabao 2-1 na Juventus juzi, Jumamosi kwenye Uwanja wa Allianz.

Kiungo huyo wa zamani wa Milan amebainisha kwamba licha ya makosa yaliyotokea na kumwezesha Moise Kean kufunga bao la ushindi kwa Juventus katika dakika za mwisho, lakini kikosi chake kilionyesha kiwango bora kabisa.

Rosseneri walikuwa mbele kwa bao la kipindi cha kwanza la Krzysztof Piatek kabla ya Paulo Dybala kusawazisha kwa penalti.

Gattuso ameiambia Sky Sports Italia: "Kilikua kiwango chetu bora kwa mwaka 2019, tulipoteza katika dakika za mwisho 18-20 na si kwa sababu Juve walicheza vizuri, lakini yalikuwa ni makosa yetu.

Mambo kama haya yanatokea wakati unapocheza soka la aina kama tulivyocheza sisi.

"Juve ilibadilika baada ya dakika 20, tulijaribu kutengeneza nafasi zaidi, halafu tukabadili mchezo na kucheza mfumo wa 4-4-2, kiufundi, tulikuwa na mchezo mzuri.

"Tuliwategemea Joao Cancelo na Leonardo Spinazzola kwenye wiga, lakini mwishoni tulijikuta tukitengeneza makosa sisi wenyewe."





# GUARDIOLA:

## HAIWEZEKANI KUSHINDA MATAJI MANNE

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema anaamini uwezekano wa kushinda mataji manne msimu huu ni mgumu, licha ya kuifunga Brighton bao 1-0 na kutinga fainali ya Kombe la FA juzi Jumamosi.

Man City sasa itacheza fainali ya FA kwenye dimba la Wembley, baada ya bao la kichwa la Gabriel Jesus kuipa ushindi huo.

Hii inamaanisha kwamba, matumaini ya City kushinda mataji manne msimu huu ni mkubwa kwa sababu wapo kwenye nafasi nzuri katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Guardiola alisema: "Ni vigumu kushinda mataji manne. Ni miujiza tu itawezesha hilo.

"Mawazo yangu ni kwamba hakuna mtu ambaye amefanya hilo, kwa nini tunaulizwa sisi tu? Kwa uhakika kabisa ni jambo gumu kwa upande wetu, kwani ni vigumu kufanikisha kila jambo."

Manchester City imevunja rekodi nyingi hadi sasa chini ya Guardiola, lakini kama ikifanikiwa kushinda mataji manne msimu huu, yatakuwa mafanikio makubwa zaidi.

Hakuna klabu yoyote ya Uingereza iliyoshinda mataji manne kwa msimu mmoja, lakini wapinzani wao wa jiji moja, Manchester United walikaribia kufikia rekodi hiyo mwaka 1999.




## Zidane bado hajui hatima ya Bale Real

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane alishuhudia timu yake ikirudi kwenye njia ya ushindi baada ya Karim Benzema kuonyesha kiwango kizuri na kuiwezesha timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1 kwenye dimba la Santiago Bernabeu, juzi Jumamosi, lakini alishindwa kuzungumza kuhusu hatima ya mchezaji wake, Gareth Bale.

Benzema alifunga mabao yote mawili katika kipindi cha pili wakati Madrid ikitoka nyuma na kuifunga Eibar iliyopo katikati ya msimamo wa ligi.

Wageni hao walikuwa mbele kwa bao la dakika ya 39 baada ya Real kushinda kuondoa hatari langoni mwao, licha ya kutawala mpira kwa muda mrefu.

Bale alianza kwenye mchezo huo, huku Zidane akitumaini mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales anaweza kuthibitisha uwezo wake na kuendelea kubakia na Madrid kipindi cha majira ya joto kijacho.

Hata hivyo, Zidane mwenye umri wa miaka 46, alishindwa kujibu swali juu ya hatima ya Bale.

Katika mazungumzo yake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, Zidane alisema: "Tutaona hapo baadaye kama Bale bado atabakia kuwa mchezaji wa klabu yetu msimu ujao. Gareth bado ana mkataba wa miaka miwili na Real Madrid, hivyo tunatakiwa kusubiri."

"Kwa sasa ni ngumu kuzungumza hatima yake, lakini jambo la msingi ni kwamba bado ni mchezaji wetu, kama ataondoka baada ya kipindi cha majira ya joto hilo siwezi kulizungumza kwa sasa."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA ATOA ZAWADI 100 ZA ZIDANE LA LIGA

## Akimbiza kwa mabao ya kichwa Ligi Kuu Hispania, Navas naye adaka ya...

**MADRID, Hispania**

KARIM Benzema aliipaisha Real Madrid wakati alipofunga mabao mawili kuiwezesha kupata ushindi wa 2-1 juzi Jumamosi dhidi ya Eibar katika dimba la Santiago Bernabeu.

Huo ulikuwa ni mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, wakati vijana hao wa Zinedine Zidane wakijibu kwa ushindi baada ya kutoka kufungwa Jumatano na Valencia, na Benzema akachagiza ushindi huo katika mechi ya 100 kwa kocha huyo kwenye La Liga.

Madrid walionekana kuimarika zaidi katika dakika za awali na walipata bao dakika ya tisa, lakini kazi ya Benzema kumtengenezea pande Gareth Bale ilionekana kuwa ameotea.

Na wenyeji hao wakajikuta wakiadhibiwa kwa bao la Gonzalo Escalante ambaye aliwapita kirahisi mabeki wa Madrid na kumfunga golikipa, Keylor Navas.

Madrid walipata bao mapema kipindi cha pili, lakini lilikataliwa kupitia teknolojia ya maamuzi ya video (VAR), kwani ilionyesha Benzema aliotea kwa kuwahi kukimbia kabla ya mpira.

Mfaransa huyo alipata bahati nyingine, wakati alipokutana na krosi ya Marco Asensio na kupiga kichwa na mpira ukajaa wavuni moja kwa moja.

Benzema alifunga bao la pili kwa pasi nzuri ya Toni Kroos kutokea winga ya kulia na kuujaza mpira wavuni.

Zidane alikianzisha kikosi kisichozoeleka, huku wanufaika wakuu wakiwa ni Alvaro Odriozola, Nacho Fernandez na Federico Valverde ambao hawapati nafasi ya kucheza mara kwa mara.

Lakini Benzema, Odriozola na Asensio ndio walionekana kuing'arisha zaidi Madrid, huku Luka Modric na Bale wakionekana kutokuwa kwenye kiwango cha juu zaidi.

Ingawa mabao yake mawili yalikataliwa, Benzema bado anastahili kuongoza safu ya ushambuliaji kwa kuwa kiwango chake kinaonekana kuimarika zaidi.

Aliifanya safu ya ulinzi ya Eibar kuwa na kazi ya ziada na hivyo kuonekana kuwa kwenye kiwango kisichoshuka.

**Mambo muhimu**

- Zidane ni kocha wa saba kuiongoza Real Madrid katika mechi 100 katika historia ya La Liga, akishinda kwa asilimia 71 kati yao.
- Hakuna mchezaji kwenye La Liga aliyefunga mabao mengi zaidi kwa kichwa katika mashindano yote msimu huu zaidi ya Benzema akiwa amefunga mabao tisa.
- Keylor Navas alidaka mechi ya 100 La Liga kwa Madrid, akiwa mchezaji wa kwanza ambaye si Mhispania kufikisha mechi hizo kwa Los Blancos hao.

## KWA UFUPI

### LEWANDOWSKI, CHELSEA WATETA

CHELSEA imefanya mawasiliano na mawakala wa mshambuliaji wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski, 30, huku pia ikivutiwa na straika wa Borussia Dortmund na Sweden, Alexander Isak, 19. ***(Sunday Mirror)***

### POGBA, DE GEA SHAKANI UTD

KIUNGO wa Ufaransa Paul Pogba, 26, na kipa wa Hispania, David de Gea, 28, ni sehemu ya wachezaji wa saba wa Manchester United wanaofikiria kuachana na klabu hiyo wakati huu ikihaha kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Sunday Times)***

### ROBBEN KUTIMKIA MAREKANI

WINGA wa Bayern Munich na Uholanzi, Arjen Robben, 35, atakataa kujiunga na Inter Milan ili kutoa upendeleo wa kutimkia Ligi Kuu ya Marekani, MLS. ***(Calciomercato)***

### PICKFORD, OBLAK KUMRITHI DE GEA

KIPA wa Everton, Jordan Pickford, 25, na wa Atletico Madrid, Jan Oblak, 26, wapo katika orodha ya wanaowindwa na Manchester United endapo itampoteza David de Gea, ambaye anawindwa na PSG. Kipa huyo wa kimataifa wa England, Pickford anaweza kuwagharimu hadi pauni milioni 60, wakati Mslovenia Oblak anaweza kuwagharimu ada itakayoweka rekodi ya dunia. ***(Sunday Express)***

### NEYMAR AJUTA KUONDOKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Neymar, 27, "anajuta kuliko kawaida" kuondoka Barcelona, amesema mchezaji wa zamani wa Barca na mchezaji mwenza wa Brazil, Adriano. (Cadena Ser)

### NDOMBELE AZIVUTIA, UTD, PSG

KIUNGO wa Lyon, Tanguy Ndombele anawindwa na Manchester United, lakini itakumbana na vita kali kutoka kwa PSG kwa Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(L'Equipe - in French)***

### DEPAY KUMRITHI MANE LIVER

Liverpool inaweza kumfuata mshambuliaji wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay, 25, kama winga Msenegal Sadio Mane, 26, ataondoka Anfield majira haya ya joto. ***(L'Equipe, via Mail on Sunday)***

### TRIPPIER KUMPISHA WAN-BISSAKA

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino anapanga kuziba pengo la beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, 28, kwa kumsajili beki wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21. ***(Sunday Express)***

### SARRI AMTAKA GIROUD KUBAKI

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, anataka mshambuliaji Mfaransa Olivier Giroud kubaki klabuni hapo. Mkataba wa straika huyo mwenye umri wa miaka 32, unamalizika Juni lakini klabu hiyo ya Stamford Bridge ina uamuzi wa kuongeza kwa miezi 12. (Star on Sunday)

### MITROVIC AGEUKA LULU EPL

Leicester City imejiunga katika mbio moja na Everton, Southampton, Tottenham na West Ham za kumsajili straika Mserbia Aleksandar Mitrovic, 24, kutoka Fulham kufuatia miamba hiyo ya Craven Cottage kuwa katika nafasi ya kushuka daraja. ***(Sportski Zurnal, via Leicester Mercury)***

### SESSEGNON KUSHUKA NA FULHAM

WINGA wa Fulham, Ryan Sessegnon, 18, atamalizia mwaka wake mmoja uliobaki klabu hiyo katika kinyang'anyiro cha Ligi Daraja la Kwanza ['Championship'] msimu ujao na kisha kujiunga na Borussia Dortmund, ambayo italipa tu fidia ya ada ya kujifua kwa nyota huyo wa kimataifa wa England U-21. ***(Sun on Sunday)***

### MTOTO WA 'DINHO' ASAINI CRUZEIRO

MTOTO wa nguli wa Brazil, Ronaldinho, Joao Mendes, 14, amesaini mkataba wa miaka mitano wa kuichezea Cruzeiro. Mendes amekuwa akiitumikia klabu hiyo tangu mwaka jana. ***(Cruzeiro - in Portuguese)***

### MEUNIER AWINDWA UNITED

Manchester United inamfuatilia beki wa kulia wa PSG na Ubelgiji, Thomas Meunier, 27, tangu kuanza kwa msimu. ***(Sun on Sunday)***

HABARI MICHEZO

# IVO MAPUNDA ATOA RAI CASTLE LAGER AFRICA 5S

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Castle Lager Africa 5s nchini Tanzania, Ivo Mapunda, amewaomba wamiliki wa baa kuunda timu bora za kiushindani zitakazoziwakilisha vema kwenye fainali ya Bonanza kubwa itakayoshirikisha timu 32 kutoka baa tofauti za jijini Dar es Salaam na kupata timu moja itakayowakilisha Tanzania kwenye mashindano hayo ngazi ya Afrika yanayotarajiwa kufanyika nchini baadaye mwaka huu.

Mapunda aliyasema hayo jana kwa waandishi wa habari wakati akijiandaa rasmi na ziara ya kutembelea baa 60 za jijini Dar es Salaam zilizoingia kwenye mchakato wa kiushindani kupitia promosheni zinazoendelea kwenye baa hizo na kuwaomba wamiliki hao wajitahidi kuunda timu bora.

Alisema ushindani unatarajiwa kuwa mkubwa kwenye mashindano hayo ya soka yanayoshirikisha wachezaji watano kila upande, kabla ya mwisho wa siku kutoa timu moja itakayoiwakilisha Tanzania katika mashindano hayo ngazi ya Afrika yanayotarajiwa kufanyika nchini kwa mara ya kwanza, lakini ikiwa ni mara ya pili kwa Tanzania kushiriki chini ya udhamini wa Kampuni ya Bia nchini (TBL) kupitia bia yake ya Castle Lager.

"Nawasihi wamiliki wa baa shiriki tutambue bingwa wa fainali ya bonanza atatuwakilisha Watanzania wote na kwa maana hiyo, uundaji wa timu zetu na maandalizi kwa ujumla unapaswa kuwa mzuri," alisema Balozi wa Castle Lager Tanzania, Mapunda na kuongeza:

"Mwaka jana tulishiriki mashindano haya kwa mara ya kwanza na kupata mwakilishi aliyeshiriki katika michuano ya kimataifa ya Afrika, yaliyofanyika nchini Zambia kwa kuzikutanisha timu za Afrika Kusini, Zimbabwe, Swaziland Lesotho na wenyeji Zambia.

"Binafsi niwapongeza sana wadhamini wa mashindano haya, Castle Lager kwa kudhamini mashindano haya ambayo yanawapa fursa wanywaji wao kushiriki michezo ambayo mwisho wa siku inatupa nafasi ya kuitangaza nchi yetu ya Tanzania, lakini pia niwashukuru sana kwa kuniona mimi kama nastahili kuwa Balozi wa Castle Lager Africa 5s nchini Tanzania.

"Nafahamu mchakato wa kupata timu zitakazoshiriki katika bonanza hilo umeboreshwa zaidi mwaka huu, ambapo washiriki watapatikana kupitia katika promosheni zinazoendelea katika baa mbalimbali jijini Dar es Salaam."

Ili kuingia 32 bora, moja ya kigezo muhimu ni kufanya mauzo mengi ambapo kutakuwa na makasha maalumu katika baa husika kwa ajili ya kukusanyia vizibo baada ya mteja kununua bia ya Castle Lager.




Meneja wa Bia ya Castle Lager, Pamela Kikuli (kulia), akimkabidhi Balozi wa Castle Lager Africa 5s, Ivo Mapunda mpira kuashiria uzinduzi wa mashindano ya Castle Lager Africa 5s (ya wachezaji watano watano) yanayotarajiwa kufanyika nchini mwaka huu.
**MPIGAPICHA WETU**

# Twiga Stars waahidi 'kufia' uwanjani kesho

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake (Twiga Stars), kimetua salama jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), huku wachezaji wakiahidi kutomwangusha Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye alikwenda kuwaaga na kuwatakia mafanikio katika mchezo wao wa marudiano.

Mbali na kuwaaga, Mama Samia aliwapa wachezaji hao Sh. milioni tano na kuwaambia wachezaji wa Twiga Stars kwamba wasikate tamaa, kwa kuwa uwezo wa kuwafunga wapinzani wao wanao.

"Wakongo wanatushinda katika muziki tu, katika soka hawatuwezi, nendeni mkafanye vizuri, mkifanya vema nitaenda kwa baba (Rais John Magufuli) kuwaombea zawadi kama walizopata wenzenu (Taifa Stars), Dodoma itawahusu," alisema Makamu wa Rais juzi, Jumamosi alipokuwa anazungumza na wachezaji hao wa Twiga Stars.

DRC kesho inatarajiwa kuwakaribisha Twiga Stars katika mchezo wa marudiano wa kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha na mshambuliaji mkongwe wa Twiga Stars, Asha Rashid, alisema wamejiandaa kupambana na mechi ya kesho haitakuwa ngumu kama ya awali kwa sababu wameshawafahamu.

Asha alisema pia wameshayafanyia kazi marekebisho ya makosa waliyofanya katika mchezo uliopita na kesho wataingia uwanjani ili kusaka ushindi.

"Tulitamani kushinda katika mechi ya kwanza, lakini mambo hayakuwa mazuri, ndio mpira, lakini mechi ya Jumanne tutaingia tukiwa imara zaidi, naamini kila mmoja wetu anajua hii ni sawa na fainali, hatutakubali kushindwa," alisema nahodha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, alisema wamejipanga kuendelea pale walipoishia na hilo linawezekana kwa kikosi chake ambacho kinashikilia ubingwa wa Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Shime alisema kuwa timu yake imeshacheza mechi ngumu zaidi na kama watakuwa makini, nafasi ya wao kusonga mbele katika mashindano hayo ni kubwa.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2.

# Kuogelea kuwania ubingwa wa Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

Jumla ya klabu 10 zimethibitisha kushindana katika mashindano ya Klabu Bingwa ya mchezo wa kuogelea yaliyopangwa kufanyika kwenye bwawa la kuogelea la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), Upanga jijini Dar es Salaam kuanzia Aprili 13 hadi 14, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Hadija Shebe, ameliambia gazeti hili kuwa klabu 10 zitakazoshiriki ni Bluefins, Champion Rise, Mis Piranhas, Klabu ya Kuogelea ya Mwanza (MSC), FK Blue na Wahoo ya Zanzibar.

Hadija alizitaja klabu nyingine zitakazoshiriki mashindano hayo ambayo yamedhaminiwa na Kampuni za Asas, Samsung, DTB Bank, Snow Cream, Knight Support na Kituo cha Utangazaji cha Clouds FM, kuwa ni ISM-Moshi, ISM-Arusha, FK Blue Marlins, Talis-IST na mabingwa watetezi, Dar es Salaam Swim Club (DSC).

Alisema mashindano hayo yamepangwa kuanza saa 2:00 asubuhi siku ya Jumamosi na waogeleaji watashindana katika staili tano ambazo ni Freestyle, Breaststroke, Butterfly, Backstroke na Individual Medley.


Hadija alisema waogeleaji hao pia watashindana katika mashindano ambayo yamepitishwa na Shirikisho la Mchezo wa Kuogelea duniani (Fina), kuwa ya kutafuta alama za kufuzu mashindano ya dunia yaliyopangwa kufanyika nchini Korea Julai mwaka huu.

**"Tunatarajia kuona ushindania mkali kwa waogeleaji wetu ili kutafuta nafasi ya kufuzu mashindano ya dunia. Waogeleaji wengi wapo katika maandalizi ya mwisho mwisho kwa ajili ya mashindano hayo, bado tunahitaji wadhamini wa mashindano haya," alisema Hadija.**

# Michezo

Jumatatu Aprili 8, 2019

Nipashe



Benzema atoa zawadi 100 za Zidane La Liga

HABARI UK 30

TUTA?...




Beki wa Kati wa Everton, Kurt Zouma, akiepuka kusababisha penalti licha ya kumgusa kwenye kifundo cha mguu mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Goodison Park na wenyeji kushinda 1-0 kupitia kwa Phil Jagielka. **PICHA: DAILY MAIL**

# AUSSEMS: MAZEMBE HAWATAAMINI CONGO

●●● Afurahia sare tasa, asema lolote linaweza kutokea Jumamosi na kwamba Simba...

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikilazimishwa sare tasa na TP Mazembe Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema timu yake bado iko katika nafasi salama ya kutinga nusu fainali ya mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo yataendelea Jumamosi wiki hii.

Timu hizo zinatarajiwa kurudiana Aprili 13, mwaka huu jijini Kinshasa na mshindi atatinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems alisema anaamini kila timu inahitaji ushindi ili iweze kusonga mbele, lakini kikosi chake ambacho hakikupewa nafasi ya kufika hatua hiyo kinaweza kuendelea kufanya kile kisichotarajiwa.

Aussems alisema sare ya bila kufungana ni nzuri na bado hawajakata tamaa ya kusonga mbele katika mashindano hayo.

"Haya ni mashindano makubwa na magumu katika kila hatua, naamini bado nafasi tunayo ya kushinda na kuendelea mbele, hakuna ambaye alijua kama tutafika hapa, kuna changamoto nyingi, lakini bado tunapambana nazo, tunahitaji matokeo chanya," alisema Aussems.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa kuumia kwa beki wake, Pascal Wawa katika dakika za mapema kulivuruga mipango yake, lakini anaamini hali hiyo ni sehemu ya mpira.

Naye Rais wa Simba, Swedi Mkwabi, alisema kuwa matokeo ya sare waliyopata juzi hawakuyatarajia, lakini wamekubaliana nayo kutokana na kuuheshimu mchezo huo.

"Na kama suala la kukosa penalti, hili ni la kawaida, anakosa Messi (Lionel) mwenye mpira wake, itakuwa Bocco (John), tunaenda Congo kumalizia kazi tuliyoifanya Taifa, uwezo wa kuwafunga tunao, naamini hilo, " alisema kiongozi huyo.

**...YASAKA UWANJA**

Katika hali isiyo ya kawaida, Mkwabi, alisema hawana uhakika kama watacheza mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting iliyopangwa kuchezwa Jumanne kutokana na kukosa uwanja.

Kiongozi huyo alisema kuwa Uwanja wa Jamhuri, Morogoro ambao wameuchagua hauko katika hali nzuri na endapo watacheza, wanaweza kuhatarisha afya za wachezaji wao, wakati wanakabiliwa na mchezo wa marudiano dhidi ya TP Mazembe ndani ya siku chache.

"Kama tutakosa uwanja na kushindwa kucheza Jumanne, basi tutakuwa na ratiba ngumu, mechi 11 ndani ya siku 23, hii itakuwa bandika bandua," alisema Mkwabi.

Simba imekuwa na viporo vingi kutokana na kubanwa na mashindano hayo ya kimataifa wanayoshiriki.

# Yanga yaichambua African Lyon ikiisubiri leo

**Na Mwandishi Wetu**

UKURASA mpya! Kocha Msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, amesema kikosi chao kinaikaribisha African Lyon katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, kikifikiria kuongeza pointi nyingine.

Mwandila aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wake wako tayari kwa mechi hiyo licha ya kukosa muda mzuri wa maandalizi kutokana na kubanwa na safari ya kutoka Mtwara.

Kocha huyo alisema wataingia uwanjani wakiwa wanawaheshimu wapinzani wao, hasa kutokana na nafasi waliyopo mkiani katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.

"Tumetumia siku mbili kwa ajili ya safari, hatukupata muda mzuri wa kujiandaa, lakini tuko tayari kwa mchezo huu, wachezaji wanajua kile tunachokitafuta, tunahitaji kupata pointi tatu katika mechi hiyo ya kesho (leo)," alisema Mzambia huyo ambaye awali alikuwa chini ya George Lwandamina.

Alisema habari kuhusu mchezo uliopita ambao walitoka sare na Ndanda FC wameshaumaliza na sasa wamefungua "ukurasa mpya" ambao wanauangalia mchezo dhidi ya African Lyon tu.

"Habari ya Ndanda tumeshaifunga, sasa tunaangalia ukurasa mpya, tunajiandaa na mechi ya African Lyon ambayo tutacheza hapa CCM Kirumba," aliongeza.

Beki wa timu hiyo, Juma Abdul, alisema kuwa wamejiandaa vizuri na wanawaheshimu wapinzani wao African Lyon.

"African Lyon ni timu nzuri, si mbovu, timu yoyote inayoshiriki Ligi Kuu ni nzuri, akili yetu na mawazo yetu yanaufikiria mchezo huo, tumejipanga kupambana na tusiingie uwanjani katika hali ya kuwadharau," alisema Abdul.

Yanga yenye pointi 68 ndio inaongoza msimamo wa ligi ikifuatiwa na Azam FC wenye pointi 63, lakini Wanalambalamba hao wakiwa mbele mechi moja wakati Simba iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 57 na imeshuka dimbani mara 22 tu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >